

**UCHANGANUZI WA UMILISI WA KIISIMU WA WANAFUNZI WA LUGHA YA
KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA MASENO NCHINI KENYA**

NA

JAIKA PATRICK

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA

NDAKI YA MASENO

© 2017

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu kingine.

Jaika Patrick..... Tarehe.....

PG/MA/051/2008

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa mtahiniwa.

Prof. Florence Indede Tarehe.....

Chuo Kikuu cha Maseno, Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika.

Prof. Ernest Mohochi..... Tarehe.....

Chuo Kikuu Cha Rongo, Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi.

SHUKRANI

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu, baada ya kujitosa baharini na kupiga mbizi hadi nikafika ufuoni. Natoa shukrani zangu kwa wasimamizi wangu Prof. Florence Indede na Prof. Ernest Mohochi na bila kumsahau Dkt. Asiko Ambuyo na Dr. Debora Nanyama kwa hakika mliweza kuniongoza na kunielekeza ili nisizame baharini. Kila wakati mlikuwa tayari kunishika mkono na kunionyesha mbinu za kuepukana na mawimbi na vizingiti katika safari hii. Ingawa safari ilikuwa ngumu mliifanya kuwa rahisi. Pia nawashukuru wanaidara wote wa Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Maseno walionihimiza kuweza kujitosa na kuikabili bahari. Namshukuru mwanafunzi mwenzangu Florence Mutekwa kwa kunihimiza katika safari hii. Mwisho nawashukuru wote ambao singeweza kuwataja kwa majina kwa jitihada na uvumilivu wao, Mola awabariki.

TABARUKU

Naitabarukia kazi hii mke wangu Violet na wanangu Mose, Khadasia na Brenan kwa ku-
niunga mkono wakati wa kuandika tasnifu hii.

IKISIRI

Utafiti huu umechochewa na hali kuwa, asilimia kubwa ya masomo ya isimu katika lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu nchini Kenya yanaathiriwa na matumizi ya istilahi mbalimbali za kiisimu zinazotumiwa na wataalam katika ufunzaji na ujifunzaji wa isimu. Hali hii inatunga kunawiri kwa umilisi wa kiisimu na kuathiri kiwango cha ukuaji wa umilisi wa Kiswahili. Lengo kuu la utafiti ni kuchunguza umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa somo la isimu katika Chuo Kikuu cha Maseno. Madhumuni ya utafiti ni: kuchunguza viwango vya umilisi wa kiisimu vya wanafunzi wa somo la Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno, kuchanganua vipengee vinavyoeleza badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili, kueleza athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili na kufafanua changamoto ambazo wanafunzi na wahadhiri wa isimu hukumbana nazo wakati wa ufunzaji wa umilisi wa kiisimu katika Chuo Kikuu cha Maseno. Nadharia ya Umilisi wa Kiisimu ya Lehmann na ya Motisha na Mielekeo katika kujifunza lugha ya pili ya Gardner zimetumiwa katika uchunguzi huu. Utafiti umejikita katika Chuo Kikuu cha Maseno idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika kwa sababu isimu inafunzwa katika vyuo vingi nchini Kenya na matokeo ya utafiti yangewasilisha vyuo vile vingine. Pia ni mojawapo wa sehemu ambazo zingetoa data ya utafiti huu. Muundo wa mkingamo umetumiwa katika utafiti huu. Sampuli ya kishada imetumiwa kuchagua wanafunzi wa mwaka wa kwanza na mwaka wa nne, nao uteuzi maksudi imetumiwa kuchagua wanafunzi sitini na sita kutoka mwaka wa kwanza na hamsini na tano kutoka mwaka wa nne. Vilevile sampuli ya ujaji imetumika ambapo wahadhiri watatu wamechanguliwa kushiriki katika utafiti huu. Data imekusanywa kupitia usaili, hojaji na jarabati. Utafiti majaribio umefanywa kupima uhalali wa vifaa vya utafiti. Data imewasilishwa na kuchanganuliwa kiwingi idadi na kimaelezo kufuata madhumuni ya utafiti. Utafiti huu imebainisha kuwa wanafunzi wanapoingia chuoni huwa na umilisi wa viwango tofauti vya umilisi wa lugha ya Kiswahili. Vilevile vipengee vinavyooyesha badiliko la umilisi wa kiisimu vimebainishwa. Utafiti umebainisha athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili Chuoni Maseno. Mwisho, utafiti umeeleza changamoto ambazo wanafunzi na wahadhiri wanakumbana nazo wakati wa ujifunzaji na ufunzaji wa isimu katika lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa sababu, kuelewa isimu kutaimarisha umilisi wa wanafunzi katika lugha ya Kiswahili na hivyo kuwafanya wawe wasemaji bora wa lugha hii ya Kiswahili. Utafiti unapendekeza kuwa mabadiliko yafanywe katika mbinu za kufundisha isimu ya Kiswahili ili kurahisisha istilahi ngumu. Aidha, utafiti unapendekeza kuwa uchunguzi zaidi ufanywe kuhusu njia mbadala za kupima umilisi wa kiisimu. Vilevile utafiti zaidi ufanywe kuhusu athari za lugha za kwanza kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili vyaoni.

ABSTRACT

The research has been kindled by the fact that a big percentage of linguistics studies in Kiswahili in the Kenyan universities is affected by the use of different linguistic vocabularies used during the teaching and learning process. The situation has diminished the growth of linguistics competence and affected the level of competence among Kiswahili learners. This research aims at analyzing the linguistic competence of Kiswahili students at Maseno University. The objectives of the research were to identify the level of linguistic competence of Kiswahili learners at Maseno University, to evaluate the main cause of linguistic competence change of Kiswahili learners, to indentify the effects of sheng' on competence of linguistics in Kiswahili language and to identify the challenges that are faced by the lecturers and learners in their linguistic classes in Maseno university. This study is based on the theories of Linguistic Competence by Lehmann and Motivation and Attitudes in learning second language by Gardner. Maseno University has been chosen because linguistics in Kiswahili is taught in all universities in Kenya and the results of the research would represent other universities. Also the area would give the required data. The study employs a cross-sectional research design. Cluster sampling was used to select first and fourth year students. Purposive random sampling was used to select sixty six first year students and fifty five fourth year students. Judgmental sampling was used to select three lecturers who took part in the study. Data was collected using, interviews, questionnaires and examination. A pilot study was conducted to test the reliability of the instruments of the study. Data was presented and analyzed qualitatively and quantitatively by establishing analytical categories from statements of respondents. The study finds out that when students enter the university they have low linguistic competence in Kiswahili. The study highlights the indicators that show linguistic change in Kiswahili students and the effects of sheng' on linguistic competence in Kiswahili language. Lastly, the study analyzes the challenges faced by the students and lecturers in the teaching and learning process. The findings are important in that the linguistics learned will be able to improve the student's competence in Kiswahili and therefore make them better speakers of the Kiswahili language. The study recommends that changes be made on the mode of teaching of linguistics in Kiswahili so as to ease the vocabularies used, the study recommends that more be done on alternative ways of measuring linguistic competence and the study also recommends that more research be done on effects of first languages on Kiswahili linguistics.

YALIYOMO

JALADA.....	i
IKIRARI.....	ii
SHUKRANI.....	iii
TABARUKU.....	iv
IKISIRI.....	v
ABSTRACT.....	vi
YALIYOMO.....	vii
VIFUPISHO.....	xi
UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU.....	xii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xiii
VIAMBATISHO.....	xiv
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI.....	1
1.1. Utangulizi	1
1.2. Usuli	1
1.3. Suala la utafiti.....	5
1.4. Maswali ya utafiti.....	6
1.5. Madhumuni ya utafiti.....	6
1.6. Umuhimu wa utafiti.....	7
1.7. Upeo wa utafiti.....	8
1.8. Sababu za kuchagua mada ya utafiti.....	9
1.9. Misingi ya nadharia ya utafiti	9
1.9.1. Nadharia ya Umilisi wa Lugha.....	10
1.9.2. Nadharia ya Motisha na Mielekeo ya Kujifunza Lugha ya pili.....	12
1.9.3. Upimaji wa umilisi.....	14
1.9.3.1. Vigezo vya kupima umilisi wa kiisimu.....	15
1.10. Hitimisho la sura.....	16
SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI.....	17

2.1. Utangulizi.....	17
2.2. Umilisi wa kiisimu.....	17
2.2.1. Umilisi wa mawasiliano.....	20
2.2.2. Umilisi wa usemaji.....	21
2.2.3. Kupima umilisi wa lugha	22
2.3. Tafiti kuhusu umilisi wa kiisimu wa lugha.....	23
2.3.1. Vipengee vinavyoonyesha badiliko la kiisimu.....	27
2.3.2. Athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu	29
2.3.3.Changamoto za umilisi wa kiisimu katika lugha	31
2.4. Dhana na ujenzi wa mielekeo.....	35
2.4.1. Mielekeo kuhusu lugha	36
2.4.2. Tafiti kuhusu mielekeo ya lugha	36
2.5. Historia ya ufundishaji wa Kiswahili katika Vyuo Vikuu nchini Kenya.....	42
2.6. Pengo la utafiti.....	43
2.7. Hitimisho la sura.....	43
SURA YA TATU: NJIA NA MBINU ZA UTAFITI.....	45
3.1. Utangulizi.....	45
3.2. Muundo wa utafiti.....	45
3.2.1. Mbinu ya kithamano.....	45
3.2.2. Mbinu ya kiwingi idadi.....	46
3.3. Eneo la utafiti	47
3.4. Kundi lengwa.....	48
3.5. Sampuli na usampulishaji.....	48
3.5.1. Sampuli ya utafiti.....	48

3.5.2. Mchakato wa utafiti.....	49
3.6. Utafiti majaribio.....	50
3.7. Udabiti wa vifaa vya utafiti.....	51
3.8. Mbinu ya utafiti.....	51
3.8.1. Mbinu za ukusanyaji data.....	51
3.8.1.1. Usaili.....	52
3.8.1.2. Hojaji.....	53
3.8.1.3. Jarabati ya mwaka wa nne.....	53
3.8.1.4. Upimaji wa umilisi	54
3.8.2. Mbinu za kuchanganua data.....	55
3.9. Maadili katika utafiti.....	56
3.10. Hitimisho la sura.....	56
SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA.....	57
4.1. Utangulizi.....	57
4.2. Kuchanganua viwango vya umilisi.....	58
4.2.1. Viwango vya kisiimu.....	58
4.2.2. Alama za KCSE katika somo la Kiswahili.....	58
4.2.3. Matokeo ya jarabati.....	62
4.3. Vipengee vinavyoonyesha badiliko la kiisimu.....	67
4.3.1. Majibu ya watafitiwa.....	67
4.4. Athari za sheng’.....	71
4.4.1. Matokeo ya watafitiwa.....	71
4.4.2. Athari za Kiisimu.....	71
4.4.2.1. Athari za kifonolojia	72

4.4.2.2. Athari za kimofolojia.....	73
4.4.2.3. Athari za Kisintaksia.....	74
4.4.2.4. Athari za kisesantiki.....	76
4.4.2.5. Athari za kimsamiati.....	78
4.5. Changamoto za wanafunzi na wahadhiri.....	80
4.5.1. Majibu ya watafitiwa.....	80
4.5.2. Changamoto za kiisimu.....	81
4.5.3. Changamoto zisizo za kiiisimu.....	82
4.6. Jinsi wahadhiri na wanafunzi hukabiliana na changamoto.....	86
4.6.1. Majibu ya watafitiwa.....	86
4.7. Hitimisho.....	87
SURA YA TANO: MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	89
5.1. Utangulizi.....	89
5.2. Muhtasari wa utafiti.....	89
5.3. Matokeo ya utafiti.....	90
5.3.1. Viwango vya umilisi.....	91
5.3.2. Vipengee vya kupima umilisi	91
5.3.3. Athari za lugha nyingine kwa umilisi	92
5.3.4. Changamoto wanazokumbana na nazo.....	93
5.4. Mahitimisho kulingana na madhumuni.....	93
5.5. Mapendekezo ya utafiti zaidi.....	97
Marejeleo.....	98
Viambatisho.....	107

VIFUPISHO

CKM.....	Chuo Kikuu cha Maseno
AU.....	Afrika Union
L2	Lugha ya pili
KCSE.....	Kenya Certificate of Secondary Education
KN.....	Kundi Nomino
KT.....	Kundi Tenzi
S1.....	Sentensi ya kwanza
S2.....	Sentensi ya pili

UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU

Umilisi wa lugha: Ufasaha au uwezo wa kutumia lugha vilivyo.

Isimu: Sayansi ya lugha.

Umilisi wa kiisimu: Ni uwezo wa mzungumzaji kuweza kuunda na kutumia sentensi kwa kufuata misingi ya kisarufi iliyowekwa na lugha hiyo. Vilevile uwezo wa mzungumzaji kutambua makosa katika sentensi za lugha husika.

Matumizi ya isimu katika utafiti. Umilisi wa kiisimu katika lugha kulingana na utafiti huu ni vile vigezo vya kiisimu au sarufi ambavyo hupatikana katika zile stadi nne za lugha. Utafiti huu ulitumia umilisi kama uwezo wa mtu kutumia lugha akifuata sheria zote za kisarufi bila kufanya makosa.

Mielekeo: Hali ya kupenda au kuchukia kitu au mtu, kupenda kuzungumza lugha.

Mielekeo ya umilisi wa isimu ya lugha: Hali ya kupenda au kuchukia sayansi ya lugha.

Mielekeo chanya: Kigezo cha kupenda kitu ijengwayo kwa muda katika hisia.

Mielekeo hasi: Kigezo cha kuchukia kitu, ijengwayo kwa muda katika hisia za binadamu.

Jinsia: Kigezo cha kuwa mwanamke au mwanamme kibayolojia.

Mielekeo kijinsia: Kigezo cha kupenda au kuchukia mume au mke.

Uchanganuzi: Kupima kwa kutumia hatua maalum kulingana na utafiti huu uchanganuzi ni vile vifaa, mbinu au hatua zilizochukuliwa na mtafiti katika kukusanya na kuchanganua habari kama ilivyopatikana nyanjani.

Motisha: Ari, azma au hamu ya kufanya jambo.

Jarabati: Mitihani au vigeu vya kupima umilisi wa kiisimu.

Marafukizi: Hesabu ya wahojiwa waliosailiwa na kutoa jibu moja.

ORODHA YA MAJEDWALI.

Jedwali 1. Idadi ya sampuli ya waliotafitiwa.....	49
Jedwali 2. Alama za KCSE.....	61
Jedwali3. Matokeo ya Jarabati	62
Jedwali 4. Athari za kiisimu.....	72

VIAMBATISHO

Kiambatisho 1. Saili ya wahadhiri.

Kiambatisho 2. Saili ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza.

Kiambatisho 3. Hojaji ya mwaka wa nne

Kiambatisho 4. Jarabati ya wanafunzi ya mwaka wa nne.

Kiambatisho 5a. Matokeo ya jarabati ya mwaka wa nne

Kiambatisho 5b. Muhtasari wa matokeo ya wavulana.

Kiambatisho 5c. Kibali cha kushiriki utafiti

Kiambatisho 6. Mwongozo wa kusahihisha jarabati ya wanafunzi.

Kiambatisho 7. Baadhi ya karatasi za jarabati.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1. Utangulizi

Sura hii inaangazia usuli, ufafanuzi kuhusiana na msingi wa mada ya utafiti, maswali yanayoongoza utafiti huu yameorodheshwa na swala la utafiti limengaziwa. Aidha madhumuni ya utafiti huu, upeo wake, umuhimu wake na misingi ya uteuzi wa mada umebainishwa. Mwisho inashughulikia nadharia za utafiti.

1.2. Usuli

Viwango vya umilisi katika lugha yoyote ile huweza kukadiriwa kwa namna nyingi. Mwanaisimu Chomsky (1965) alizua dhana ya umilisi wa lugha. Kulingana naye, umilisi wa lugha ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kufahamu vyema sheria za kiisimu za lugha anayozungumza. Sheria hizi ni kama vile: Kufahamu kuhusu leksia, fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ya lugha husika. Mbali na kuzifahamu sheria za lugha, mzungumzaji anafaa kuwa na ule uwezo wa kutumia lugha ipasavyo.

Mtalaam Newmark (1966) aliyaunga mawazo haya mkono kwa kudokeza kuwa, kumiliki sheria za kimsingi za lugha, umilisi wa usemaji, umilisi wa isimujamii kati ya mengine mengi ni baadhi ya mambo ambayo mtu lazima ajue ili aweze kuwa na umilisi wa kiwango cha wastani au cha juu. Naye Stern (1983) anadai kuwa viwango vya umilisi katika lugha yoyote ile huwa tofauti kulinga na usemaji wa lugha hiyo. Ili isemekane kuwa mtu ana umilisi wa kiwango cha juu cha kiisimu katika lugha, sharti mtu huyo awe na uwezo wa kuunda maneno na sentensi katika lugha hiyo. Vilevile
aweze kuitumia lugha hiyo ipasavyo katika matumizi ya kila siku na stadi nne za lugha ambazo ni: Kusoma, kusikiliza, kuzungumza na kuandika.

Mawazo haya yanaungwa mkono na Richard na Rodgers (1986) wanaosema kuwa mtu kuwa na kiwango fulani cha lugha sio lazima amiliki sheria za lugha pekee bali aweze kutumia sheria hizo katika utendaji (yaani katika mazungumzo na maandishi). Utafiti huu unafanywa katika eneo la wingi lugha ambapo lugha za kwanza ni nyingi mno. Wanafunzi wanapojiunga na chuo huwa na viwango tofauti vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo viwango hivi tofauti havijulikani bayana na ni vipi viwango hivi huathiri umilisi wao wa lugha ya Kiswahili. Utafiti kuhusu viwango hivi katika Chuo Kikuu utawapa wahadhiri, wataalam wengine na wakuza mitaala habari muhimu ambayo itawawezesha kutafuta njia na mbinu za kuimarisha ufundishaji wa umilisi wa Kiisimu katika uandishi wa kiakademia miongoni mwa wanafunzi wa somo la kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

Mwanaisimu Carell (1989) anasema kuwa, mtu anayefahamu lugha na kuwa na umilisi wa kiisimu katika lugha hiyo huonekana kuwa na ufunguo wa kufanikiwa katika masomo yake ya kiakademia. Naye Adams (1993) anaeleza kuwa kusoma na kuzungumza ni stadi muhimu kwa kupata masomo ya juu ya kiakademia. Stadi hizi hufuatwa na kusikiliza na kuandika. Hata hivyo uandishi wa kiakademia katika isimu huwa swala lenye kuleta utata miongoni mwa wanafunzi. Hali hii ni kwa sababu ya mielekeo yao hasi kuhusu isimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo utafiti huu una nafasi ya kuwapa motisha watumiaji wa lugha ya Kiswahili wa viwango tofauti katika Chuo Kikuu cha Maseno. Vilevile utafiti una nafasi ya kutathmini utoshelevu wa nadharia ya umilisi wa kiisimu katika kutafiti maswala ya ufunzaji na ufunzaji wa isimu katika lugha ya Kiswahili. Vipengee vinavyoonyesha badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha hulingana na mtu na mahali anapoishi. Rubin (1992) anasema kuwa ni vigumu kupima vipengee vinavyoonesha umilisi wa kiisimu katika lugha. Ingawa upimaji huu huegemea zaidi katika uwezo wa mzungumzaji kutumia sheria za lugha katika kusoma, kuzungumza na kuandika. Kulingana na Rubin badiliko linaonekana katika ma-

tumizi ya lugha husika, mtu anapozimudu sheria zilizotajwa awali za kisarufi katika kusema na kuandika makala ya kiusomi.

Mtalaam Mcmanara (2000) naye anasema kuwa kimsingi, mitihani ya umilisi wa mawasiliano yafaa kupima uwezo wa mzungumzaji katika kiwango cha sheria za lugha na vile vile katika kiwango cha utendaji wa lugha. Hata hivyo, mitihani mingi ya umilisi wa mawasiliano hujikita katika kupima umilisi wa kiisimu ambao huchukuliwa kama msingi wa kufahamu lugha yoyote ile. Hata ingawa umilisi wa kiisimu haumaanishi kuwa mzungumzaji ana umilisi wa kutosha katika mawasiliano. Umilisi huu wa kiisimu ndio msingi ama nguzo ya umilisi wa mawasiliano. Hata hivyo pana haja ya kutafiti na kutambua makosa ya kiisimu na namna makosa hayo yanathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili ili kuweza kupendekeza njia ambazo wahadhiri wanaweza kutumia kuimarisha umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili katika Vyuho Vikuu nchini Kenya.

Kulingana na Nunnan (2003), mtu ambaye anasitasita katika mazungumzo huonyesha umilisi wa kiwango cha chini katika lugha husika. Vilevile kuonesha matamshi mabaya ya maneno, kuchanganya na kuhamisha misimbo, kutofuata ruwaza maalum katika mazungumzo, kiimbo kibaya, na ung'amuaji wa maana ya maneno ni baadhi ya vigezo ambavyo huonesha badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha. Mtu aliye na umilisi wa juu katika lugha hataonesha upungufu huu. Hata hivyo anaweza kuonesha upungufu huu ikiwa umilisi wake ni wa kiwango cha chini. Lakini anapozidi kusoma na kuimarika umilisi wake unaimarika na kisha anafuata sheria kamili za lugha. Kwa hivyo ni muhimu kwa uchunguzi huu kuchanganua vigezo ambavyo huonesha mabadiliko ya kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya. Athari za lugha nyingine na haswa sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika Kiswahili huonekana wakati wa mtagusano wa lugha hizo na lugha ya Kiswahili.

Kulingana na Brezinger (1992), Gachiri (2009), Babusa (2010) na Muchemi (2011), lugha huweza kuathiriwa na mtagusano wa lugha nyingine. Athari hizi huonekana katika mazungumzo na maandishi. Naye Chomba (2013) alifanya utafiti kuhusu athari za sheng' kwa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za upili jijini Nairobi. Matokeo yanaonyesha kuwa lugha ya Kiswahili inaathiriwa sana na matumizi ya sheng' na hali hii inafanya umilisi wa kiisimu wa wanafunzi hao kuwa wa kiwango cha chini. Kwa hivyo pana haja ya kuchunguza ni athari zipi na ni vipi umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili huathiriwa na sheng'.

Mtalaam Buliba (1998) anaeleza kuwa wahadhiri wa isimu katika Kiswahili hukumbana na matatizo katika ufunzaji wa somo hili katika vyuo vikuu. Anaeleza kuwa changamoto za istilahi tofauti huwakanganya wanafunzi na kufanya umilisi wao wa isimu katika Kiswahili kuwa wa kiwango cha chini. Naye Mathooko (2000), anaongezea kwa kusema kuwa, dhana nyingi na tofauti za kiisimu katika lugha ya Kiswahili hutokana na tafsiri za Kiingereza ambazo hutumiwa na wahadhiri wakati wa ufunzaji wa somo la isimu katika lugha ya Kiswahili. King'ei (2000), anadai kuwa kuna ukosefu wa maandishi ya kiisimu katika Kiswahili. Majarida machache mno yameshughulikia isimu katika Kiswahili na mengi yanashughulikia fasihi. Hali hii inafanya umilisi wa kiisimu katika Kiswahili kuwa wa kiwango cha chini. Nao Musau na Ngugi (1997) wanasema kuwa idadi kubwa ya wanafunzi katika kozi za Kiswahili hufanya ufundishaji kuwa mgumu kwa sababu ya uchache wa vifaa vya kufunzia isimu hali hii inaathiri umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili. Ingawa lugha hii imefanyiwa utafiti na uchunguzi nyingi na wataalam mbalimbali, umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili unazidi kukumbwa na changamoto nyingi. Hivyo ni muhimu kwa utafiti huu kuchunguza na bainisha

changamoto wanazokumbana nazo wahadhiri na wanafunzi wa Chuo Kikuu katika ujifunzaji na ufunzaji wa isimu katika Kiswahili.

Mielekeo hujengwa kutokana na hali inayomkumba binadamu katika maisha. Kama vile: Kuzungumza, kusoma, kukua na kupata maarifa. Mielekeo vilevile hukua, hupungua na hui-marika mtu anapozidi kuongeza maarifa katika shughuli mbalimbali. Mtu huchukua mwelekeo fulani na kuushikilia mpaka anapobadili huo mwelekeo na kuchukua mwelekeo mwingine kuhusu jambo fulani kama asemavyo (Sheriff 1965). Watu hujenga mielekeo kuhusu mambo mbalimbali maishani kwa mfano watu huwa na mielekeo kuhusu siasa, uchumi, utamaduni, elimu, kati ya mengine mengi maishani. Wao hufanya hivyo kwa sababu tofauti tofauti kama vile, mielekeo husaidia mtu kubadilika kulingana na mabadiliko ya kilimwengu.

Mtu hazaliwi na mielekeo bali hujenga kupitia maingiliano yake na shoga wake, jamii na hata pengine shuleni. Mfumo huu wa mielekeo hujumuisha uelewaji wa mielekeo na maadili (Holloran, 1967). Kulingana na mtaalamu huyu kuna aina tatu za mielekeo nazo ni: tajriba ya moja kwa moja, pili mtu kujifunza kutoka kwa mtu mwingine na ujenzi wa tabia za mtu husika.

1.3. Suala la utafiti

Ufundishaji wa isimu kwa Kiswahili umezongwa na matumizi ya istilahi mbalimbali zinazotumiwa na wataalam katika ujifunzaji na ufunzaji wa isimu. Hali hii huenda inatinga kunawiri kwa kozi hizi za isimu na kuathiri kiwango cha ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Tafiti zim-edhihirisha kuwa wanafunzi hutofautiana katika umilisi wa stadi za kiisimu. Hata hivyo kazi hizi zinakosa uangavu wa kutosha wa kuchanganua umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa vyuo vikuu, changamoto na athari za kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa misingi hii

kunahitajika utafiti bayana unaotambulisha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Vilevile kuchambua katika kitengo finyu zaidi makosa ya kiisimu na namna makosa haya yanaathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa kufanya hivyo utafiti uweze kupendekeza njia ambazo wahadhiri wanaweza kutumia ili kuimarisha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

1.4. Maswali ya utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

- i. Je, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno wana kiwango kipi cha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili?
- ii. Badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili linaweza kuelezwa na vipengee vipi?
- iii. Umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili huathiriwa vipi na matumizi ya Sheng’?
- iv. Ni changamoto zipi ambazo huwakumba wanafunzi na wahadhiri wa isimu katika lugha ya Kiswahili katika idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Maseno?

1.5. Madhumuni ya utafiti

Lengo kuu la utafiti ni kutathmini kiwango cha umilisi wa kiisimu cha wanafunzi wa idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno.

Lengo kuu hili limefaulishwa kupitia madhumuni mahsusi yafuatayo:

- i. Kuchunguza kiwango cha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno.
- ii. Kueleza ni vipengee vipi vinavyoeleza badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno.

iii. Kueleza athari za Sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno.

iv. Kufafanua changamoto ambazo zinawakumba wanafunzi na wahadhiri wa isimu katika lugha ya Kiswahili katika idara ya Kiswahili na lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Maseno.

1.6. Umuhimu wa utafiti

Utafiti huu unatoa mchango katika kuendeleza Kiswahili kwani unafafanua sababu na athari zinazotinga umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, kwa kusoma kazi hii, wanajamii lugha wataelewa athari za sheng' zinazojitokeza katika lugha ya Kiswahili na hivyo kuachana na msimbo huu. Vilevile, matokeo ya utafiti yanaweza kutumiwa na wataalamu wa lugha kuelewa viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Halikadhalika, unatoa mchango katika taaluma ya isimujamii na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili wataelewa vyema matumizi yake katika miktadha tofauti. Pia pamekuwa na pendekezo la kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya umoja wa Afrika (AU) katika mikutano yake. Utafiti huu waweza kutumiwa na walimu wa Kiswahili wanaofunza katika vyuo vikuu nchini Kenya. Vilevile wataelewa matatizo ambayo yanawakumba wanafunzi wa isimu na kutafuta mbinu mwafaka ya kukabiliana na matatizo haya. Hali hii itawafanya wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili waelewe changamoto watakazokumbana nazo na jinsi ya kukabiliana nazo. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha sehemu ambazo wanafunzi wanahitaji msaada zaidi wanapojifunza isimu katika Kiswahili. Vilevile umilisi huu unaweza kuwa chombo cha kupimia uelewaji wa Kiswahili katika mihadhara na matatizo ya uandishi wa matini ya kiusomi katika vyuo vikuu, Chuo Kikuu cha Maseno kikitumiwa kama kigezo cha kupima umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

1.7. Upeo wa utafiti

Utafiti huu unajikita katika idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Maseno. Utafiti unahusisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza kwa sababu ndio mwanzo wanajiunga na Chuo Kikuu na wanafunzi wa mwaka wa nne ambao inaaminika kuwa wanakaribia kumaliza mtaala mzima wa isimu katika chuo mwaka huo. Umilisi wa kii-simu unahusisha vipengee vingi kama vile: Fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na Mofolojia. Hata hivyo utafiti huu unashughulikia sintaksia katika kitengo cha uchanganuzi wa sentensi katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na Radford (1981), sintaksia ni taaluma inayojishughulisha na namna maneno yanavyoweza kupangwa pamoja ili kutoa miundo ya sentensi sahihi katika lugha husika. Nao Massmba, kihore na Hokororo (2001), wanasema kuwa sintaksia ni taaluma ya isimu inayoshughulikia kanuni zinazotawala mpangilio wa maneno katika lugha husika ili kuunda tungo zenye maana. Jarabati inahusisha vipengee vya sintaksia ambapo wanafunzi wanaagizwa kuchanganua sentensi changamano ya lugha ya Kiswahili. Sintaksia ya lugha inahusisha mpangilio wa sentensi na kwa kuzingatia umilisi wa kiisimu katika sentensi ya Kiswahili, umilisi huu unampa mtafiti nafasi ya kuchanganua viwango vya umilisi vya wanafunzi wa mwaka wa kwanza na mwaka wa nne na jinsi wanavyomudu miundo sahihi ya sentensi katika lugha ya Kiswahili. Ingawa utafiti huu unalenga umilisi wa Kiisimu tulipima umilisi huu katika utendaji wao wa kimaandishi. Utafiti unafanywa kwa muda wa mwaka mmoja ukihusisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wa nne. Wanafunzi wa kike na kiume wanahusishwa katika utafiti. Mtafiti amechagua Chuo Kikuu cha Maseno kwa sababu isimu hufundishwa katika vyuo vyote nchini Kenya na matokeo ya utafiti huu yatakuwa kiwakilishi cha vyuo vile vingine. Vilevile idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika ni mojawapo wa idara kongwe ikilinganishwa na vyuo vingine katika eneo hili na data tunayohitaji inaweza kupatikana katika chuo hiki.

1.8. Sababu ya kuchagua mada ya utafiti.

Lugha ya Kiswahili ina hadhi na majukumu mengi katika vyuo vikuu nchini Kenya kwa ujumla. Kwa sababu hii, ni muhimu kwa wanafunzi wa chuo kikuu kuelewa na kuchambua isimu katika lugha ya Kiswahili kwa mapana zaidi. Kwa kuzingatia yale yanayosemwa kuhusu lugha hii ya Kiswahili ni dhahiri kwamba lugha hii ni muhimu sana na ina mawanda mapana kimatumizi. Ingawa lugha hii imefanyiwa utafiti na uchunguzi mwingi na wataalamu mbalimbali, lugha hii bado inakumbwa na athari za lugha nyingine katika vyuo vikuu nchini Kenya sheng' ikiongoza.

Pana haja ya kutafiti na kutambua makosa ya kiisimu na namna makosa haya yanaathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa kuelewa makosa haya utafiti unaweza kupendekeza njia ambazo wahadhiri wanaweza kutumia ili kuimarisha lugha ya Kiswahili. Vilevile utafiti una nafasi ya kutathmini utoshlevu wa nadharia ya Umilisi wa Kiisimu ya Lehmann katika kutafiti maswala ya ufunzaji na ujifunzaji lugha. Utafiti pia unaweka bayana mambo yanayochangia umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili aidha kudorora ama kuimarika.

1.9. Misingi ya nadharia

Utafiti huu unaongozwa na nadharia mbili. Nadharia ya kwanza ni ya Umilisi wa Kiisimu wa Lugha ya Lehmann (2006) na ya pili ya Gardner (1985) ambayo ni ya Motisha na Mielekeo ya Kujifunza L2. Katika kuchunguza na kuchanganua umilisi katika Chuo Kikuu cha Maseno utafiti umeweza kuelewa ikiwa madhumuni ya kufundisha isimu ya lugha katika Kiswahili yanafanikiwa au la. Utafiti umefahamu mambo mengine ambayo huchangia umilisi kudorora au kuimarika kwa wanafunzi wa isimu ya lugha katika Chuo Kikuu cha Maseno.

1.9.1. Nadharia ya umilisi wa lugha ya Lehmann.

Utafiti huu unajikita katika nadharia ya Umilisi wa Kiisimu ya Lehmann (2006). Dhana hii ya umilisi wa lugha si ngeni, ilikuwepo tangu wanafilolojia walipoingiza katika isimu karne ya kumi na nane (Chomsky 1957). Umilisi wa kiisimu katika lugha ni uwezo wa mtu binafsi kuelewa na kutumia vigezo vya kiisimu vinavyoshamiri matumizi ya lugha husika.

Kutokana na maelezo haya ya Lehmann (2006), mtu huwa na umilisi wa kiisimu katika lugha yoyote ikiwa ni mzaliwa wa lugha hiyo au ikiwa anajifunza kama lugha ya pili. Lehmann anaendelea kusema kuwa umilisi hupatikani tu katika lugha bali hupatikana katika taaluma nyingine kama vile; sosholojia na saikolojia. Lehmann katika nadharia yake ya umilisi wa kiisimu anaeleza kuwa umilisi hupatikana kupitia mazoezi na ujuzi. Pia anasema kuwa umilisi huu hupimwa kupitia mfumo maalum unaotengwa na wanajamii lugha husika, kwa mfano katika jarabati au vigezo vingine kama vile ufasaha katika mawasiliano. Jarabati ni mthani wa majaribio ambao hupewa wasemaji wa lugha ili kupima umilisi wao wa kiisimu katika lugha husika. Nadharia hii inaeleza kuwa umilisi wa kiisimu wa mtu hukuzwa na hali yake mwenyewe. Mtu anapozidi kufanya mazoezi katika lugha husika ndivyo ujuzi wake katika matumizi ya lugha hiyo huongezeka na kuimarika.

Umilisi wa kiisimu katika lugha yoyote ile huambatanishwa na matumizi yake katika usemi au katika maandishi na kuelewa jinsi lugha hiyo inavyopangwa kisarufi na jinsi inavyoathiri maisha ya mtu. Mwanaisimu huyu Lehmann anahitimisha kwa kusema kuwa umilisi wa kiisimu huhusisha kila kitu kinachohusiana na lugha kama vile; muundo, mawasiliano na utendaji. Utafiti huu unanua kupima umilisi wa kiisimu kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wa mwaka wa nne katika Chuo Kikuu cha Maseno, kwa kutumia nadharia hii ambapo mtafiti atatumia vigezo anavyotumia Lehmann katika nadharia hii.

Jarabati huweza kupima umilisi wa mwanafunzi kuweza kujibu maswali vizuri katika lugha husika bila dosari yoyote. Katika mazungumzo, mtu aliye na umilisi katika lugha hii huweza kuwasiliana na mwenzake kuhusu umilisi wa kiisimu na kuweza kupima umilisi wake. Maandishi ya mwanafunzi huonesha weledi wake katika umilisi wa kiisimu kufuatana na jinsi anavyoandika na kuwasilisha hoja zake katika isimu ya lugha ya Kiswahili. Nadharia hii inaongozwa na mihimili mitatu, ambayo ni:

i. Umilisi hupatikana katika mazoezi na hukua maishani mwa mtu

Mhimili huu unatumiwa kupima ukuaji wa umilisi wa kiisimu katika maisha ya mtu binafsi. Mtu huwa na umilisi wa kiwango fulani anapojifunza lugha. Umilisi wake hukua kadri msemaji huyu anapozidi kukua kiumri na vilevile kitaaluma. Lehmann anadai kuwa mtu anapozaliwa huanza kufahamu lugha na kadri anavyoendelea kukua ndivyo umilisi wake wa kiisimu huongezeka. Hii huweza kupimwa kwa kutumia jarabati maalum. Mhimili huu unatumiwa kuelewa ikiwa umilisi wa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Maseno hukua kuanzia mwaka wa kwanza hadi mwaka wa nne. Mwanafunzi anapojiunga na chuo huimarika kiumri na kimasomo kadri anapoendelea kukaa chuoni. Mhimili huu umemfaa mtafiti kwa sababu kuimarika kwa mwanafunzi kunaonekana anapozidi kusoma isimu katika Kiswahili chuoni. Hali hii inaonesha badiliko la umilisi wa kiisimu kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno. Aidha umilisi wake huwa unashuka au kuimarika.

ii. Umilisi wa kiisimu huhusishwa na mtu binafsi anayemiliki lugha

Kila mtu huwa na umilisi wa kiisimu wa kipekee na hutofautiana na mwenzake. Lehmann anadai kuwa watu wawili wakijifunza lugha katika mazingira sawa kila mmoja atakuwa na umilisi wa kipekee. Umilisi wa kiisimu huwa tofauti kati ya hawa watu wawili. Mhimili huu unasaidia mtafiti kuweza kufahamu umilisi wa awali wa kila mwanafunzi katika idara ya

Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Maseno ingawa wanatoka katika sehemu tofauti na kujifunza katika mazingira sawa ya Chuo Kikuu.

iii. Umilisi wa kiisimu huwa na vigezo vya kupimia kiwango katika lugha

Umilisi wa kiisimu wa lugha yoyote ile huwa na vigezo vya kupimia umilisi huu. Vigezo hivi ni: jarabati, ufasaha na uandishi au matini. Katika mazungumzo, ufasaha wa mwanafunzi hupimwa kupitia ujuzi hisa ambacho ni kipimo maalum kinachotumiwa kupima hisa ya umilisi wa lugha. Jarabati maalum ya kiisimu ambao ni mtihani unapewa wanafunzi na majibu yao yanakukadiriwa na kusaidia katika kupata umilisi wa kiisimu wa mwanafunzi. Jarabati inahusisha uchanganuzi wa sentensi changamano na ambatani. Vigezo hivi vitatu vinatumia kupima umilisi wa kiisimu wa wanafunzi. Mhimili huu unamfaa mtafiti katika kupima umilisi wa kiisimu katika Kiswahili kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno. Vilevile unamfanya kuelewa viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaosoma isimu katika Chuo kikuu cha Maseno.

1.9.2. Nadharia ya motisha na mielekeo ya kujifunza lugha ya pili ya Gardner.

Nadharia ya motisha ya kujifunza L2 ya Gardner ndiyo ya pili ambayo inatumia katika utafiti huu. Gardner (1985) alifafanua motisha ya kujifunza lugha ya pili kuwa na kiwango kinachojumuisha vipengee vitatu. Vipengee hivi ni;

i. Mielekeo ya kujifunza lugha

ii. Hamu ya kujifunza lugha

iii. Kiwango cha motisha

Kulingana na nadharia hii mtu aliye na kiwango cha juu cha motisha atataka kujifunza lugha hiyo na atatia bidii sana katika kujifunza lugha hiyo. Nadharia ya Gardner ya motisha ya kujifunza lugha ya pili inajikita katika maana na motisha ni kile kiwango ambacho mtu huwa na-

cho katika kujifunza lugha hiyo na furaha anayoipata kwa kujifunza lugha husika. Gardner anapendekeza kuwa ili mtu aweze kuifahamu lugha ya pili vilivyo, mtu huyo hupewa motisha ya kujifunza lugha husika. Ni vyema pia lengo au madhumuni ya kujifunza lugha hiyo yajulikane kwa mtu huyo. Gardner anaeleza Mihimili miwili katika nadharia yake, nayo ni:

i. Mkondo changamano

Mkondo changamano ni hamu ya mwanafunzi au mtu kujifunza zaidi kuhusu lugha na utamaduni wa jamii inayozungumza lugha husika na atajenga hamu ya kutaka kujua ile lugha na kuitumia katika mawasiliano. Mkondo changamano ni ile hamu ya kutaka kujua zaidi kuhusu lugha husika ya jamii hiyo. Hii humsaidia mwanafunzi kuwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha anayojifunza. Kwa hivyo mwanafunzi ambaye atakuwa na hamu ya kutaka kujifunza umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili ataweza kuboresha umilisi wake wa lugha ya Kiswahili.

ii. Mkondo wa kiala

Haya ni manufaa zaidi na ile hamu ya mwanafunzi ya kujifunza lugha fulani kwa minajili ya kufanikisha hali ya mtu ya kibinafsi na ya kufaulu mtihani na kujiendeleza kikazi. Kulingana na Gardner, mwanafunzi aliye na motisha ya mkondo changamano atakuwa na ari ya kujifunza lugha husika kuliko yule aliye na motisha ya mkondo wa kiala. Mwanafunzi aliye na motisha ya mkondo changamano atakuwa na mwelekeo chanya katika kujifunza lugha husika na atatia bidii katika shughuli hiyo. Hali hii itamfanya awe na umilisi wa hali ya juu. Hata hivyo Gardner anasema kuwa mikondo yote miwili ya motisha, yani ule wa changamano au kiala, husaidia mtafitiwa kujifunza L2. Kwa sababu mtafitiwa ataelewa manufaa ya kujifunza lugha na umuhimu wa lugha hiyo katika maisha ya kila siku.

Nadharia hizi mbili, ya Lehmann na ya Gardner, ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu nadharia ya Lehmann inachanganua umilisi wa kiisimu wa wanafunzi na ile ya Gardner inasaidia utafiti huu kama Kigezo cha kuamulia mambo yanayoathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na mambo haya utafiti unachanganua viwango tofauti vya wanafunzi wa mwaka wa kwanza na mwaka wa nne.

1.9.3. Upimaji wa umilisi wa kiisimu

Upimaji wa umilisi wa kiisimu huchukua mikondo tofauti. Kuna mkondo wa jarabati ambapo ufasaha wa mwanafunzi au mwanajamii lugha husika hupimwa kwa kutumia jarabati mahsusi ambapo huwa na vipengee sita au zaidi kuhusu isimu ya lugha husika Lehmann (2006). Ufasaha katika lugha hupimwa kupitia umilisi wa kiisimu katika lugha hiyo kwa sababu mtu au mwanafunzi aliye na umilisi wa kiisimu katika lugha, husemwa kuwa na umilisi katika lugha hiyo. Tewes (1991) anadai kuwa jarabati ya kupima umilisi wa kiisimu katika lugha yoyote ile hufanywa kupitia mazungumzo. Mtu anapozungumza, umilisi wake hufahamika kwa namna anavyojieleza na kuweza kuendeleza mazungumzo. Kigezo cha pili kinachotumiwa kupima umilisi wa kiisimu ni ujuzi hisa wa umilisi wa lugha, na hiki ni kigezo ambacho hutumiwa na wanasaikolojia kupima welekevu au ujuzi wa mtu katika akili. Kigezo hiki hutumia ufasaha maalumu katika kuelewa umilisi wa kiisimu wa mtu. Kigezo hiki huwa na idadi ya asilimia moja hadi asilimia mia moja.

Ufasaha wa mtu ukiwa zaidi ya asilimia thelathini hadi arobaini na tano huwa na umilisi wa hali ya wastani katika lugha husika. Akiwa na ufasaha wa zaidi ya asilimia sabini na tano huwa na umilisi wa juu zaidi, akiwa na ufasaha wa asilimia chini ya thelathini yeye huwa na umilisi wa kiisimu wa hali ya chini. Katika kupima umilisi wa mwanafunzi, mtafiti anatunga jarabati kuhusu isimu na majibu ya wanafunzi yanatumiwa kupata umilisi wao kwa kutumia

kigezo cha ujuzi hisa. Pia kupitia mazungumzo yao, mtafiti anaweza kuelewa umilisi wao (Tewes, 1991). Katika kutumia jarabati maandishi na jarabati mazungumzo mtafiti anapata kuelewa umilisi wa kiisimu wa wanafunzi katika ya lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno.

1.9.3.1 Vigezo vingine vya kupima umilisi

Vigezo vingine vya kupima umilisi wa kiisimu ni vile vilivyoasisiwa na Nunnan (2003).

Mtalaam huyu anaendelea kusesitiza kuwa, katika kupima umilisi wa kiisimu wa mtafitiwa katika lugha husika, vigezo vifuatavyo hutumika. Vigezo hivi ni vitano na hutumika wakati wa kupima umilisi katika maandishi. Navyo ni:

- i. Sarufi
- ii. Namna au kwa ufundi fulani wa kuitumia sarufi katika mazungumzo.
- iii. Kwa kusudi fulani la kuandika na kupanga mawazo yako.
- iv. Mshikamano wa mawazo
- v. Uhusiano kuhusu kile wanachokiandika.

Kila kigezo hutuzwa alama kuanzia 1-10. Wale wanaopata alama 9-10 huwa adhimu, wale ambao hupata alama 7-8 huwa vizuri sana, wale ambao hupata alama 5-6 huwa vizuri, wale ambao hupata alama 3-4 huwa wastani na wale ambao hupata alama ya 1-2 huwa hafifu. Kwa ujumla mtu anayepata alama ya 9-10 katika vigezo hivi vyote husemekana kuwa na umilisi wa kiisimu wa kiwango cha juu katika lugha husika.

1.10. Hitimisho.

Sura hii imeeleza misingi muhimu ya utafiti huu. Usuli wa utafiti umefafanua masuala muhimu kuhusu umilisi wa kiisimu. Maoni ya wataalamu mbalimbali yamezingatiwa ili kueleza misingi ya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Aidha, kwenye usuli pia imebainika kuwa kuna baadhi ya wanafunzi ambao wana umilisi tofauti tofauti kulingana na jinsia yao. Utafiti huu umebainisha na kueleza sababu zingine ambazo huathiri umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili. Maoni haya yanalenga kudhihirisha umuhimu wa kuendeleza na kufanikisha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno. Isitoshe, upeo wa utafiti, misingi ya uteuzi wa mada pamoja na nadharia za utafiti zimeelezwa pia. Utafiti umejikita katika kuchunguza umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno na masuala ibuka kuhusu umilisi huu wa wanafunzi. Sura inayofuata inashughulikia uhakiki wa maandishi.

SURA YA PILI

UHAKIKI WA MAANDISHI

2.1. Utangulizi

Sura hii inaangazia mapitio ya maandishi ambayo yanahusiana na umilisi wa kiisimu katika lugha. Vilevile inamulika jinsi mielekeo na motisha huchangia kuimarika au kushuka kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya. Tafiti zingine zinazokaribiana na utafiti huu zimehusishwa.

2.2. Umilisi wa kiisimu

Umilisi ni uwezo au ujuzi wa msemaji kuimudu lugha yake. White (1959) anasema kuwa mtu binafsi ana umilisi katika shughuli fulani ikiwa ana uwezo wa kutatua matatizo katika shughuli hiyo. Umilisi wa kiisimu ni utaratibu wa kielimu katika isimu ya lugha inayomilikiwa na wanajamii lugha. Mtu kusema kuwa ana umilisi katika lugha fulani lazima awe na ufasaha wa kiwango fulani. Chomsky (1965) aliipa dhana hii ya umilisi wa lugha umuhimu zaidi alipozungumza kuhusu umilisi na utendaji. Kulingana na Chomsky wanajamii lugha huwa na ujuzi wa kuelewa mipango na matumizi ya sentensi na sheria katika lugha husika. Ujuzi huu aliuita umilisi na ule wa matumizi ya lugha akauita utendaji ambao ni ule uwezo wa msemaji kutumia lugha bila kufanya makosa. Anaendelea kusema kuwa mtu anaweza kuwa na uwezo na maarifa katika lugha na sio matumizi yake. Chomsky anasema kuwa umilisi wa kiisimu huhusisha maarifa katika lugha kuliko matumizi katika lugha hiyo ambayo aliita utendaji.

Hymes (1971) anaendeleza mawazo ya Chomsky kwa kuongezea kuwa ni vyema kuchunguza umilisi wa kiisimu lakini ni bora zaidi kuchunguza jinsi mtu anavyotumia lugha hiyo. Yeye anazua wazo la umilisi katika mawasiliano, ambapo anasema kuwa unaweza kuelewa

umilisi wa kiisimu wa msemaji kwa kuwasiliana naye katika miktadha mbalimbali. Pia anazua wazo la umilisi wa sarufi na utendaji ambao anaita pragmatiki. Chomsky (1980) anakubaliana na mawazo haya kwa kusema kuwa umilisi hupatikana katika matumizi ya lugha. Kwa kuelewa haya, utafiti unaweza kufahamu umilisi wa kiisimu wa mwanafunzi wakati wa kuzungumza naye ili kufahamu ikiwa umeimarika na kwa kiwango kipi.

Mtalaam Lehmann (2006) anasema kuwa umilisi wa kisarufi ni kule kujua umbo la lugha na maana katika matumizi yake. Pragmatiki ni zile sheria na jinsi ya kutumia sheria hizi katika miktadha mbalimbali. Hivyo tunaweza kuchukua lugha kama chombo kinachoweza kutumiwa katika miktadha tofauti. Usarufi huonesha umilisi wa kisarufi na sheria tofauti hushamiri umilisi wa kipragmatiki na jinsi sheria hizo huweza kutumiwa. Chomsky (1986) anasema kuwa ubongo wa binadamu huwa na kitivo cha lugha ambacho huhusiana na elimu ya lugha husika.

Kitivo hiki pia kina na uwezo wa kutumia lugha katika shughuli mbalimbali. Anadai kuwa umilisi wa mtu katika lugha haukui, lakini wazo hili linapingwa na Lehmann (2006) anayedai kuwa umilisi wa mtu hukua katika maisha na ufasaha wake huongezeka jinsi anavyoimarika katika miaka na sio tu katika lugha ya kwanza lakini katika lugha ya pili na ya tatu. Vilevile Coseriu (1988) anasema kuwa mtu huongeza umilisi wa kiisimu katika maisha anapozidi kuka na hufika viwango tofauti kwa watu tofauti. Widdowson na Henry (1973) wanadai kuwa umilisi ni uchunguzi wa uwezo wa mtu wa kujua na kutumia lugha. Umilisi wa kiisimu anauona kama si jambo muhimu kwake. Vollmer (1982) anaeleza umilisi kama kuwa na sheria na elimu ya kisarufi katika lugha husika, na kuweza kutumia sheria hizi katika mawasiliano. Fillmore na Charles (1979) anasema kuwa lugha katika miktadha mbalimbali huweza kupimwa kutumia vigezo vilivyokubaliwa na wanajamii lugha husika. Canale na Swain

(1980) wanaeleza umilisi wa kimawasiliano kama uwezo wa matumizi ya lugha katika mawasiliano ya kila siku. Wao wanaeleza umilisi wa kiisimu kama shughuli ya kiusomi, wanasema kuwa ufasaha katika umilisi hupimwa kupitia lugha husika. Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili (1939) inaeleza maana ya umilisi kama ustadi wa kitu au shughuli, umahiri au ujuzi wa mtu katika shughuli yoyote ile. Kamusi ya Oxford (1974) inaeleza kuwa, umilisi ni ujuzi wa msemaji kuelewa mambo mbalimbali kuhusu lugha.

Fraser na Nolan (1981) wanaeleza umilisi kama njia anayotumia mwanafunzi katika kupata elimu na ujuzi wa kufanya shughuli za kikazi. Wanalinganisha umilisi na njia ya kutekeleza mambo muhimu. Wanatoa maana ya umilisi kama mchezo kati ya majukumu yanayotajwa na jinsi yatakavyofanikishwa. Kutokana na maelezo haya mtafiti anaweza kufahamu matatizo wanayopata wahadhiri na wanafunzi wakati wa shughuli za kimasomo na jinsi wanavyokabiliana na masuala haya.

Watalaam Canale na Swain (1980) wanadai kuwa umilisi huwa katika majukumu tofauti. Mawazo haya yanaungwa mkono na Stern (1983) anayedai kuwa weledi katika lugha ni jukumu ambalo lazima litimizwe. Msemaji wa lugha hiyo sharti awe na umilisi wa kuweza kutumia lugha vilivyo na awe mwepesi wa kuunda maneno na sentensi. Carol (1968) anaeleza kuwa umilisi wowote wa lugha unahusisha umilisi wa kiisimu na umilisi wa utendaji katika lugha hiyo. Anasema kuwa mtu huweza kuwa na ujuzi wa kusema lugha yoyote ile ikiwa ana umilisi wa matumizi ya lugha. Mawazo haya yanaungwa mkono na Clark (1977) anayedai kuwa mtu aliye na weledi katika lugha ni lazima awe anaweza kufahamu miundo tofauti ya kileksia, kifonolojia, kisintaksia, kisemantiki na uchanganuzi usemi katika muktadha wa kijamii. Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa lugha ni mali ya jamii na huhusiana na mambo ya kijamii. Umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili hutegemea

mambo kama vile mazingira anamokulia mtu. Mtu akiwa katika mazingira ambayo yana umilisi mkubwa wa kiisimu basi weledi wake huweza kuongezeka na kufikia kiwango cha juu cha asilimia sabini na tano au zaidi. Kuna viwango vingi vya umilisi wa kiisimu katika lugha yote ile kama vile:

2.2.1. Umilisi wa mawasiliano katika lugha

Umilisi wa mawasiliano ni suala ambalo limejadiliwa na wanaisimu na wanaisimujamii kwa muda mrefu kufikia sasa. Mjadala huu zaidi unajikita katika kule kujaribu kutambulisha hasa ni vipengee vipi mzungumzaji anafaa kuvimudu ili isemekane kuwa ana umilisi tosha wa lugha anayoizungumza na hatimaye kuelezewa kuwa ana umilisi wa mawasiliano. Baadhi ya wale ambao wamechangia pakubwa mjadala huu ni wataalamu kama vile Hymes (1971) na Canale na Swain (1980) na Nicuolo (1991). Wengine ni kama vile Nunan (2003) na Fletcher na Davidson (2007).

Chomsky (1965) alizua dhana ya umilisi wa lugha. Kulingana naye, umilisi wa lugha ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kufahamu vyema sheria za kiisimu za lugha anayoizungumza. Sheria hizi ni kama vile kufahamu kuhusu leksia, fonetiki, fonolojia, morfolojia, sintaksia na semantiki ya lugha husika. Mbali na kuzifahamu sheria za lugha, mzungumzaji anafaa kuwa na ule uwezo wa kutumia lugha ipasavyo.

Mtazamo huu wa Chomsky (1965) kuhusu umilisi wa lugha uliegemea katika masuala ya kiisimu pekee. Kulingana na Hymes (1971), mtazamo huu ulikuwa finyu kwa vile kuzifahamu sheria za kiisimu za lugha pekee hakutoshi kumwezesha mtu kuweza kuitumia lugha kikaamilifu katika jamii yake. Hivyo basi Hymes (1971) na wanaisimu wengine kama vile Savignon (1972) waliyapanua mawazo ya Chomsky kuhusu umilisi wa lugha kwa kuanzisha

dhana ya umilisi wa mawasiliano. Mbali na kuhusisha umilisi wa sheria za lugha, Hymes alifafanua kuwa umilisi wa mawasiliano pia huhusisha masuala ya kiisimujamii ya lugha yaani utendaji wa lugha ama kule kuweza kutumia lugha kwa ufaafu katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Kwa kuelewa mitazamo hii mtafiti alifahamu aina tofauti za umilisi wa kiisimu ambazo alikuwa anatafiti katika lugha. Vilevile unapochunguza umilisi wa kiisimu lazima pia uchunguze umilisi wa mawasiliano kama kitengo cha utendaji.

2.2.2. Umilisi wa usemaji

Mtalaam Newmark (1966) anasema kuwa lazima mtu ajue mambo mengi kama vile: sheria za kimsingi za lugha, umilisi wa usemaji, umilisi wa isimujamii kati ya mengine mengi ili aweze kuwa na umilisi wastani au wa juu zaidi. Nao Richard na Rodgers (1986) wanaunga mkono mawazo haya kwa kusema kuwa mtu kusema ana umilisi wa lugha sio kitu rahisi, huchukua mambo mengi sio tu umilisi wa sheria za lugha na utendaji bali zaidi ya hayo. Kwa mfano sentensi ya Kiswahili huundwa na kiima na kiarifa.

Hizi ni sheria ambazo zimekubaliwa na wanajamii lugha husika. Kwa mfano sentensi kama, *Juma anacheza mpira*. Katika sentensi hii Juma ni kiima na anacheza mpira ni kiarifa. Katika sentensi *Mama anapika chapati*, mama ni kiima na anapika chapati ni kiarifa. Sentensi zote katika lugha hii ya Kiswahili hufuata mtindo huu. Sentensi haiwezi kuanza na kiarifa kisha ifuatwe na kiima. Kwa mfano; *Mpira anacheza Juma au Chapati anapika mama*. Sentensi hizi zikiandikwa hivyo zitakuwa na maana tofauti na ilivyokusudiwa na msemaji wa sentensi hizi atakuwa na umilisi wa chini katika lugha ya Kiswahili. Hivyo ni vyema kuelewa kuwa mpangilio wa sentensi ya Kiswahili hufuata muundo maalum na ukibadilishwa sentensi huwa na maana tofauti na ilivyokusudiwa.

2.2.3. Kupima umilisi wa mawasiliano

Utafiti huu unanuia kupima umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Madhumuni ya pili ambayo inaeleza vipengee ambavyo huonyesha badiliko la umilisi vimehusishwa katika utafiti. Katika kupima viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili, utafiti huu unahusisha kipengele cha umilisi wa kiisimu katika lugha na kipengele cha umilisi wa mbinu za lugha na wala sio vipengele vingine vya umilisi wa mawasiliano kama vile umilisi wa kiisimujamii.

Mitihani mingi ya upimaji wa umilisi wa mawasiliano zaidi huegemea katika kipengele cha umilisi wa kiisimu na wala sio vipengele vingine vya umilisi wa mawasiliano kama vile umilisi wa kiisimujamii, umilisi wa mbinu za mawasiliano na umilisi wa uchanganuzi usemi. Hii ni kwa sababu, kama asemavyo Rubin (1992), “sio muhimu kila mara kupima vipengele vyote vya umilisi wa mawasiliano ili kufahamu kama mzungumzaji ana umilisi wa mawasiliano ama la”. Hakika, kama anavyoendelea kuelezea Rubin, “ni nadra sana kupata vipengele vyote vya umilisi wa mawasiliano vikipewa uzito sawa katika utafiti iwapo vyote vitahusishwa katika upimaji wa umilisi wa kiisimu”.

Kupima umilisi wa mawasiliano huegemea zaidi katika umilisi wa kiisimu kwa kupima uwezo wa mzungumzaji wa kutumia sheria za lugha sana sana kupitia stadi za lugha zinazolenga maandishi na mazungumzo yaani stadi za kuongea, kusoma na kuandika. Aidha, Nicuolo (1991) anadai kuwa vipengele vile vingine vya umilisi wa mawasiliano, kama vile umilisi wa kiisimujamii, huhitaji kipindi kirefu cha wakati kupimwa kwani vimejikita zaidi katika masuala ya tamaduni za jamii, tabia na lugha za mzungumzaji.

Mcmanara (2000) naye anasema kuwa kimsingi, mitihani ya umilisi wa mawasiliano yafaa kupima uwezo wa mzungumzaji katika kiwango cha sheria za kisarufi za lugha na vile vile

katika kiwango cha utendaji wa lugha. Hata hivyo, mitihani mingi ya umilisi wa mawasiliano hujikita katika kupima umilisi wa kiisimu ambao huchukuliwa kama msingi wa kufahamu lugha yoyote ile. Hata ingawa umilisi wa kiisimu haumaanishi kuwa mzungumzaji ana umilisi wa kutosha katika mawasiliano, umilisi huu wa kiisimu ndio msingi ama nguzo ya umilisi wa mawasiliano. Nicuolo (1991) anatoa hoja kuwa umilisi wa mawasiliano huanza kwa umilisi wa kiisimu wa lugha yaani kufahamu na kuzimudu sheria za lugha. Utafiti huu unachunguza upimaji wa umilisi wa kiisimu kuhusisha umilisi wa mawasiliano. Ingawa vigezo hivi viwili vinategemeana katika shughuli yote ya upimaji, kwa sababu huwezi kupima umilisi wa mawasiliano bila kuchunguza umilisi wa kiisimu na vilevile huwezi kupima umilisi wa kiisimu bila kuchunguza utendaji katika mazungumzo ama maandishi.

2.3. Tafiti kuhusu umilisi wa kiisimu

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu ni kuchunguza viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno. Ni muhimu kuchunguza tafiti za kiisimu zinazohusiana na utafiti huu. Ni muhimu pia kujua jinsi tafiti hizi zinavyolingana na kutofautiana katika madhumuni, sampuli na matokeo ya utafiti huu. Utafiti wa Ramadhan (1998) ulichunguza umilisi wa kiisimu wa walimu wa shule za msingi katika Kiingereza nchini Iraq ambapo, walimu sabini wa shule za msingi walishiriki katika utafiti huu. Matokeo yameonyesha kuwa umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiingereza kama kifaa cha kufundishia ulikuwa wa kiwango cha wastani, umilisi wao wa lugha ya Kiingereza kwa ujumla ulikuwa wa kiwango cha chini na hii iliathiri umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wao. Utafiti huu unachunguza umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili, matumizi ya istilahi mbalimbali na changamoto zinazowakumba wahadhiri na wanafunzi wa isimu katika Kiswahili tofauti na ilivyo na utafiti wa Ramadhan. Tofauti hapa ni kuwa umilisi wa kiisimu katika Kiingereza umechunguzwa na ulihusisha walimu waliohitimu ilhali katika utafiti huu umilisi wa kiisimu katika Kiswahili

ulichunguzwa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ambao walikuwa bado hawajahitimu shahada kwenda kufundisha katika shule za upili.

Essa (2001) alichunguza umilisi wa mazungumzo katika lugha ya Kiingereza kwa walimu wa shule za msingi katika Chuo cha Elimu cha Baghdad. Walimu thelathini na sita walishiriki ambapo mtafiti alitumia mjarabu wa mazungumzo kupima umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiingereza kwa walimu hawa. Matokeo yameonyesha kuwa walimu wanapohitimu wanaonekana kuwa na kiwango cha wastani katika mazungumzo na vitengo vingine vya isimu kama vile: fonetiki, sintaksia na semantiki. Viwango vya wastani kwa walimu wanaohitimu ni dhihirisho tosha kuwa wana umilisi wa kiisimu ambao hautoshi kuweza kufunza katika shule. Hali hii ya viwango vya chini vya umilisi inaathiri wanafunzi ambao wanawafunza. Vilevile utafiti huu unachunguza umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno na utafiti wa Essa umechunguza umilisi wa lugha ya Kiingereza kwa walimu wa shule za msingi. Utafiti huu unachunguza wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno ambao walikuwa hawajahitimu na kuangazia changamoto wanazokumbana nazo wakati wa ujifunzaji wa isimu katika lugha ya Kiswahili.

Naye Ng'ong'a (2002) alifanya uchunguzi kuhusu umilisi wa kiisimu katika Kiingereza kwa wanafunzi wa somo la Kiingereza katika Chuo Kikuu cha Maseno, alipata kuwa wanafunzi wengi wa Kiingereza hawakuwa na welekevu katika somo hili ilhali wao ndio walitakiwa kwenda kufundisha katika shule za upili nchini Kenya. Wanafunzi hawa walikuwa na makosa mengi ya kisarufi, walikosa ufasaha wa lugha hii ya Kiingereza katika mawasiliano yao na walishindwa kuelewa vipengee muhimu vya kimsingi kuhusu lugha ya Kiingereza. Alipata kuwa wahadhiri na wanafunzi walikuwa na ukosefu wa vifaa vya kufundisha, kati ya matatizo mengine. Ingawa utafiti huu unakaribiana na wetu kwa sababu ulifanya katika Chuo Kikuu

cha Maseno, lakini lugha iliyochunguzwa ilikuwa ya Kiingereza na utafiti wetu unachunguza lugha ya Kiswahili. Vilevile alichanganua viwango vya umilisi katika Kiingereza na utafiti huu unachanganua viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Pia utafiti huu unachunguza athari za msimbo wa sheng' kwa isimu katika Kiswahili ambapo ni tofauti na alivyofanya Ngong'a katika utafiti wake.

Utafiti wa Jokey (2007) ulichunguza umilisi wa mazungumzo kwa walimu wa Kiingereza katika mji wa Baghdad. Walimu arobaini na tano walishiriki katika utafiti huu. Matokeo ya uchunguzi yameonyesha kuwa walimu walikuwa na upungufu katika matumizi ya lugha ya Kiingereza. Hii ilionekana katika matamshi ya maneno ya Kiingereza na walitumia msamiati usiyofaa katika sentensi wakati wa mazungumzo.

Utafiti huu umechunguza umilisi wa Kiingereza wa walimu waliokuwa wamehitimu. Lakini utafiti huu unachunguza umilisi wa kiisimu wa wanafunzi katika Kiswahili ambao bado wanasoma katika Chuo Kikuu cha Maseno na utafiti ule mwingine uliwahusisha walimu ambao walikuwa wamehitimu. Tofauti hapa ni kuwa umilisi wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno na changamoto wanazokumbana nazo ni tofauti na ilivyo katika vyuo vya Baghdad. Idadi iliyoshiriki katika utafiti wa Jokey ilikuwa ndogo ikilinganishwa na utafiti huu. Vilevile utafiti huu unachunguza athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili ambapo utafiti wa Jokey haukuchunguza hayo.

Mwanaisimu Raheem (2007) alichunguza matumizi ya Kiingereza katika ufundishaji wa wanafunzi katika shule za msingi mjini Baghdad. Walimu hamsini walishiriki katika utafiti huu. Matokeo yameonesha kuwa walimu walikuwa na upungufu wa kutumia Kiingereza katika mazungumzo na wanafunzi wao. Hali hii imeonesha kuwa umilisi wa kiisimu katika

lugha ya Kiingereza wa walimu hawa ulikuwa wa kiwango cha chini. Pia imeonekana katika matamshi na maandishi yao. Utafiti huu ulichunguza umilisi katika lugha ya Kiingereza katika ufundishaji wa wanafunzi wa shule za msingi katika mji wa Baghdad, lakini utafiti huu unachunguza umilisi wa kiisimu katika Kiswahili kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno na wanafunzi ambao wanategemewa kwenda kufundisha katika shule za upili tofauti na ilivyo katika shule za kimsingi mjini Baghdad.

Mtafiti Kamau (2015) alichunguza athari za lugha ya Kiingereza, Kiswahili na sheng' kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu katika kaunti za Nairobi, Kiambu na Murang'a kwa wanafunzi wa shule za upili. Matokeo yameonesha kuwa lugha ya Kikuyu huathiriwa na matumizi ya Kiingereza, Kiswahili na sheng'. Utafiti huu unachunguza umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili na vilevile sampuli yetu ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno ilhali ya Kamau ilikuwa ya wanafunzi wa shule za upili. Lugha ya Kiswahili huathiriwa na lugha nyingine kama vile Kiingereza na sheng'. Athari hizi huonekana katika matamshi na maandishi. Mtu anapozungumza athari hizi huonekana katika uundaji wa maneno na sentensi. Hali hii pia inaonekana katika maandishi, kwa sababu mtu huchanganya lugha zote.

Kwa ujumla utafiti wa Ng'ong'a, jokey na Raheem zimechunguza walimu waliohitimu na kwenda kufunza katika shule mbalimbali mjini Bagdad. Utafiti wa Essa (2001) umechunguza walimu waliokuwa katika chuo wakisomea ualimu na walipohitimu walienda kufundisha katika shule nyanjani. Utafiti huu wa Essa unakaribiana na utafiti huu, kwa sababu utafiti huu unachunguza umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa isimu ya Kiswahili na wanafunzi hawa huwa walimu baada ya kuhitimu shahada. Utafiti wa Ngo'ng'a (2002) vilevile unakaribiana na utafiti huu wetu ingawa yeye alifanya utafiti katika lugha ya Kiingereza nasi tukafanya katika lugha ya Kiswahili isipokuwa sote tulichunguza wanafunzi wa Chuo Kikuu cha

Maseno. Utafiti wa Ng'ong'a umependekeza kuwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu umilisi wa kiisimu katika lugha nyingine zinazotumiwa na wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Maseno, Kiswahili kikiwa mojawazo. Sampuli iliyotumika katika utafiti wa awali ilikuwa ndogo, kati ya thelathini na sita hadi sabini na utafiti huu unatumia idadi ya zaidi ya mia moja. Jarabati ya mazungumzo ilitumiwa katika utafiti wa awali na jarabati ya maandishi inatumiwa katika utafiti wa sasa.

2.3.1. Vipengee vinavyoonyesha badiliko la umilisi

Mtafiti Verhoeven (1992), anaeleza kuwa vipengee vinavyoonyesha mabadiliko katika umilisi wa kiisimu wa lugha huwa tofautitofauti. Anatoa mfano wa uwezo wa mzungumzaji wa kuunda na kutambua miundo ya sentensi sahihi na isiyo sahihi katika lugha husika (sintaksia), kufahamu msamiati mbalimbali wa lugha (leksimu), kuwa na matamshi bora (fonolojia) na kufahamu maana ya maneno (semantiki) na uundaji wa maneno na sentensi sahihi (mofolojia na sintaksia). Ujuzi huu wote kulingana na Verhoeven ndio msingi wa kufahamu vipengee muhimu katika umilisi wa kiisimu. Kwa ufupi, umilisi wa kiisimu ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kuweza kutumia sheria hizi za lugha kuunda maneno na sentensi sahihi na zenye maana. Jambo linamwezesha kushiriki katika mazungumzo bila shida yoyote. Ikiwa mtu ataweza kushiriki mazungumzo vizuri, hiki ni kigezo mojawapo cha kuonyesha mabadiliko katika umilisi wa kiisimu.

Mwanaisimu Nicuolo (1991) anasema kuwa, umilisi wa mawasiliano huanza kwa umilisi wa kiisimu wa lugha yaani kufahamu na kuzimudu sheria za lugha. Akifafanua zaidi, Nicuolo anasema kuwa hii labda ndio sababu mara nyingi mitihani mingi ya kupima umilisi wa mawasiliano huegemea zaidi katika umilisi wa kiisimu kwa kupima uwezo wa mzungumzaji wa kutumia sheria za lugha sana sana kupitia stadi za lugha zinazolenga maandishi na ma-

zungumzo yaani stadi za kuongea, kusoma na kuandika. Mwanaisimu Mcmanara (2000) naye anasema kuwa kimsingi, mitihani ya umilisi wa mawasiliano yafaa kupima uwezo wa mzungumzaji katika kiwango cha sheria za lugha na vile vile katika kiwango cha utendaji wa lugha. Hata hivyo, mitihani mingi ya umilisi wa mawasiliano hujikita katika kupima umilisi wa kiisimu ambao huchukuliwa kama msingi wa kufahamu lugha yoyote ile. Kigezo hiki cha mawasiliano ndicho hutumiwa kama kipengee muhimu cha kuonesha badiliko la umilisi katika lugha. Kwa sababu mtu anapozungumza akifuata sheria za lugha hiyo vyema, basi yeye husemekana kuimarika.

Wanaisimu hawa, Nicuolo (1991), Rubin (1992), Verhoeven (1992) na Mcmanara (2000) wana msimamo wa pamoja kuwa suala la upimaji wa umilisi wa mawasiliano kama kigezo kinachoonsha badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha. Hii ni kwa sababu mitihani mingi ya kupima umilisi wa mawasiliano huegemea zaidi katika upimaji wa umilisi wa kiisimu hata ingawa hiki sicho kipengee pekee kinachohusishwa na umilisi wa mawasiliano. Nunnan (2003) anaeleza kuwa vigezo vinavyoonesha badiliko la umilisi wa kiisimu ni: mtu kusema maneno bila kusitasita, kutochanganyia au kuhamisha misimbo, kutokuwa na matamshi mabaya ya maneno na vilevile kuelewa maana ya maneno bila shida. Vigezo hivi huonesha kuwa mtu huyu ameimarika katika lugha husika. Kamau (2015) anakubaliana na mawazo ya Nunnan katika uchunguzi wake kuhusu athari za Kiingereza, na Kiswahili kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Murang'a. Alipata kuwa wanafunzi walitasita katika kusema Kikuyu, walikuwa na matamshi mabaya ya maneno na walihamisha na kuchanganyia misimbo kila mara walipowasiliana na wenzao. Hali hii ilifanya umilisi wa isimu katika Kikuyu kuwa ya kiwango cha chini. Hali hii iliathari umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kikuyu.

2.3.2. Athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu

Madhumuni ya tatu ya utafiti huu ni kuchunguza athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Watafiti wafuatao wamefanya utafiti kuhusu athari za sheng kwa umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili. Babusa (2010) kwa kutumia mtazamo linganuzi, amelinganisha mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili kuhusu lugha ya Kiswahili na vile mielekeo hii inavyoathiri viwango vya umilisi wa lugha hii miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili mikoani Mombasa na Nairobi. Pia utafiti wa Babusa umeangalia tofauti za viwango vya umilisi wa lugha ya Kiswahili kijinsia katika mikoa hii miwili. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa wanafunzi wa mkoa wa pwani wana mielekeo chanya zaidi kuhusu lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na wale wa mkoa wa Nairobi. Wasichana nao wameonesha kuwa na viwango vya juu vya umilisi wa Kiswahili kuliko wavulana.

Ingawa Babusa hakuchunguza athari za lugha moja kwa moja, matokeo yameonesha watafitiwa kutoka eneo la Nairobi walikuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili kuliko wenzao wa Mombasa ambao walikuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili. Athari ya lugha ya Kiswahili imeonekana Nairobi kwa sababu ya matumizi ya sheng' na Kiingereza. Utafiti huu wetu unachunguza umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno. Vilevile sampuli yetu ni wanafunzi wa Chuo Kikuu ilhali ya Babusa ilikuwa wanafunzi wa shule za upili. Chomba (2013), alifanya uchunguzi kuhusu athari za sheng' kwa umilisi wa lugha ya Kiingereza. Matokeo yaliyopatikana yameonesha kuwa lugha ya Kiingereza huathiri na matumizi ya sheng' kwa wanafunzi wa shule za mji wa Nairobi. Athari hizi zimeonekana kwa maandishi na mazungumzo yao.

Mtafiti Kamau (2015) alifanya utafiti kuhusu athari za lugha ya Kiingereza, Kiswahili na Sheng' kwa lugha ya Kikuyu. Utafiti wake ulifanywa katika miji ya Nairobi, Kiambu na Mu-

rang'a. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa, lugha hizi tatu huathiri kwa kiwango kikubwa umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kikuyu kwa wanafunzi wa shule za upili. Hali hii huwafanya wanafunzi kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu. Utafiti wa Kamau ulichunguza athari za lugha ya Kiingereza, Kiswahili na sheng' kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu ilhali utafiti wetu unachunguza athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Sampuli ya Kamau ilikuwa wanafunzi wa shule za upili ilhali yetu ni wanafunzi wa Chuo Kikuu. Utafiti wa Kamau ni kiisimu jamii ilhali utafiti huu ni wa isimu tumikizi. Mtalaam mwingine ni Miguda (2003) ambaye alifanya utafiti kuhusu athari za sheng' kwa Kiswahili sanifu katika mji wa Nairobi. Utafiti huu ulipendekeza kuwa, njia zitafutwe za kuimarisha ufundishaji na ufunzaji wa Kiswahili sanifu ili athari za sheng' ziweze kupunguzwa au kuondolewa kabisa. Utafiti huu wa Miguda ni wa kiisimu jamii ilhali utafiti huu ni wa isimu tumikizi.

Mtafiti Muchemi (2011) alitafiti kuhusu vijana wa jamii ya Kikuyu mashambani wanavyoathirika kutokana na mtagusano wa lugha ya Kikuyu na lugha ya Kiingereza na namna mtagusano huu huathiri umilisi wa lugha ya Kikuyu. Katika utafiti huu, muchemi anasema kuwa sababu kuu ya vijana ya jamii ya Kikuyu mashambani kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ni msisitizo wa matumizi ya lugha ya Kiingereza katika shule za upili nchini Kenya na hatimaye msisitizo huu unachangia katika kupotea kwa vipengee vya isimu katika lugha ya Kikuyu kama vile leskia na mofosintaksia.

Kwa mujibu wa utafiti wa Muchemi (2011), mtagusano wa lugha ya Kiingereza na Kikuyu umepelekea kupotea kwa vipengee fulani vya kiisimu katika lugha ya Kikuyu kama vile nyakati na mpangilio wa maneno katika sentensi. Hivyo, ni kama vijana wa jamii ya Kikuyu mashambani wameanza kuhama kutoka kwa matumizi ya lugha ya Kikuyu hadi kwa ma-

tumizi ya Kiingereza na hivyo kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu. Utafiti huu ni muhimu kwetu kwa sababu umetueleza mbinu alizotumia Muchemi alipochunguza mtagusano wa lugha ya Kiingereza na Kikuyu. Utafiti huu unachunguza mtagusano wa lugha ya Kiswahili na sheng' ukitumia mbinu hizo. Tofauti ni kuwa, sampuli yake ni ya wanafunzi wa shule za upili ilhali yetu ni wanafunzi wa Chuo Kikuu.

Kutokana na tafiti za Miguda (2003), Muchemi 2011, Babusa (2010), Chomba (2013) na Kamau (2015) ni wazi kuwa umilisi wa kiisimu katika lugha moja huathiriwa na mtagusano wa lugha nyingine kama ilivyoelezwa. Tafiti hizi zina mchango mkubwa kwa utafiti huu kwa sababu kutokana na tafiti hizi utafiti huu unaelewa jinsi mtagusano wa lugha ya Kiingereza na sheng' huathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Tafiti hizi zote ni za isimujamii ilhali utafiti huu ni wa isimu tumikizi.

2.3.3. Changamoto katika umilisi wa kiisimu katika lugha.

Madhumuni ya nne ya utafiti huu ni kuchunguza changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa isimu katika lugha ya Kiswahili katika vyuo vikuu. Kitsao (1978) anaeleza kuwa asilimia kubwa ya wanafunzi wa lugha ya Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya hawafanyi vizuri katika somo la isimu tukilinganisha na masomo mengine yanayofundishwa na idara zetu za Kiswahili na lugha za Kiafrika. Akilalamikia mafunzo ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi, alisema kuwa chuo hakina vipindi vya mafunzo ya Kiswahili. Kwa sababu inachukuliwa kuwa wale wanaokuja kwa masomo ya Kiswahili katika chuo hicho huwa tayari wameshapata msingi wa kutosha wa lugha hii. Hivyo, kuwafundisha Kiswahili darasani itakuwa kuwapotezea muda na kuwafundisha tena mambo wanayoyajua.

Sultani (1976) alilalamikia mambo haya aliposema kuwa mafunzo mengi yanayohusika na sayansi ya lugha huwa magumu kwa wanafunzi hasa wanapofunzwa na walimu ambao wana-

tumia lugha ngumu isiyofahamika. Lugha hii ngumu inayodaiwa na wanafunzi ni zile istilahi tofauti zinazotumika. Mielekeo na fikira hizi mbovu zimeathiri wanafunzi wengi. Shida nyingine inayokabili somo la isimu ni utata na wingi wa istilahi. Buliba (1998) anasema kuwa wahadhiri katika vyuo vikuu mbalimbali hutumia istilahi zinazotofautiana kuzungumzia dhana ileile moja. Hali hii ya kutumia istilahi tofauti kwa dhana ile moja huzua utata kwa wanafunzi wa isimu katika Kiswahili na hufanya umilisi wao katika isimu kuwa wa kiwango cha chini.

Vitabu vinavyoshughulikia somo la isimu na lugha ya Kiswahili hutumia istilahi zinazokanganya. Zaidi ya hayo waandishi kutoka nchi tofauti kama Tanzania na Kenya hutumia istilahi tofauti. Tatizo hili la istilahi linazua wasiwasi kati ya wanafunzi ambao wanakanganywa na wingi wa istilahi na kuhitilafiana kwake. Hali hii huzua hisia na mielekeo hasi kuhusu kozi za isimu huku wanafunzi wakiziogopa na wengine wakizichukia. Matokeo yake ni kuanguka au kuponea chupuchupu katika mitihani yao ya isimu wanayoifanya katika chuo.

Buliba (keshatajwa) anaongezea kuwa, dhana nyingi za kiisimu hutokana na tafsiri ya Kiingereza. Wahadhiri wengi hujaribu kuzitafsiri na kuzitolea maelezo mwafaka. Tafsiri hizi huenda hazifikii kile kiwango kamili cha kuzieleza dhana zile kwa uwazi na ukamilifu. Zaidi ya hayo, makisio huenda yakatumiwa katika juhudi za kufikia zile tafsiri kamili au tafsiri zinazoridhisha. Jambo hili limewalemea wanafunzi na walimu wa isimu katika Kiswahili. Makala na maandishi mengine yanayoshughulikia isimu kwa Kiswahili hayapatikani kwa urahisi. Uhaba wa maandishi umefanya maendeleo ya isimu katika lugha ya Kiswahili kuwa haba mno. Inastaajabisha kusema kuwa, hadi kufikia mwaka wa 1976 TUKI haikuwa na sehemu ya isimu katika jarida lake *Mulika*. Majarida mengine yanayoshughulikia isimu katika Kiswahili ni ya kutoka Tanzania. Hali nchini Kenya haitajiki, majarida si mengi, twaweza

kutambua tu *Baragumu* katika Chuo Kikuu cha Maseno lililoshughulikia fasihi na isimu lakini sasa hivi jarida hili halichapishwi tena. Kwa ujumla, uchache wa machapisho mengi ya isimu upo kwa sababu ya kisingizio kuwa huenda vitabu, majarida na maandishi mengine ya-sipate soko.

Buliba (keshatajwa) anaongezea kusema kuwa, muda uliotengewa kozi za isimu katika baadhi ya vyuo vikuu ni mchache mno tukilinganisha na upana wa nyanja tofauti tofauti za isimu kama vile: fonetiki, fonolojia, mofolojia, semantiki na pragmantiki. Kwa miaka mingi isimu katika lugha ya Kiswahili ilifundishwa kwa Kiingereza. Hali hii lilizorotesha umilisi wa isimu, ingawa wakati huu isimu hufundishwa katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo bado makala mengi yangali yameandikwa kwa Kiingereza na jambo hili bado linaathiri umilisi wa kiisimu katika Kiswahili. Kwa upande wa utafiti ni wazi kuwa isimu katika Kiswahili haitiliwi mkazo. Kazi nyingi za uzamili na uzamifu hulenga kozi za fasihi. Kwa mujibu wa Musau na Ngugi (1997), ni kazi chache tu zinazoshughulikia isimu ya Kiswahili. King'ei (2000) anaeleza kuwa kazi nyingi za utafiti zilizo za uzamili zimeandikwa kwa Kiingereza. Anasisitiza kuwa katika historia ya usomi ya Kenya hadi kufikia wakati alipoandika makala yake ni kazi mbili tu za uzamifu ambazo zilikuwa zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi. Hii inaonyesha kuwa wasomi wengi hukwepa kufanya utafiti katika Kiswahili kwa sababu ya ugumu wake na huegemea katika Kiingereza. Hali hii huenda ilitinga kunawiri kwa isimu katika lugha ya Kiswahili, ingawa kufikia sasa kuna tasnifu nyingi ambazo zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Mtalaam Mathooko (2000) anapendekeza kuwa, kwa sababu ya shida nyingi zinazoikumba lugha ya Kiswahili na isimu katika Kiswahili, kuwe na kusawazisha na kusanifisha katika viwango vyote vya usanifishaji ili kuimarisha kozi za isimu kwa Kiswahili vya vyuo. Kusawa-

zishwa huku kutashirikisha istilahi zinazotumiwa katika mihadhara na wahadhiri mbalimbali na katika maandishi kama vile makala na vitabu. Pia anaomba ushirikiano kati ya wapenzi wa Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki ili kusawazisha istilahi za kiisimu. Mathooko anaongezea kwa kusema kuwa serikali ya Kenya itasaidia sana ikiwa itaitikia mwito wa wasomi kuwa iunde Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili nchini Kenya. Waandishi, wachapishaji na watafiti wanapaswa kutilia maanani kazi za kiisimu. Wanafunzi watafaidika na kazi hizi na ile shida ya kufahamu mambo ya kiisimu itarahisishwa. Hii ni kwa sababu wanafunzi watajisomea mambo haya moja kwa moja kwa lugha ya Kiswahili na sio kujifasiria istilahi na dhana kwa Kiingereza kisha kuzitolea tafsiri kwa Kiswahili. Isimu katika Kiswahili isichukuliwe tu kama uchanganuzi wa lugha bali itazamwe katika uhusiano wake na mawanda mengine ya maisha halisi kama vile: uhusiano wa isimu na wanafunzi na walimu, uandishi wa magazeti, vitabu na majarida, utangazaji na tafsiri. Vilevile nadharia mbalimbali za kiisimu zapaswa kufundishwa kwa uangalifu.

Kuhusu sera ya lugha ya kufunzia kozi za isimu katika Kiswahili, kila Chuo chapaswa kutoa sera kamili na kila kozi ifunzwe katika Kiswahili. Hata hivyo ni vyema ifahamike kuwa vyuo vingi nchini Kenya vimeanza kutekeleza suala hili la kufunza isimu ya Kiswahili katika lugha ya Kiswahili. Mwisho, yafaa mitihani ya isimu katika Kiswahili ihusishe zaidi uchanganuzi wa data na mbinu mbalimbali za mijadala na ulinganishi.

Kulingana na maoni haya ya Mathooko, ni muhimu kuelewa kuwa isimu katika Kiswahili huenda isiwe inafundishwa katika vyuo kwa kutumia istilahi za Kiswahili kwa sababu vitabu vingi vya isimu bado havijatafsiriwa katika Kiswahili na vile ambavyo vimeandikwa na wataalamu ni vichache na haviwezi kutosheleza mahitaji ya kiisimu. Maoni yake haya yanasaidia mtafiti kuelewa kuwa kulikuwa na upungufu wa ufundishaji wa isimu katika Kiswahili

kwa miaka ya nyuma katika vyuo vikuu. Utafiti unataka kujua maendeleo yamefikia wapi mpaka sasa wakati ambapo inaaminika kuwa isimu hii sasa imeanza kufundishwa katika lugha ya Kiswahili. Tukisha elewa hayo basi tunaweza kukadiria viwango vya umilisi katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya ili kuweka mikakati ya kuboresha viwango vya chini.

2.4. Dhana na ujenzi wa mielekeo

Mielekeo hujengwa kutokana na hali inayomkumba binadamu katika maisha. Kama vile: Kuzungumza, kusoma, kukua na kupata maarifa. Mielekeo vilevile hukua, hupungua na hui-marika mtu anapozidi kuongeza maarifa katika shughuli mbalimbali. Mtu huchukua mwelekeo fulani na kuushikilia mpaka anapobadili huo mwelekeo na kuchukua mwelekeo mwingine kuhusu jambo fulani kama asemavyo Sheriff (1965). Watu hujenga mielekeo kuhusu mambo mbalimbali maishani kwa mfano watu huwa na mielekeo kuhusu siasa, uchumi, utamaduni, elimu, kati ya mengine mengi maishani. Wao hufanya hivyo kwa sababu tofauti tofauti kama vile, mielekeo husaidia mtu kubadilika kulingana na mabadiliko ya kilimwengu.

Mtu hazaliwi na mielekeo bali hujenga kupitia maingiliano yake na shoga wake, jamii na hata pengine shuleni. Mfumo huu wa mielekeo hujumuisha uelewaji wa mielekeo na maadili (Holloran, 1967). Kulingana na mtaalamu huyu kuna aina tatu za mielekeo nazo ni: tajriba ya moja kwa moja, pili mtu kujifunza kutoka kwa mtu mwingine na ujenzi wa tabia za mtu husika. Triendla (1971) aligawa mielekeo katika vigezo vitatu:

Ufahamu, hisia na vitendo. Sehemu ya ufahamu ni ile ambayo mtu anajenga imani juu ya jambo fulani. Ikiwa imani yake ni kubwa yeye atakuwa na mwelekeo mkubwa lakini imani ikiwa ndogo mwelekeo wake utakuwa wa chini. Mtu hujenga hisia fulani juu ya jambo fulani linalohusika, kama ufahamu huo unamfurahisha basi atakuwa na mwelekeo chanya kuhusu

jambo fulani na ikiwa ufahamu unamuudhi basi atakuwa na hisia duni juu ya jambo hilo na kuwa na mwelekeo hasi. Sehemu ya mwisho ni pale ambapo baada ya kupata ufahamu na kujenga hisia, mtu hudhihirisha hisia zake kwa vitendo vyake. Ufahamu wa mielekeo katika umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili ulifaa utafiti huu kwa sababu umesaidia kuelewa jinsi aina mbalimbali za mielekeo huathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

2.4.1. Mielekeo kuhusu lugha

Edwards (1982) anasema kuwa wazungumzaji wa lafudhi zilizokubalika na wengi huheshimiwa na wale wanaozungumza lafudhi zisizokubalika hawaheshimiwi. Fasold (1984) anaeleza kuwa mielekeo kuhusu lugha fulani huwa ni makisio ya mielekeo kuhusu makundi tofauti ya kikabila. Mwelekeo ni kigezo cha kidhahania kinachotumiwa kueleza njia na msisitizo wa tabia za binadamu kama asemavyo (Baker 1992). Crystal (1992) anadai kuwa mwelekeo huwa ni hisia walizonazo watu juu ya lugha yao na lugha za watu wengine. Mwelekeo huwakilisha fikira iliyo fiche, hisia na mikondo ya hisia za mtu katika shughuli tofauti tofauti. Katika kujifunza lugha mtu huwa na uhusiano wa karibu na mielekeo kuhusu lugha hiyo kama asemavyo Patridge (1996). Mielekeo ina majukumu muhimu katika kuikuza na kuiboresha lugha hiyo.

2.4.2. Tafiti kuhusu umilisi na mielekeo ya lugha nyingine

Kutokana na tafiti ambazo zimefanywa juu ya mielekeo ya lugha duniani hususan, Fahmy na Bilton (1990), Tan (1990), Shim (2002), Kim (2007), mtafiti anafafanua na kueleza mchango unaotokana na kazi hizo huku akibainisha tofauti na utafiti huu. Tafiti hizi zilizotajwa zimehibitisha kuwa wanafunzi hujenga mielekeo chanya na kuipenda lugha ambayo inaonekana kuwa na hadhi ya juu au faida fulani. Lugha ikitumiwa kama lugha ya shughuli za kiserikali kama bungeni, mahakamni au kufundishia hadhi ya lugha hii huwa juu na hivyo wanafunzi

watapata motisha ya kujifunza lugha hiyo, lakini ikiwa lugha haitakuwa na umuhimu maishani basi mielekeo yao huwa hasi na matumizi ya lugha hudidimia. Fahmy na Bilton (1990) walichunguza mielekeo ya wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Omani kuhusu matumizi ya Kiingereza kama lugha ya kufundisha sayansi. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa wanafunzi walikuwa na mwelekeo mzuri kuhusu Kiingereza kwa sababu walijua kuwa lugha hii ingewasaidia kupata kazi baada ya masomo yao kuliko lugha ya kienyeji. Utafiti mwingine wa Tan (1990) ulichunguza mielekeo ya wanafunzi wa vyuo vikuu vya Malasya kuhusu lugha ya Kiingereza kama lugha ya masomo. Matokeo ya uchunguzi yameonesha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza kwa sababu walijua kuwa lugha hii ya Kiingereza ingewasaidia kuwapa kazi nzuri baada ya masomo. Mwelekeo wao huu mzuri uliwafanya wawe na bidii sana katika masomo yao.

Buscherhofer (1998) naye akichunguza wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Papua New Guinea kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili alipata kuelewa kuwa wanafunzi walipenda Kiingereza cha Marekani kwa sababu ya hadhi yake na walikuwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha hii, hivyo iliwafanya wapende Kiingereza cha Marekani zaidi kuliko lugha yao ya kwanza. Hali hii iliwafanya wafanye vyema katika mitihani yao ya Kiingereza kwa sababu walijua kuwa Kiingereza kingewafaidi maishani.

Shim (2002) alifanya utafiti kuhusu Kiingereza kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya Korea. Matokeo yameonesha kuwa, wanafunzi walikipenda Kiingereza kuliko lugha yao ya Kikorea. Mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiingereza ilikuwa chanya kwa sababu wanafunzi walikuwa na hamu ya kutaka kujifunza Kiingereza cha kimataifa kuliko lugha yao. Walipendelea sana Kiingereza cha Amerika ili waonekane kama wanaishi Marekani na wazungumze kama Wamerika. Mtalaamu mwingine aliyeshughulikia suala la mielekeo ni Fredrich (2003) ali-

yechunguza mielekeo ya wanafunzi katika nchi ya Argentina kuhusu matumizi ya Kiingereza. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa wanafunzi hao walipenda kutumia Kiingereza cha Marekani kwa sababu walikiona kuwa cha manufaa hasa upande wa kupata kazi huko Marekani na wakawa na mielekeo chanya kuhusu lugha hii ya Kiingereza.

Kim (2007) alitafitia mielekeo ya wanafunzi wa Kikorea kuhusu Kiingereza cha kienyeji na Kiingereza cha kimataifa. Matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa waliotafitiwa walikiona Kiingereza cha kimataifa kuwa na hadhi ya juu na walikuwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha hii. Wasailiwa walikiona Kiingereza cha kimataifa kuwa muhimu katika shughuli ya kimawasiliano nchini mwao na nchi zingine. Karaha (2007) alitafiti mielekeo ya wanafunzi katika shule za msingi nchini Uturuki kuhusu matumizi ya Kiingereza katika masomo yao. Matokeo ya utafiti huo yameonesha kuwa asilimia kubwa ya wanafunzi katika nchi hii ya Uturuki wana mwelekeo hasi kuhusu Kiingereza na matumizi yake katika masomo. Wao walikipendelea Kituruki zaidi kuliko Kiingereza.

Utafiti mwingine ni ule uliofanywa na Siregar (2009) alichunguza mielekeo ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maranadha kuhusu Kiingereza. Alipata kuelewa kuwa wanafunzi walionyesha mielekeo chanya kuhusu Kiingereza kama lugha ya kufundisha kwa sababu walijua kuwa Kiingereza kingewafaidi katika shughuli nyingi maishani. Hii iliwafanya wawe na mielekeo hasi kuhusu lugha yao ya Kiindonesia kwa sababu hawakuona umuhimu wa lugha ya Kiingereza.

Tafiti hizi za Shim (2007), Kim (2007), Karaha (2007) na Siregar (2009) zilitoa ushahidi kuwa mielekeo na sera ya lugha huwafanya wanafunzi kuipenda lugha kwa sababu mbalimbali kama vile ajira, masomo, mawasilano na kujiona wao kuwa watu wenye busara kwa kutumia

lugha hiyo. Tafiti hizi zinaeleza kuwa mwelekeo ni kigezo muhimu katika kuelewa hamu walionayo wanafunzi katika kujifunza lugha. Utafiti

huu unalenga kuchunguza mwelekeo walionayo wanafunzi katika kujifunza isimu ya lugha ya Kiswahili na tafiti hizi ni muhimu katika utafiti huu wetu.

Kimemia (2001) anasema kuwa Kiingereza kimepewa hadhi kubwa nchini Kenya. Wanafunzi wengi huwa na mielekeo chanya katika kujifunza lugha hii, kwa sababu wanajua kuwa kuelewa Kiingereza kutawafaidi maishani. Hoffman (1977) alichunguza mielekeo ya watu wazima wa kabila la Washona nchini Zimbabwe. Alipata kuwa walikuwa na mwelekeo hasi kuhusu Kiingereza na mwelekeo chanya kuhusu Kishona. Hii iliathiri mwelekeo wao kuhusu Kiingereza walichokizungumza. Kwa sababu hawakuona umuhimu wa kujifunza lugha ya Kiingereza na hii ikawafanya wawe na mielekeo hiyo. Ngara (1982) alichunguza mielekeo ya wanafunzi wa kidato cha tatu katika nchi ya Zimbabwe na alipata kuelewa kuwa washona walikuwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kishona kuliko lugha ya Kiingereza na walikipenda kishona zaidi kuliko Kiingereza. Hali hii iliathiri umilisi wao wa lugha ya Kiingereza.

Woods (1985) alifanya utafiti kuhusu mielekeo ya lugha ya Kikongo kwa watu wa umri tofauti nchini Kongo. Matokeo ya utafiti huu yameonesha mielekeo tofauti kuhusu miktadha mbalimbali kama vile: Tabia na imani. Matokeo yameonesha mielekeo tofauti kulingana na imani tofauti ingawa utafiti huu haukushughulikia umilisi wa lugha ya wakongo, unasaidia kuelewa mielekeo ya imani kuhusu lugha hiyo ya Wakongo na jinsi ilivyopendwa na wananchi. Utafiti wa Woods umeonesha kuwa vijana wana mielekeo tofauti katika lugha ya kigeni, mfano Kifaransa kilipendwa na vijana kuliko wazee. Mwelekeo wa vijana kuhusu Kifaransa ulikuwa chanya ilhali mielekeo ya wazee ilikuwa hasi. Sababu ni kuwa vijana walipenda

Kifaransa kwa sababu tofauti tofauti, kama vile kupata ajira nchini Ufaransa, nao wazee hawakuona umuhimu wa lugha ya Kifaransa na hivyo msimamo wao ulikuwa hasi kuhusu lugha ya Kifaransa.

Mwanaisimu Mparutsa (1986) alifanya utafiti kuhusu wakaazi wa Harare nchini Zimbabwe kuhusu mwelekeo wa lugha ya Kiingereza. Matokeo ya utafiti wake yameonesha kuwa ingawa Kiingereza kilitumiwa serikalini na katika elimu, watu wengi walikuwa na mwelekeo chanya kuhusu Kishona na sio Kiingereza. Hii iliwafanya kutumia Kishona katika shughuli zao nyingi na hali hii ilifanya umilisi wao wa lugha ya Kiingereza kuwa duni.

Tafiti hizi za nchi ya Zimbabwe zinahusu lugha ya Kiingereza na Kishona na zinahusisha wanafunzi wa shule na vyuo na hata wenyeji. Utafiti wetu unachunguza wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno na haulinganishi lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo utafiti wa Ngara unatufaa sana kwa sababu tunaweza kuonesha mwelekeo chanya kuhusu Kiswahili na kupandisha hadhi yake ili iwe sawa na ya Kiingereza kama wanavyofanya Washona na lugha ya Kishona.

Watalaamu Gorman (1974), Onyango (1990), Okwanyi (1993), Mohochi (2006) na Munialo (2009) nchini Kenya walifanya utafiti juu ya mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili na Kiingereza na athari za mielekeo hii kuhusu lugha hizi mbili. Utafiti huu unadurusu tafiti hizi na kuona jinsi zinavyotofautiana na utafiti wetu. Gorman (1974) akifanya utafiti kuhusu mielekeo ya Kiswahili nchini Kenya alipata kuelewa kuwa wanafunzi wanaonesha mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Pia aligundua kuwa wanafunzi hawakuonesha ari ya kujifunza Kiswahili kama walivyofanya kuhusu Kiingereza. Alipata kufahamu kuwa wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali za nchi wana umilisi tofauti kuhusu lugha ya Kiswahili-

li. Onyango (1990) alifanya uchunguzi kuhusu mielekeo ya wasomi wa Kiswahili na matumizi yake nchini Kenya. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na Kiingereza. Okwanyi (1993) alifanya utafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya kuhusu lugha ya Kiswahili. Hii ilikuwa karibu miaka minane baada ya Kiswahili kufanywa somo la lazima na kuweza kutahiniwa. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa wanafunzi wa shule za upili walikuwa na mielekeo tofauti kuhusu lugha ya Kiswahili, kuna wale walio na mielekeo chanya kuhusu lugha na wale walio na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili.

Mtalaam Mohochi (2006) alifanya utafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa Kiswahili katika mtihani wa kidato cha nne mkoa wa Pwani na Nyanza. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa wanafunzi wa mkoa wa Pwani walikuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na wenzao wa mkoa wa Nyanza ambao walikuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wa mkoa wa Pwani walikitumia Kiswahili katika shughuli zao nyingi kuliko wanafunzi wa mkoa wa Nyanza ambao wengi walikipenda Kiingereza na lugha za kwanza.

Mtafiti Munialo (2009) akifanya utafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili katika wilaya ya Rachuonyo mkoani Nyanza, alipata kuelewa kuwa wanafunzi katika shule za wilaya hii walikuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili na hii iliwaathiri katika shughuli za kimasomo na mitihani yao. Pia alifahamu kuwa wanafunzi wa kike walikuwa na mielekeo chanya kuliko wenzao wa kiume ambao walikuwa na mielekeo hasi. Hii iliwafanya wasichana kuwa na umilisi mkubwa wa lugha ya Kiswahili kuliko wenzao wa kiume na walifanya vizuri katika mtihani wa kitaifa kuliko wale wa mkoa wa Nairobi.

Vigezo alivyovitumia Babusa ni jarabati katika maandishi na mazungumzo. Kutokana na tafiti hizi ni wazi kuwa mambo mengi yameshughulikiwa kuhusu mielekeo ya wanafunzi katika mikoa mbalimbali nchini Kenya. Tafiti hizi zinalinganisha mielekeo ya Kiswahili na Kiingereza katika shule za upili. Kutokana na maelezo haya hakuna utafiti ambao umefanywa juu ya mielekeo kuhusu umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno. Utafiti huu unanua kueleza jinsi mielekeo huathiri umilisi wa kiisimu miongoni mwa wanafunzi wa isimu ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno.

2.5. Historia ya ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya

Mathooko (2002) anasema kuwa vyuo vingi nchini Kenya vimekuwa vikifundisha Kiswahili kwa wanafunzi wake kama somo kwa wale wanaochaguliwa katika idara ya Kiswahili. Inga-wa somo hili limepewa nafasi katika vyuo kwa kutengewa idara kamili, vyuo vingine vimechukua Kiswahili na kukiweka katika idara ya Kiingereza na lugha nyingine. Idara ya isimu na lugha ilianzishwa katika Chuo Kikuu cha Nairobi mnamo mwaka 1969. Kufikia mi-aka ya themanini vyuo vikuu vingine kama vile Kenyatta na Egerton vilianzisha Idara ya Kiswahili ambapo Fasihi, Lugha na Isimu kwa Kiswahili ilifundishwa. Hali hii ilifanya isimu katika Kiswahili kuimarika.

Katika ripoti ya Mackay (1984) iliyopendekeza kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha pili nchini Kenya, ripoti hii ilipendekeza kuwa Kiswahili kifundishwe katika vyuo vyote na kwa wanafunzi wote bila kujali ni kozi zipi walikuwa wakifanya. Chuo Kikuuu cha Maseno kilikuwa na Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika na baadaye kikaanzisha idara iliyojisimamia ya lugha za Kiafrika. Lugha zilizofundishwa zilikuwa Kikalenjin, Kiluhya, Dholuo na Ekegusi. Lakini baadaye idara hizi zilifanyiwa mabadiliko na kuwekwa katika masomo mengine kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani. Hii ilifanyika katika vyuo vikuu vya Nairobi na

Kenyatta. Vyuo Vikuu vya Moi, Maseno na Egerton vina Idara ya lugha, Isimu na Fasihi, Mpangilio huu ulidunisha Kiswahili na kukifanya kurudi nyuma ukilinganisha na Kiingereza au Kifaransa kama asemavyo Mathooko (2002).

2.6. Pengo la utafiti

Kwa ujumla umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili ni suala ambalo ni changamano. Licha ya kuwa lugha hii ilianza kutafitiwa toka miaka mingi iliyopita katika maeneo tofauti, tafiti hizo hazijatosheleza kwani bado kuna maeneo mengi kama vile: Fonetiki, fonolojia na mofolojia yanahitaji kufanyiwa utafiti. Kwa uelewa wa mtafiti hadi sasa hakuna utafiti wowote uliyoandikwa kuhusu uchanganuzi wa umilisi wa kiisimu katika lugha Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno. Hata hivyo wanafunzi hutofautiana katika umilisi wa stadi za kiisimu. Utafiti huu una nafasi ya kutathmini utoshelevu ya Nadharia ya Umilisi wa Kiisimu katika kutafiti maswala ya ufunzaji na ujifunzaji kwa uangavu wa kutosha. Pia kuchanganua umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa vyuo vikuu, changamoto na athari zake katika lugha ya Kiswahili.

2.7. Hitimisho

Sura hii imeangazia umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili, watalaamu wengi wamelishughulikia suala la umilisi wa kiisimu wa lugha mbalimbali. Umilisi wa mawasiliano katika lugha umeangaziwa, upimaji wa umilisi, umilisi wa uchanganuzi usemi na mielekeo kuhusu umilisi wa lugha umeshughulikiwa. Tafiti ambazo zimefanywa na watalaamu mbalimbali kuhusu umilisi na mielekeo zimeangaziwa kwa mapana. Kutokana na tafiti hizi imebainika wazi kuwa kuna vipimo tofauti vya kupimia umilisi wa kiisimu kama vile; jarabati, kuwapa majukumu, mazungumzo na vipimo vya ujuzi hisa katika stadi nne za lugha ambazo ni: Kusoma, kuzungumza, kusikiliza na kuandika. Mbinu za uchunguzi zinazotumiwa na tafiti hizi

kama vile usaili na hojaji zinatumiwa katika utafiti huu. Aidha, vipengee vinavyoonesha badiliko la umilisi wa kiisimu katika utafiti wa awali vimetumiwa kutokana na mitihani ya kuandika na kuzungumza. Athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu kutokana na mtagusano wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine zimeangaziwa. Sheng' imeonekana kuathiri umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili katika sehemu tofauti kama vile: Kimsamiati, kifonolojia, kisemantiki na kisintanksia. Changamoto ambazo zinaathiri umilisi wa kiisimu vilevile zimeoneshwa kwa mfano: Matamshi mabovu, lafudhi, kusitasita katika mazungumzo, kudiarudia maneno katika kusoma makala na sarufi mbaya katika sentensi. Matatizo mengine yanayotinga umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili yameelezwa. Matatizo haya yameoneshwa kama: ukosefu wa vitabu vya isimu vilivyoandikwa kwa Kiswahili, istilahi ngumu na tofauti za isimu, mielekeo ya wanafunzi na matumizi ya sheng' yanachangia katika kudorora kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Maeneo tofauti yamefanyiwa utafiti katika tafiti za awali. Mbinu ambazo zimezotumiwa katika utafiti wa awali zimetufaa katika kuchanganua data. Pengo la utafiti limebainishwa. Sura ifuatayo inashughulikia mbinu na njia za utafiti.

SURA YA TATU

NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

3.1. Utangulizi

Sura hii inaeleza mbinu zinazotumiwa katika utafiti huu. Mbinu hizo ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi linalotafitiwa, namna ya kukusanya data, usampulishaji, mbinu za kuchanganua, kufasili na kuwasilisha data.

3.2. Muundo wa Utafiti

Utafiti huu unazingatia muundo wa mkingamo ambapo hutumiwa kuchunguza data inayopatikana kwa wakati na muda maalum kuhusu mada husika. Data hii inapatikana kutokana na makundi tofauti na mashirika makubwa makubwa (Lee 1994). Muundo huu wa mkingamo unaelezwa na Mtaalam Ilomak (2005), kuwa ni kifaa cha utafiti kinachotumiwa kukusanya habari kutoka kwa washirika wengi kwa wakati mahsusi. Data hii hutokana na washiriki wenye uwezo na tabia tofautitofauti. Muundo huu unamwezesha mtafiti kulinganisha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na mwaka wa nne. Muundo huu unachunguza wahusika kulingana na miaka, jinsia, mapato na viwango vya elimu. Muundo huu unafaa utafiti huu kwa sababu unachunguza viwango vya umilisi wa kiisimu, viwango vya kielimu na kijinsi.

3.2.1. Mbinu ya kithamano

Utafiti wa kithamano unaeleza na unachanganua maandishi kama yanavyopatikana katika usaili. Marshall (1996) anasema kuwa, utafiti wa kithamano ni bora zaidi kutokana na sifa yake ya kushughulikia masuala kwa undani zaidi. Uzuri wa kutumia mbinu ya kithamano katika utafiti huu ni kuwa: Utafiti wa kithamano ni muhimu katika kueleza masuala yenye

utata. Suala la umilisi wa kiisimu linajitokeza kuwa na utata mwingi kulingana na namna wataalamu mbalimbali wanavyolieleza. Utata huu hutokana na sifa za kijamii na utamaduni unaozunguka matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. Utafiti huu unaeleza suala la umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno na mbinu hii inashughulikia ufahamu wa suala na kutoa maelezo bila kupotoshwa na masuala au tajriba za kibinafsi ambazo huenda ziathiri matokeo ya utafiti.

Mtafiti anaweza kutaka kueleza suala kwa njia fulani lakini hali halisi ya namna mambo yalivyo inamlazimu kuyaeleza vinginevyo. Hata hivyo mbinu hii ina udhaifu wake kwa sababu huchukua muda mwingi kukusanya na kuchanganua data. Pia huenda utafiti uathiriwe na mitazamo finyu ya mtafiti ambaye huenda apendelee upande fulani wa utafiti zaidi kuliko upande mwingine. Mbali na udhaifu huu mbinu hii ndiyo inafaa utafiti huu kutokana na malengo yake ya kutaka kupata undani na uhalisia wa suala nzima la namna umilisi wa kiisimu hufaulisha mawasiliano katika Chuo Kikuu.

3.2.2. Mbinu ya Kiwingi idadi

Mbinu hii inatumiwa kutoa data ya kihisabati au ya nambari. Mbinu hii inaweza kujibu maswali kama vile; ni wangapi? Au ni idadi gani?. Majibu ya maswali haya huwa ya idadi kamili kama vile kumi, tano, ishirini au idadi isiyodhihirika kama vile, wachache au wengi. Mbinu hii inatumia maswali funge ili kupata data kamili. Kwa mfano kupata data kuhusu viwango vya umilisi wa kiisimu vya wanafunzi inapatikana kupitia majibu ya jarabati ya wanafunzi wa mwaka wa nne. Idadi ya wanafunzi wanaopata alama za wastani au juu inajulikana kupitia maswali kama; Ni wanafunzi wangapi ambao walipata alama za wastani? Au ni wanafunzi wangapi ambao wana viwango vya chini vya umilisi wa kiisimu wa lugha

ya Kiswahili? Hata hivyo mbinu hii haitakueleza kwa nini idadi hiyo ya wanafunzi inapata viwango hivyo.

Ukusanyaji na uchanganuzi wa data kitakwimu unaonekana kutekelezwa kwa haraka kuliko ya kithamano. Isitoshe, matokeo ya utafiti wa kitakwimu aghalabu hayazingatii mitazamo ya kibinafsi ya mtafiti. Matokeo yanachanganuliwa jinsi yalivyo kupitia mtindo wa mbinu za kati. Utafiti huu unajitokeza kuwa bora zaidi katika kuchunguza idadi kubwa ya matukio ambayo yanaweza kuleta utata katika uchanganuzi wa kithamano. Kila utafiti una malengo mbalimbali ya utafiti ambapo baadhi ya malengo huafikiwa kupitia mbinu za kithamano na mengine mbinu za kitakwimu.

Katika utafiti huu lengo la pili linaafikiwa tu kwa kutumia mbinu za kihisabati ilhali yale mengine yote kithamano. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti anaweza kupata data ya kitakwimu kutokana na jarabati ya wanafunzi. Mbinu zote mbili huchangiana kwani upungufu wa mbinu moja unaweza kushughulikiwa na mbinu nyingine. Utafiti wa kithamano unaeleza kwa undani umilisi wa kiisimu na changamoto wanazopitia wanafunzi ilhali utafiti wa kiwingi idadi nao unatoa takwimu za viwango mbalimbali vya umilisi wa kiisimu wa wanafunzi. Ni muhimu kuelewa kwamba kila mbinu ina uzuri wake na ubaya, hivyo basi huweza kufidiana katika harakati za kufaulisha malengo yote ya utafiti.

3.3. Eneo la utafiti

Eneo la utafiti huu ni Chuo Kikuu cha Maseno nchini Kenya. Chuo hiki kinapatikana kilomita ishirini na tano kutoka mji wa Kisumu katika barabara kuu ya kutoka Kisumu hadi Busia. Hiki ni chuo cha kiserikali na hufundisha kozi nyingi, Kiswahili kikiwemo. Utafiti

unafanywa katika idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika chuo hiki. Sehemu ya isimu inashughulikiwa ikiwa ni uchanganuzi wa sentensi changamano.

3.4. Kundi lengwa

Walliman (2011) anafafanua kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti (vinavyotafitiwa), yaani watu, taasisi, vitu au matukio. Kwa ujumla, kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa. Hivyo, kundi lengwa katika utafiti huu ni wanafunzi wa isimu katika Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Maseno Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika na wahadhiri wanaunda idadi lengwa ya utafiti huu. Wanafunzi wanaoshiriki katika utafiti huu ni wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wanafunzi wa mwaka nne. Vilevile wahadhiri wanashiriki katika utafiti huu. Walengwa hawa wanachaguliwa kwa sababu ndio wenye uwezo wa kutoa taarifa zinazohitajika katika utafiti huu.

3.5. Sampuli na Usampulishaji

Sehemu hii inashughulikia sampuli ya utafiti na namna sampuli hiyo inavyoteuliwa.

3.5.1. Sampuli ya Utafiti

Kothari (2004) anafafanua sampuli kuwa ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo kwalo mtafiti hupata data na kutoa mahitimisho yake. Utafiti huu unahusisha sampuli ya watafitiwa 124 kutoka kundi nzima la watu 412, kati ya hawa wanafunzi 220 ni wa mwaka wa kwanza na 66 wanaoshiriki ambayo ni asilimia 30. Wanafunzi 180 ni wa mwaka wa nne na 55 wanashiriki ambayo ni asilimia 30. Hii ni sampuli ya asilimia 30 ya wale wote wanaoshiriki katika utafiti huu. Pia utafiti unahusisha wahadhiri watatu kutoka idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika ambayo ni asilimia 30. Kila

mwanafunzi wa nne katika orodha ya usajili anateuliwa kushiriki katika utafiti katika mwaka wa kwanza na mwaka wa nne.

3.5.2. Jedwali 1. Idadi ya sampuli ya watafitiwa

Sampuli	Idadi	Watafitiwa	Asilimia
Wanafunzi wa mwaka wa 1	220	66	30
Wanafunzi wa Mwaka wa 4	180	55	30
Wahadhiri	12	03	30
Jumla	412	124	30

3.5.2 Mchakato wa Usampulishaji

Kwa mujibu wa Sigh (2007), usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Sampuli inachaguliwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na usampulishaji nasibu na usampulishaji usio nasibu.

Ruane (2005) anafafanua usampulishaji nasibu kuwa ni mchakato wa kuchagua sampuli ambapo uwezekano wa kuchagua mhusika yeyote katika kundi lengwa huwa mkubwa. Kwa maneno mengine usampulishaji nasibu ni mbinu ya kuchagua sampuli ambayo kila mamba katika kundi lengwa ana fursa sawa ya kuchaguliwa kuingia katika utafiti. Usampulishaji usio nasibu ni mchakato wa kuchagua sampuli ambao huegemea zaidi maamuzi ya mtafiti na hauwezi kutoa matokeo jumuishi kuhusiana na kundi lengwa. Yaani, ni mbinu ya kuchagua sampuli ambayo sehemu ya watafitiwa huchaguliwa kwa kuzingatia zaidi upatikanaji wao kuliko uwakilishi wao. Wahadhiri watatu wanachaguliwa kwa kuzingatia sampuli hii.

Moja kati ya sampuli inayopatikana kwa njia hii ni sampuli ya makusudi. Sampuli ya makusudi ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huichagua huku akiwa na matarajio kuwa itawakilisha kundi lengwa. Mtafiti anaamua kutumia aina hii ya sampuli katika utafiti wake kwa sababu anaamini kuwa kundi hili ndilo lenye uwezo wa kutoa taarifa faafu na wakilishi kwa kundi lengwa katika utafiti. Saunders na Lewis (2003), wanasema kuwa usampulishaji ni njia ya kuchunguza habari kutoka kwa watu wachache ambao watawasilisha idadi kubwa ya watu. Milroy (1987) anasema kuwa sampuli zinazotumiwa katika utafiti wa kiisimu ni wakilishi na matokeo yake huwa sawa kutokana na sampuli ndogo inayoteuliwa almuradi usampulishaji ufanywe vyema. Sampuli hii inateuliwa kwa sababu ni ridhishi kulingana na Chassan (1979), anayesema kuwa idadi ya asilimia ishirini au ishirini na tano ni ridhishi katika utafiti wa aina hii. Nao Alreck na Settle (1995) wanapendekeza idadi ya asilimia kumi ya sampuli kutumiwa. Mugenda (1999) anapendekeza kuwa sampuli nzuri huwa na asilimia 10-30 ya idadi inayochunguzwa. Mtafiti anajumuisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza kwa sababu ndio mwanzo wanajiunga na chuo na ni muhimu kujua viwango vya umilisi wao wa kiisimu katika Kiswahili. Nao wanafunzi wa mwaka wa nne wanajumuishwa kwa sababu wanaelekea kumaliza mtaala mzima wa kiisimu katika Chuo Kikuu cha Maseno na hivyo wako katika hali nzuri ya kuelewa kama umilisi wao wa lugha katika Kiswahili unaimarika au la.

3.6. Utafiti majaribio.

Utafiti majaribio umefanywa kupima uaminifu wa vifaa vya utafiti. Mtafiti ameshirikisha wanafunzi ishirini wa isimu ya Kiswahili ambao ni tofauti na wale wanaoshiriki katika utafiti huu. Mbinu ya jaribu- jaribu tena inatumika ambapo wanafunzi hawa wanapewa hojaji ya kujaza na wakarudishiwa tena kujaza ile hojaji mara ya pili. Fahirisi ya uaminifu imechanganuliwa na kukubaliana na Mugenda (1999) ambapo matokeo yanaonesha kuamini-ka.

3.7. Udhabiti wa vifaa vya utafiti

Katika utafiti huu mtafiti ameonesha viwango mbalimbali vya umilisi wa kiisimu vya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno. Mtafiti ameshauriana na wenzake katika idara na wasimamizi wake kuhusu uhalali wa vifaa na kama vingezalisha matokeo yanaokusudiwa. Watalaamu wengine kutoka Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine ya Kiafrika wameshauriwa kuhusu vifaa hivi na ikiwa vingefaa kwa utafiti huu. Vifaa vya kukusanya data vinafidiana na kuchangiana ili kuhakikisha kuwa data inayokusanywa inaaminika. Vile vile utafiti wa awali umeonekana kufaulu kwa kutumia vifaa hivi hususan, Babusa (2010), Macmanara (2000) na Kamau (2015). Orodha ya uchunzaji na jarabati ni baadhi ya vifaa vinavyotumiwa katika tafiti hizo na kufaulu na vinaweza kuaminika katika utafiti huu

3.8. Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti zinafanuliwa na Kothari (2004) kuwa ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Mbinu za utafiti ziko katika makundi makubwa mawili, ambayo ni mbinu za kukusanyia data na mbinu za kuchanganua data.

3.8.1. Mbinu za ukusanyaji data

Data ya msingi inakusanywa kupitia usaili, hojaji na jarabati ya isimu. Vifaa vinavyotumiwa kukusanya data ni: vifaa vya ipod kunasa mahojiano baina ya mtafiti na wahojiwa na maswali ya usaili. Tasnifu mbalimbali, mtandao, majarida na makala muhimu kwa utafiti huu. Mtafiti anahitajika kutembelea maktaba ya Chuo Kikuu cha Maseno na vyuo vikuu vingine ili kupata mapitio ya maandishi na kuyanakili kwa kalamu na karatasi.

3.8.1.1. Usaili

Kuna mahojiano ya ana kwa ana kati ya wasailiwa na msaili. Mahojiano ya wanafunzi yamesadia kuelewa ikiwa umilisi wa kiisimu wa wanafunzi unaimarika kwa kiwango kipi wanapoendelea kusoma katika chuo hiki. Data inayopatikana inasaidia kuafiki lengo nambari moja na nambari nne, ambapo lengo nambari moja linataka kujua kiwango cha umilisi na lengo nambari nne linataka kufahamu changamoto wanazokumbana nazo wanafunzi hawa wa isimu ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno nchini Kenya.

Kulingana na Cohen na Manion (1994), usaili ni mazungumzo ya watu wawili kwa sababu ya kupata data ya utafiti. Naye Weiner (2000) anasema kuwa usaili ni mazungumzo ya ana kwa ana kwa ajili ya kukusanya data kutoka kwa wasailiwa. Katika kuandaa na kushiriki katika usaili mtafiti anatilia maanani umuhimu na udhaifu wa usaili. Katika utafiti huu majibu ya wasailiwa hayaelekezwi na msaili, sampuli ndogo inatoa data inayoridhisha, kujulikana kwa msailiwa haikua shida kwa sababu anatoa data inayohitajika, gharama ya utafiti imepunguzwa kwa kutumia muda mchache katika usaili huu na msaili anajaribu sana kupunguza maswali wazi, ili data inapochanganuliwa isilete utata.

Aina mbili ya maswali yameulizwa, maswali ya wahadhiri na yale ya wanafunzi. Maswali ya wanafunzi yanasaidia katika kukusanya data kuhusu umilisi wa wanafunzi katika lugha ya Kiswahili. Maswali kumi kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza yameulizwa na majibu kuandikwa (Kiambatisho 2). Wahadhiri wameulizwa maswali kuhusu umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wanaowafunza katika Chuo Kikuu cha Maseno. Maswali haya ni wazi ili kuweza kupata data kamili kuhusu umilisi wa kiisimu wa wanafunzi (kiambatisho 1)

3.8.1.2. Hojaji ya wanafunzi wa mwaka wa nne

Madhumuni ya mbinu hii ni kupata picha halisi kuhusu umilisi wa kiisimu, kile kinachoonesha kuimarika kwa umilisi huu na changamoto ambazo wanafunzi wanakumbana nazo katika kusoma lugha hii ya Kiswahili. Mtafiti ametunga maswali ambayo yanaweza kueleweka kwa urahisi na ambayo ni funge. Kulingana na Norval (1990) anasema kuwa hojaji nzuri inafaa kuuliza maswali kuhusu suala la utafiti, iwe fupi na ya kueleweka kiurahisi na kila swali linafaa lishughulikie hoja moja. Kutokana na hojaji hii, utafiti umepata kupunguza gharama za utafiti, unaweka siri ya wahojiwa, wanaojaza hojaji wamepewa muda wa kutosha wa kujibu maswali kuhusu umilisi wa kiisimu, maswali ambao yameulizwa hayakuwakera wanaoshiriki katika kujaza hojaji na muundo wa hojaji ni rahisi ili kuwafanya wanaojaza kuwa na wakati mwepesi wa kujibu maswali hayo.

3.8.1.3. Jarabati ya mwaka wa nne

Wanafunzi wa mwaka wa nne wamepewa mtihani wa majaribio, wanafanya jarabati hii na imesahihishwa na majibu kuchanganuliwa. Jarabati imehusisha sehemu ya sintaksia ya Kiswahili ambapo wanafunzi wanaulizwa kuchanganua sentensi kwa kutumia mstari, majedwali na matawi. Mfano wa jarabati, mwongozo wa kusahihisha, baadhi ya karatasi za wanafunzi na matokeo yao yameoneshwa, (Kiambatisho 4). Sababu kuu za kuteua jarabati ya kisintaksia kwa wanafunzi wa mwaka wa nne ni kuwa: Sintaksia hushughulika na miundo ya sentensi na mwanafunzi anayeweza kuunda sentensi sahihi katika mazungumzo na maandishi huwa na umilisi wa kiwango cha juu katika lugha husika. Malengo ya kozi ya sintaksia ni: Baada ya kozi mwanafunzi awe na uwezo wa kutumia isimu tumikizi katika lugha ya Kiswahili, awe na maarifa ya kutafiti isimu na lugha ya Kiswahili na aoneshe umilisi katika isimu na lugha ya Kiswahili. Sentensi ya Kiswahili huundwa na Kiima na Kiarifa, hivyo mwanafunzi ambaye anaelewa mpangilio huu na kuweza kuutumia katika maandishi au mazungumzo huwa

anaimarika kiisimu katika lugha husika. Pili uchanganuzi wa sentensi huzua utata na hufanya wanafunzi kuwa na mwelekeo hasi kuhusu somo hili na ni somo ambalo hufunzwa katika mwaka wa nne na wanafunzi wana ufahamu wa kutosha kulihusu somo hili. Malengo haya yanaweza kuafikiwa ikiwa mwanafunzi anaelewa vyema uchanganuzi wa sentensi.

3.8.1.4. Upimaji wa umilisi wa kiisimu

Mwongozo wa kupima umilisi wa kiisimu katika lugha, hupima mazungumzo na maandishi. Kulingana na Nunnan (2003) vitengo hivi huwa vitano na kila kitengo hupewa alama. Vitengo hivi ni;

- i. Matamshi. ii. Ufasaha
- iii. Miundo ya sentensi iv. Kusudi v. Umakini.

Kila kitengo huwekewa alama 1-10. Ikiwa msemaji atatuzwa alama 9-10 inasemekana kuwa umilisi wake ni wa adhimu. Akituzwa alama 7-8 inasemekana kuwa umilisi wake ni mzuru sana. Ikiwa atatuzwa alama 5-6 inasemekana kuwa umilisi wake ni mzuri. Akituzwa alama 3-4 katika kila kitengo inasemekana kuwa umilisi wake ni wa kiwango cha wastani na akituzwa alama 1-2 inasemekana kuwa umilisi wake ni hafifu. Utafiti wa Al Juboury (1999) alioufanya nchini Iraq ulitumia vitengo hivi.

Katika kupima umilisi wa kiisimu katika maandishi vigezo vifuatavyo hutumiwa. Kulingana na Nunnan (2003) vigezo hivi ni;

- i. Sarufi
- ii. Miundo ya sentensi iii. Hijai
- iv. Mshikamano v. Uhusiano.

Kila kigezo pia huwekewa alama 1-10. Ikiwa msemaji atatuzwa alama 9-10 inasemekana kuwa umilisi wake ni wa adhimu. Akituzwa alama 7-8 inasemekana kuwa umilisi wake ni

mzuru sana. Ikiwa atatuzwa alama 5-6 inasemekana kuwa umilisi wake ni mzuri. Akituzwa alama 3-4 katika kila kitengo inasemekana kuwa umilisi wake ni wa kiwango cha wastani na akituzwa alama 1-2 inasemekana kuwa umilisi wake ni hafifu.

Nunaan (kashatajwa) anasema kuwa vigezo vingine ambavyo hutumika katika kupima umilisi wa kiisimu ni pamoja na kuchunguza kusitasita katika mazungumzo, kurudiarudia maneno, kunyamaza, kuchanganya na kubadili msimbo na kucheka. Hata hivyo vigezo hivi vinatumika katika kitengo cha umilisi katika usomaji. Mtafiti anatuza alama 10-100 katika kigezo cha jarabati. Wale wanaopata alama 70-100 wanakuwa na umilisi wa viwango vya juu. Na wale wanaopata alama za 10-30 wanakisiwa kuwa na viwango hafifu katika umilisi.

3.8.2. Mbinu za Kuchanganua Data

Data katika utafiti huchanganuliwa kwa kutumia mikabala ya aina mbili. Mkabala wa kiidadi na mkabala wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Walliman (2011), mkabala wa kiidadi ni mbinu ya kuchanganua data ambayo hutumia namba kurekodi taarifa na huchanganuliwa kwa kutumia mbinu za kitakwimu. Naye Enon (1998) anaeleza kuwa mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti anaeleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo. Aidha, Kress (2008) anafafanua mkabala huu kuwa unaelezea vipi na kwa nini matukio yanatokea njinsi yalivyo.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kila mkabala, mtafiti ameamua kuchanganua data za utafiti huu kwa mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi. Mtafiti anatumia mkabala wa kiidadi kwa lengo la kupata takwimu sahihi za data. Vilevile, mkabala usio wa kiidadi unatumika kwa vile kuna data zinazotokana na majibu ya kimaelezo yanayogusa maoni ya mhojiwa. Kwa hivyo, data

hizo zinahitaji kutolewa maelezo. Data zinazopatikana zinawasilishwa kwa kutumia maelezo na jedwali kwa njia ya asilimia.

3.9. Maadili katika utafiti.

Ingawa utafiti ni muhimu katika taaluma mbalimbali, elimu hii haiwezi kupatikana bila kutilia maanani utu na hekima ya binadamu kama asemavyo Oso na Onen (2005). Mtafiti ni lazima aeleze jinsi anavyolishughulikia suala la maadili katika utafiti wake. Baadhi ya maadili ambayo mtafiti lazima achunguze ni: Kueleza wasailiwa kuhusu utafiti. Kuweka maoni yao siri, kutowajulisha kwa uma wasailiwa kati ya mengine mengi. Mtafiti amewauliza wasailiwa wote ruhusa ya kuwasaili, na kuwapa nafasi ya kujaza fomu ya kukubali kushiriki utafiti huu (kiambatisho 5a uk 112). Wale wanaojaza hojaji pia ameongea nao na kuwajulisha sababu ya kufanya utafiti huu. Wote wameelezwa kuwa maoni yao yatatumiwa kwa ajili ya utafiti na sio kuwadhihaki au kuwakejeli wasailiwa hao.

3.10. Hitimisho

Sura hii imewasilisha hatua mbalimbali zinazofuatwa katika utafiti huu, kila awamu imeelezwa kwa undani jinsi inavyotumiwa kufanikisha utafiti. Sura hii pia imefafanua namna utafiti unavyofanyika. Sehemu ya kwanza imeeleza muundo wa utafiti. Sehemu ya pili imeeleza eneo la utafiti. Sehemu ya tatu imefafanua kundi lengwa. Sehemu nne ya imeeleza mchakato wa usampulishaji. Sehemu ya tano imeeleza mbinu za kukusanyia na kuchanganua data. Sehemu ya sita inaeleza maadili katika utafiti. Sehemu ya saba imeeleza utafiti majaribio, sehemu ya nane imeeleza udhabiti wa vifaa vya utafiti na sehemu ya tisa imehitimisha sura. Sura inayofuata inawasilisha na kuchanganua data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

4.1. Utangulizi

Lengo la sura hii ni kuwasilisha na kuchambua data zinazokusanywa juu ya “Umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno.” Data zote zote ambazo zimekusanywa kwa njia ya hojaji, mahojiano au usaili na jarabati zimewasilishwa na kuchambuliwa kwa kina katika sura hii. Data za msingi zimetumika katika utafiti huu. Kwa mujibu wa Vertanian (2011), data za msingi ni data ambazo zinakusanywa na mtafiti kwa kutumia mbinu kama hojaji, mahojiano, vikundi lengwa, uchunguzi au mbinu nyingine. Data hizi zinatoka moja kwa moja kwa watafitiwa. Aidha, utafiti huu unatumia data za aina mbili. Aina ya kwanza ni data zinazotokana na mawazo na maoni ya watafitiwa kuhusu umilisi wa kiisimu kwa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno na aina ya pili ya data, ni kutoka katika jarabati ya mwaka wa nne. Data hizi ambazo zimepatikana kutoka kwa watafitiwa zimegawanywa na kuchambuliwa kwa kufuata aina tatu za sampuli. Wanafunzi wa mwaka wa kwanza, wanafunzi wa mwaka wa nne, wahadhiri na jarabati kutoka mwaka wa nne.

Mgawanyo huu unafanyika ili kutoa fursa kwa mtafiti kuchanganua data kwa urahisi na kufanya ulinganishi wa matokeo ya watafitiwa. Sura inaanza kwa kuwasilisha data na kumaliza na uchambuzi wa data. Uwasilishaji na uchambuzi huo wa data unafanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti na maswali yanayoambatana na malengo hayo. Uchanganuzi huu unashirikisha mihimili ya nadharia ya Lehmann ambayo ni vigezo vya jarabati vya kupima umilisi wa kiisimu katika maandishi na mazungumzo. Vilevile ubinafsi wa mtu katika kuelewa umilisi wa kiisimu katika lugha husika kama mhimili wa pili. Hivyo mwanafunzi anapoingia chuoni katika mwaka wa kwanza kupitia mhimili huu wa ukuaji

akifanya mazoezi anapofika mwaka wa nne huwa umilisi wake unaimarika. Hili linatokea kwa sababu ya mwelekeo wake ukiwa chanya au hasi kulingana na Gardner.

4.2. Kuchanganua viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa watafitiwa wa mwaka wa kwanza na mwaka wa nne katika Chuo Kikuu cha Maseno nchini Kenya

Lengo la kwanza la utafiti huu ni kubainisha viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa watafitiwa wa Chuo Kikuu cha Maseno. Kwa kutumia mbinu ya hojaji, usaili na jarabati, mtafiti anakusanya taarifa kutoka kwa watafitiwa ili kupata majibu ya maswali yanayojibu lengo la kwanza la utafiti huu. Lengo hili linawakilishwa na maswali matatu yenye majibu yafuatayo:

4.2.1. Viwango vya umilisi wa kiisimu kwa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno.

Majibu haya yamepatikana kwa kutumia mbinu ya hojaji, saili ya wahadhiri na jarabati ya wanafunzi wa mwaka wa nne. Watafitiwa wote ambao wameshiriki katika utafiti huu wamepata fursa ya kujaza hojaji na jumla walikuwa 40. Vilevile wahadhiri watatu wameshiriki katika kutoa majibu ya usaili. Wahadhiri hawa wamepewa majina ya msimbo kama A, B na C. Mhadhiri A, anasema kuwa;

Naweza kusema kuwa kuna shida, asilimia kubwa ya wanafunzi wana umilisi wa kiwango cha chini wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili haswa katika mwaka wa kwanza (usaili)

Mhadhiri B, naye anasema kuwa;

Mimi binafsi naweza kusema kuwa wanafunzi wana umilisi wa chini wakiingia chuoni lakini baadaye umilisi huu huimarika wanapoendelea katika mwaka wa tatu na nne. Haya ni maoni yangu (saili).

Mhadhiri C, alisema kuwa;

Unapowapa kazi ya isimu ya kutafitia unapata kuona upungufu wao katika kuandika mijarabu hii. Wao huwa na makosa ya kisarufi, msamiati mpangilio wa sentensi na hijai (saili).

Mhadhiri A, anaongezea kusema kuwa;

Unapowapa kazi ya ziada au kuandika pendekezo la utafiti, unapata kuona kuwa uandishi wao ni wakutilia shaka. Wahadhiri pia walieleza sehemu ambazo zilileta shida kama vile: Kutofautisha tenzi, nahau, istilahi ngumu na mpangilio wa sentensi (sintaksia) katika maandishi ya kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

Sababu ambazo zinatolewa na mhadhiri B kuhusu umilisi wa kisiisimu wa kiwango cha chini cha wanafunzi ni kuwa:

- i. Kiswahili kama lugha haijapewa nafasi ya matumizi katika chuo, kwa sababu shughuli nyingi hufanywa katika lugha ya Kiingereza.
- ii. Wanafunzi kutumia Kiingereza na Sheng' katika muda wao mwingi
- iii. Wahadhiri wa isimu wanahamisha misimbo katika mihadhara kati ya Kiswahili na Kiingereza na hata pengine lugha zao za kwanza ili kufidia upungufu wa istilahi za kiisimu.

Kutokana na maelezo haya ya wahadhiri, viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi hawa katika chuo ni wa hali ya chini. Wahadhiri pia wanaeleza kuwa viwango vya wanafunzi ni vya chini katika mwaka wa kwanza lakini wanapofika mwaka wa nne viwango vyao vya umilisi vinaimarika. Mhadhiri C, anaeleza kuwa njia ambazo wao hutumia kupima kiwango cha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kuwa ni kupitia kwa mijarabu. Vilevile mhadhiri B, anakubali kuwa Kiswahili hakijapewa nafasi kama lugha ya kutumia chuoni kwani shughuli nyingi rasmi chuoni hutumia Kiingereza na hali hii inafanya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kushuka. Kiswahili kinatumika tu katika mihadhara ya Kiswahili na watafitiwa wanapotoka nje ni wachache tu ambao wanatumia Kiswahili, wengi wao wanatumia Kiingereza na Sheng' na hii inaathiri umilisi wao wa

kiisimu katika lugha ya Kiswahili chuoni. Wanafunzi wengi katika Chuo Kikuu cha Maseno wana mielekeo chanya kuhusu lugha za kwanza, hii inachangia pakubwa katika kudorora kwa umilisi wa kiisimu katika Kiswahili. Kulingana na Nadharia ya Gardner mhimili wa kwanza ambao mtu huwa na mwelekeo na hamu ya kujifunza lugha ili aweze kuitumia katika mawasiliano. Mhimili huu unaafiki utafiti utafiti huu kwa sababu mwanafunzi aliye na mwelekeo chanya atakuwa na hamu ya kujua lugha hiyo.

Hoja ya pili ambapo wanafunzi wengi wanatumia Kiingereza na Sheng' muda wao mwingi, inabainika kuwa wanafunzi wanafunzwa masomo mengi na yote haya isipokuwa lugha ya Kiswahili na kifaransa wanafunzwa kwa Kiingereza sana na wanapotoka katika mihadhara wao wanatumia Sheng' hali hii inafanya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kuwa hafifu na hivyo kudorora. Wahadhiri kuhamisha misimbo katika kipengee cha tatu, ni moja ya matatizo ambayo wahadhiri wanakubaliana nayo, wote watatu wanasema kuwa kwa sababu ya ukosefu wa istilahi za kiisimu katika lugha ya Kiswahili wao wanalazimika kutumia lugha zote kuelezea hoja, yaani Kiingereza na Kiswahili. Hali hii inaathiri kwa kiwango kubwa umilisi wa kiisimu wa wanafunzi katika lugha ya Kiswahili na kufanya mielekeo yao kuwa hasi.

4.2.2. Alama za KCSE katika Kiswahili.

Matokeo mengine yanatokana na saili ya mwaka wa kwanza na hojaji ya mwaka wa nne. Matokeo haya yanawasilishwa katika jedwali nambari 2.

Jedwali 2 Alama za KCSE.

Gredi	mwaka wa1	Asilimia	mwaka wa 4	Asilimia
A	10	10	5	12.5
A-	05	12.5	3	7.5
B+	06	15	6	15
B	06	15	7	17.5
B-	08	20	7	17.5
C+	11	27.5	12	30
Idadi	40	100	40	100

Chanzo; Saili ya mwaka wa kwanza na hojaji ya mwaka wa nne

Kutokana na matokeo haya, watafitiwa 4 wa mwaka kwanza ambayo ni asilimia 10 walipata alama ya A katika mtihani wa Kitaifa wa KCSE katika somo la Kiswahili. Watafitiwa 5 ambayo ni asilimia 12.5 walipata alama ya A-, watafitiwa 6 ambayo ni asilimia 15 walipata alama ya B+ na B, watafitiwa 8 ambayo ni asilimia 20 walipata alama ya B-. Nao watafitiwa 11 ambayo ni asilimia 27.5 walipata alama ya c+. Ukilinganisha na mwaka wa nne, watafitiwa 5 ambayo ni asilimia 12.5 walipata alama ya A, watafitiwa 3 ambayo ni asilimia 7.5 walipata alama ya A-, watafitiwa 6 ambayo ni asilimia 15 walipata alama ya B+, watafitiwa 7 ambayo ni asilimia 17.5 walipata alama ya B na B-. Nao watafitiwa 12 ambayo ni asilimia 30 walipata alama ya c+. Kutokana na matokeo haya utafiti umeelewa alama walizopata wanafunzi katika mtihani wa lugha ya Kiswahili na kuwawezesha kujiunga na chuo kikuu. Alama zao hizi zinatoa maelezo kuhusu umilisi wao wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili. Kujua huku kunamwezesha mtafiti kuelewa ikiwa umilisi unaimarika au la wanapozidi kusoma. Kwa kutumia mhimili wa Lehmann wa tatu unaosema kuwa umilisi wa mtu katika lugha hupimwa kupitia mtihani maalum. Hivyo mtihani wa Kis-

wahili wa kidato cha nne (KCSE) unaweza kueleza viwango vya umilisi wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojiunga na Chuo Kikuu kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo juu.

4.2.3. Matokeo ya jarabati ya mwaka wa nne

Matokeo ya jarabati ya mwaka wa nne yamewasilishwa katika jedwali lifuatalo kati ya wavulana na wasichana. Baada ya jarabati hizo kusahihishwa na alama kutuzwa.

Jedwali la 3. Muhtasari wa matokeo wavulana wasichana

Alama	marafukizi	Asilimia %	marafukizi	Asilimia
0- 29	3	16.6	2	09
30-34	2	11.1	2	09
35-39	1	5.5	3	13.5
40-44	1	5.5	2	09
45-49	1	5.5	1	4.5
50-54	0	00	5	22.5
55-59	2	11.1	0	00
60-64	4	22.2	3	13.6
65-69	3	16.5	3	13.6
70-74	1	5.5	1	4.5
75-100	0	00	0	00
Idadi	18	100	22	100

Chanzo; Matokeo ya jarabati ya mwaka wa nne.

Kutokana na matokeo haya wavulana 3 ambayo ni asilimia 16.6 walipata alama zisizo zidi 29 ikilinganishwa na wasichana 2 ambayo ni asilimia 9, watafitiwa wavulana 2 ambayo ni

asilimia 11.1 walipata alama zisizozidi 34 ikilinganishwa na wasichana 2 ambayo ni asilimia 9. Mtafitiwa mvulana 1 ambayo ni asilimia 5.5 alipata alama zisizozidi 49 ikilinganishwa na wanafunzi wasichana 2 ambayo ni asilimia 9 waliopata alama sawa na mvulana. Wavulana 9 ambayo ni asilimia 39 walipata alama zisizozidi 69 ikilinganishwa na wasichana 6 ambayo ni asilimia 27.2 waliopata alama zisizozidi 69. Hakuna mwanafunzi yeyote aliyepata zaidi ya alama 75.

Matokeo zaidi yanatokana na jarabati ya mwaka wa nne kama yafuatayo; Katika jarabati (kiambatisho 11) mtafitiwa anashindwa kuchanganua sentensi “Nyumba ilijengwa na mwashi aliyehitimu” akitumia mstari. Vilevile anashindwa kabisa kuchanganua sentensi nambari mbili “Mtoto aliupiga mpira uliokuwa mweusi”. Kushindwa kwake huku kuchanganua sentensi kunaonesha umilisi wa kiwango cha chini cha kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa sababu ukielewa uchanganuzi huu umilisi wako utakuwa wa kiwango cha juu.

Mfano wa sentensi sahihi;

Sentensi: Nyumba ilijengwa na mwashi aliyehitimu.

$S \rightarrow S1+U+S2$

$S1 \rightarrow KN+KT+U+S2 \rightarrow KN+\bar{S}$

$S1 \rightarrow KN (N) \rightarrow nyumba+ KT (T) ilijengwa + U (na) + S2 \rightarrow KN (N) Mwashi+ KT (\bar{S}) aliyehitimu.$

Mfano wa sentensi ya pili.

Mtoto aliupiga mpira uliokuwa mweusi.

$S \rightarrow KN+KT$

$KN \rightarrow N+T+N$

$N \rightarrow Mtoto$

$T \rightarrow aliupiga$

$N \rightarrow \text{mpira}$

$KT \rightarrow \bar{S}$

$\bar{S} \rightarrow \text{uliokuwa mweusi}$

Kutokana na matokeo haya, uchanganuzi wa sentensi kutumia njia ya mstari unachukua mikondo miwili. Mkondo wa kwanza ni wa mstari mmoja katika sentensi hiyo nao mkondo wa pili ni mistari mingi kama inavyooneshwa katika sentensi ya pili. Katika (kiambatisho nambari 11) mtafitiwa anashindwa kueleza sehemu ya KT na vipengee vyake vya kishazi huru na kishazi tegemezi. Sehemu ya kishazi tegemezi inaandikwa na \bar{S} yenye Kistari juu yake ambapo mtafitiwa hakuweza kueleza kwa njia ifaayo. Hali hii inaonesha kuwa umilisi wa mtafitiwa huyu ni wa kiwango cha chini kwa sababu haweza kuchanganua sehemu hizi kama inavyotakikana katika sentensi ya pili. Mfano mwingine ni ule wa kuchanganua sentensi kutumia majedwali. Katika (kiambatisho cha 11), mtafitiwa ameshindwa kuchanganua sentensi kwa njia ifaayo. Sentensi C i, ii, iii, zimechanganuliwa vibaya na mtafitiwa. Hakuweza kueleza vipashio au sehemu muhimu za sentensi hiyo. Katika sentensi ya C i “*Yeye ni mwerevu ingawa mimi simpendi mtoto huyu*”. Mtafitiwa anaonesha kuwa sentensi ina kishazi tegemezi ambayo inaoneshwa na \bar{S} yenye kistari juu. Sentensi hii haina kishazi tegemezi. Ingawa mtafitiwa anaonesha sehemu ya sentensi ya kwanza na ya pili, sehemu hizi zingine zimemshinda.

Mfano mwingine ni katika sentensi ya C ii, ambayo ni “*mwizi aliyetorokea msituni jana usiku amepatikana leo alfajiri*”. Uchanganuzi wa sentensi hii unaonesha kuwa mtafitiwa aligawa sentensi katika sehemu mbili, sentensi ya kwanza na sentensi ya pili, ambayo imeonyeshwa na S1 na S2. Lakini kwa kawaida sentensi aina hii haigawanywi kwa S1 na S2 kwa sababu haina kiunganishi. Hivyo ingewekwa sehemu ya KN na KT. Vilevile mtafitiwa

anaonesha kuwa sentensi ina sehemu kapa ambayo inoneshwa kwa alama (θ) ilhali sivyo. Uchanganuzi huu unaonesha umilisi wake duni katika isimu kwa lugha ya Kiswahili.

Mfano mwingine ni katika sentensi ya C iii, “*Mwanafunzi ambaye alimpiga mama amepele-kwa mahakamani*”. Katika sentensi hii mtafitiwa hahitaji sehemu ya S1 na S2. Kile anachohitaji ni sehemu ya kundi nomino na kundi tenzi (KN na KT). Katika sehemu ya kundi nomino (KT), angeweka nomono (N) na kishazi tegemezi (\bar{S}). Nomino hapa ingekuwa mwanafunzi na kishazi tegemezi ingekuwa ambaye alimpiga mama.

Mfano mwingine ni sentensi ya B3 katika kiambatisho (11) ambayo ni “*Sisi sote tuliohitimu juzi tumetuzwa zawadi*”. Sehemu hii inawataka watafitiwa kuchanganua sentensi kwa njia ya matawi. Mtafitiwa katika mfano huu anatumia Sentensi ya kwanza (S1) na sentensi ya pili (S2) badala ya KN na KT. Vilevile anaweka sehemu ya kapa ambayo haikuhitajika.

Mfano mwingine ni sentensi B1, 2, 3 katika kiambatisho (10), mtafitiwa anachora matawi na kuchanganua sentensi na kisha akakata mstari kwa sentensi zote. Ingawa sentensi hizo zinakuwa na makosa hapa na pale kukata mstari kunaonyesha kuwa hana imani na kile anachokifanya. Matokeo zaidi yanapatikana kutoka zile sentensi za wanafunzi ambao wanapata alama za juu na zinaonesha makosa machache mno ikilinganishwa na zile za alama ya chini. Katika kiambatisho 7, watafitiwa wanachanganua sentensi “*Nyumba ilijengwa na mwashi aliyehitimu*” vyema kutumia mistari, matawi na majedwali. Kuchanganua huku kunaonesha kuwa umilisi wa watafitiwa ulikuwa wa kiwango cha juu.

Kwa ujumla matokeo ambayo yamepatikana kutoka swali la kwanza, pili na tatu yanaonesha kuwa umilisi wa kiisimu wa watafitiwa katika lugha ya Kiswahili ni wa kiwango cha chini

kwa wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza na mwaka wa nne. Kwa mujibu wa nadharia ya umilisi wa kiisimu wa Lehmann (2006) na motisha ya Gardner (1985) matokeo yanaonesha kuwa viwango vya umilisi hupatikana katika mazoezi na hukua maishani mwa mtu. Mielekeo yake pia inachangia ukuaji huu. Umilisi wa watafitiwa wa mwaka wa kwanza unaonekana kuwa wa kiwango cha chini wanapoingia katika chuo kikuu, lakini umilisi huu unaonekana kuimarika haswa kwa watafitiwa wa mwaka wa nne kwa sababu wamekaa chuoni kwa muda mrefu na kujifunza mambo mengi kuhusu isimu. Watafitiwa wenye mielekeo chanya wanafanya vizuri katika jarabati ya mwaka wa nne kuliko wale walio na mielekeo hasi.

Matokeo haya yanafanana na Babusa (2010) alipochunguza umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa shule za upili katika miji ya Nairobi na Mombasa. Umilisi wa watafitiwa unaathiriwa na mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiswahili. Tofauti ilioko na utafiti huu ni kuwa, Babusa alichunguza wanafunzi wa shule za upili na utafiti huu ulichunguza wanafunzi wa vyuo vikuu. Vilevile utafiti wa Babusa ni wa isimujamii na huu wetu ni usimu tumikizi.

Kwa kuhitimisha hoja hii ya viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno, imebainika kuwa viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa watafitiwa huwa vya kiwango cha chini wanapokuwa katika mwaka wa kwanza. Lakini viwango hivi vinaimarika kwa watafitiwa wa mwaka wa nne. Viwango hivi vinaonekana wakati wa uchanganuzi wa sentensi wanazopewa na hivyo majibu haya yanaweka bayana viwango vya umilisi wa kiisimu katika Chuo Kikuu cha Maseno. Uchanganuzi umetimiza lengo la kwanza la utafiti huu kuhusu viwango vya umilisi wa kiisimu. Uchanganuzi katika sura hii umetazama viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na mwaka wa nne. Imebainika kuwa vikwazo vya kiumri vinaathiri viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Ujuzi wa

umilisi katika lugha husika unaimarika kadri mwanafunzi anapojifunza umilisi katika lugha ndivyo anavyong'amua na kutumia isimu hii vilivyo. Mhimili wa kwanza wa Lehmann ambao unasema kuwa viwango vya umilisi huimarika kadri mtu anapojifunza lugha husika. Hivyo kutokana na viwango tofauti vya mwaka wa kwanza na mwaka wa nne, imebainika kuwa wale wanafunzi wa mwaka wa nne wameimarisha viwango vyao ikilinganishwa na wale mwaka wa kwanza. Viwango vya umilisi vya juu kwa wanafunzi wa mwaka wa nne vinaonesha kuwa mhimili huu unaafiki vyema utafiti huu kwa kubainisha viwango tofauti kulingana na wanafunzi tofauti.

4.3. Vipengee vinavyoonyesha mabadiliko katika umilisi wa kiisimu

Lengo la pili la utafiti huu ni kubainisha vipengee vinavyoonyesha badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Lengo hili linafikiwa kwa kuuliza maswali mawili katika saili ya wahadhiri, saili ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza na hojaji ya wanafunzi wa mwaka wa nne. (Taz kiambatisho 1,2 na 3 ukurasa 107-111 swali nambari 4 na 5). Kulingana na nadharia ya umilisi ya Lehmann, mhimili wa tatu kuhusu vipengee ambavyo vinaonesha badiliko la umilisi katika maandishi na mazungumzo unatumiwa kuchanganua matokeo haya.

4.3.1. Majibu ya watafitiwa

Watafitiwa wanaeleza vipengee ambavyo vinaonesha badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Vipengee hivi vinapatikana katika utendaji ambapo mtafitiwa anapoandika na kuzungumza mabadiliko haya huonekana. Saili ya watafitiwa wa mwaka wa kwanza na hojaji ya mwaka wa nne inatoa hoja zifuatazo kama vipengee vinavyoonyesha mabadiliko katika umilisi wa kiisimu.

Katika mazungumzo vigezo hivi ni:

i. Miundo mizuri ya sentensi ii. Kuongea kwa ufasaha

iii. Kutumia sarufi nzuri iv. Kuwa na muwala v. Kutositasita katika mazungumzo

Katika maandishi vigezo hivi ni:

i. Sarufi nzuri ii. Uakifishaji mzuri wa makala

iii. Hijai nzuri iv. Miundo ya sentensi v. Nje

Kutokana na matokeo haya vigezo vinavyoonesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu vimeorodheshwa. Uundaji mzuri wa sentensi katika mazungumzo, kuongea kwa ufasaha, kutumia sarufi vyema, kuwa na muwala katika mazungumzo yako na kutositasita katika mazungumzo ni vigezo vinavyoonyesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Vilevile Katika maandishi, mtafitiwa ambaye angeandika sentensi vizuri, atumie alama za uakifishaji vizuri, awe na hijai nzuri na atumie njeo vizuri anaonesha kuwa umilisi wake wa kiisimu unaimarika.

Mfano mwingine wa matokeo ya mabadiliko ya umilisi yanatokana na wahadhiri ambao wanasema yafuatayo: Mhadhiri A anasema kuwa, *ukimpa mwanafunzi jarabati na kisha uisahihishe unaweza kujua kutokana na alama anazopata umilisi wake wa kiisimu. Vilevile ukizungumza naye utapata kuelewa jinsi anavyounda sentensi na kupanga mawazo yake katika mazungumzo hayo na utajua kama umilisi wake ni wa kiwango cha wastani, chini au cha juu, pia anapowasilisha kazi yake ya utafiti mbele ya wenzake utafahamu umilisi wake kuhusu lugha ya Kiswahili. Atatumia miundo mizuri ya sentensi, ataongea kwa ufasaha, atatumia sarufi nzuri na ataonyesha muwala katika mazungumzo yake. (saili)*

Mhadhiri B anaeleza kuwa, vigezo vinavyoonesha badiliko la umilisi katika maandishi, matokeo ni: *Sarufi, njeo, msamiati, hijai na uakifishaji*. Mwanafunzi anapoitumia sarufi vizuri, njeo, msamiati, hijai na uakifishaji unaokubaliwa na wanajamii lugha husika huwa na kiwan-

go cha juu cha umilisi wa kiisimu. Naye mhadhiri C anaeleza kuwa, wakati mwanafunzi anaposoma makala, utaona kuwa *anasitasita, kurudiarudia maneno au sentensi, kuchekacheka na wakati mwingine anashindwa na kunyamaza*. Wahadhiri A, B na C wanaeleza vipengee ambavyo huonyesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika lugha. Mhadhiri A anaeleza kuwa wanafunzi wakiwa katika mwaka wa kwanza huonesha upungufu katika maandishi yao na vilevile katika mazungumzo yao. Mhadhiri B, anaeleza kuwa sarufi, njeo, msamiati, uakifishaji mzuri na miundo mizuri ya sentensi kama vigezo vinavyoonesha mabadiliko haya. Mhadhiri C anaeleza kuwa kusitasita, kurudiarudia katika maneno, kuchekacheka wakati wa kuulizwa maswali na kunyamaza ni vipengee vinavyoonesha mabadiliko katika umilisi wa kiisimu. Mwanafunzi ambaye huonesha haya atachukuliwa kuwa na umilisi wa kiwango cha chini. Lakini yule ambaye hataonesha upungufu huu atachukuliwa kuwa ana umilisi wa kiwango cha juu wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa nadharia ya Lehmann ya umilisi wa kiisimu, vipengee vinavyoonesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika utafiti huu ni vile vinavyotumiwa na watafitiwa wengine. Vipengee hivi vinabadilika mtu anavyozidi kukua na kusoma kulingana na mhimili wa lehmann wa pili.

Kwa ujumla, vipengee ambavyo vinaonesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika lugha huwa ni vingi. Aidha, Nunnan (2003) na Kamau (2015) wameorodhesha ufahamu, usahihi, ufasaha na umakini katika lugha kama baadhi ya vigezo ambavyo huonyesha kuimarika au kudorora kwa umilisi katika lugha husika. Chomba (2013) na Mwangi (2014) wanasema kuwa kusitasita, kurudiarudia maneno, matamshi mabovu katika mazungumzo ni baadhi ya vigezo vinavyoonesha mabadiliko ya kiisimu katika lugha. Utafiti wao unalingana na utafiti huu kwa kutoa matokeo sawa ya vigezo vinavyoonyesha badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

Wahadhiri A, B na C wanakubaliana na mawazo ya Mwangi na Chomba kuhusu vipengee vinavyoonesha badiliko la umilisi katika lugha. Mtu aliye na ufasaha katika mazungumzo, mwenye kufuata sheria za kisarufi katika maandishi au mazungumzo husemwa kuwa ana umilisi wa kiwango cha juu kuliko yule anayefanya kinyume na ilivyotajwa. Upimaji huu unalingana na ule wa Kitsao (2015) na Kamau (2015) ambao walitumia kupima umilisi wa kiisimu wa wanafunzi katika umilisi wa lugha ya Kikuyu. Matokeo ya Kamau (2015) yalionesha kuwa umilisi wa lugha ya Kikuyu kwa wanafunzi wa shule za upili huathiriwa na lugha ya Kiswahili, Kiingereza na sheng' katika Gatuzi la Nairobi, Kiambu na Muranga. Kitsao (2015) naye alifanya utafiti kuhusu uchanganuzi wa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi katika kata ya Ganze. Makosa haya yanahusisha hijai, njeo, msamiati, sarufi na mshikamano. Upimaji huu wa Kitsao na Kamau unalingana na huu wetu ila tu Kamau alifanya utafiti wake katika shule za upili katika gatuzi la Nairobi, Kiambu na Muranga. Kwa mujibu wa Nadharia ya Lehmann (2006) mhimili wa tatu kuhusu upimaji wa umilisi unasema kuwa, kuna vigezo maalum ambavyo hutumiwa kupima umilisi katika lugha yoyote ile, kigezo hiki kinasaidia utafiti kuelewa ukuaji wa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wana makosa mengi ya kisarufi na umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili ni wa viwango vya chini ukilinganisha na wanafunzi wa mwaka wa nne ambao wanafanya makosa madogo madogo katika kazi zao za uandishi na usemi.

Kwa kuhitimisha hoja hii ya vipengee vinavyoeleza mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili, matokeo yameonesha kuwa, vipengee hivi vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili vinagawanywa katika sehemu mbili ambayo ni: Kuzungumza na kuandika. Katika maandishi, vipengee ambavyo huonesha mabadiliko hupatikana katika njeo, msamiati, hijai, sarufi na uakifishaji. Vilevile katika mazungumzo, vipengee ambavyo vinaonesha

mabadiliko vinapatikana katika miundo mizuri ya sentensi, sarufi nzuri, kuwa na muwala, kuongea kwa ufasaha na kutositasita katika mazungumzo. Mabadiliko haya yanaonekana kwa wanafunzi wa mwaka wa nne na kuonesha kuwa umilisi wao wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili umeimarika. Kutokana na matokeo haya imebainika kuwa kigezo cha kusikiliza chaweza pia kutumiwa kupima umilisi wa kiisimu katika lugha ingawa katika utafiti huu hakikushughulikiwa.

4.4. Athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili

Lengo la tatu la utafiti huu ni kubainisha maoni ya watafitiwa kuhusu athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa kutumia mbinu ya hojaji na saili, mtafiti amekusanya mawazo mbalimbali ya watafitiwa kuhusu athari za lugha nyingine kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Majibu yanapatikana kutoka swali nambari 6 na 7 (Taz kiambatisho 1, 2 na 3 uk 107-111). Sheng' ilichunguzwa kwa sababu ni msimbo unaotumiwa sana na watafitiwa katika Chuo Kikuu cha Maseno.

4.4.1. Matokeo ya watafitiwa

Kutokana na majibu yanayotolewa na watafitiwa kutoka saili na hojaji ya watafitiwa baada ya uchambuzi wa kina, imebainika kuwa matumizi ya sheng' inaleta athari hasi kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Athari zote ambazo zimetolewa na watafitiwa ni za kiisimu na zimeorodheshwa kama ifuatavyo:

4.4.2. Athari za Kiisimu

Athari za kiisimu ni athari zote zinazobadilisha vipengele vya lugha na kuvifanya viathirike; kwa mfano, vipengele vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisantiki na kimsamiati.

Jedwali 4. Athari za Kiisimu Zinazoletwa na sheng' katika Kiswahili

Sampuli ya watafitiwa	Athari za kiisimu				
Hojaji	A	B	C	D	E
Idadi	4	5	13	9	11
Asilimia	10	12.5	32.5	22.5	27.5
40	4	5	13	9	11

Data kutoka uwandani 2012.

Kifasili

- A----- Athari za kifonolojia
- B----- Athari za Kimofolojia
- C----- Athari za Kisintaksia
- D----- Athari za Kisemantiki
- E----- Athari za kimsamiati

4.4.2.1. Athari za Kifonolojia

Athari ya kwanza ambayo imeelezwa na watafitiwa ni ya kifonolojia. Jedwali nambari 4 linaonesha kuwa athari hii ilichaguliwa mara 4 ambayo ni asilimia 10 na watafitiwa. Watafitiwa 5 ambayo ni asilimia 12.5 walichagua athari za kimofolojia. Watafitiwa 13 ambayo ni asilimia 32.5 walichagua athari za Kisintaksia. Watafitiwa 9 ambayo ni asilimia 22.5 walichagua athari za kisemantik na watafitiwa 11 ambayo ni asilimia 27.5 walichagua athari za kimsamiati.

Athari za kifonolojia ni athari zote ambazo zinaathiri matamshi au sauti (fonimu) za lugha mahususi. Katika utafiti huu, watafitiwa wanaeleza kuwa athari kubwa ya kifonolojia ina-

yoletwa na mtagusano wa lugha ya Kiswahili na sheng'. Hali hii hubadilisha baadhi ya herufi na sauti za Kiswahili. Kubadilisha sauti za Kiswahili ni athari kubwa katika lugha kwani ndizo zinazotofautisha maana. Pia, sauti huunda silabi na silabi ndizo zinazounda maneno ya lugha mahususi. Katika utafiti huu imegundulika kuwa baadhi ya herufi za Kiingereza na lugha za kwanza zinatumiwa kwa ajili ya kuwakilisha herufi na silabi za Kiswahili.

4.4.2.2. Athari za Kimofolojia

Watafitiwa 5 ambayo ni asilimia 12.5 walichagua hii hoja kama inayoathiri umilisi wa kiismu katika Kiswahili kwa watafitiwa wa Chuo Kikuu cha Maseno. Athari za kimofolojia ni athari zote ambazo zinaharibu maumbo ya maneno katika utafiti huu. Watafitiwa wanaeleza kuwa matumizi ya sheng' yanasababisha kuharibika kwa mofolojia (maumbo) ya lugha ya Kiswahili. Yaani Kuundwa kwa viambishi na maneno yasiyokubalika katika Kiswahili kutokana na kutofuata utaratibu sahihi wa kuunda maneno kwa baadhi ya mbinu. Athari za kimofolojia ni mbaya sana katika lugha kwa sababu tawi hili ndilo linalohusika na uundaji wa maneno. Hivyo, kama litaathirika maneno yatakayoundwa hayatakubalika katika lugha. Licha ya kuwa uundaji wa maneno katika sheng' unatumia mbinu mbalimbali kama vile *finyazo*, *kutohoa na unyambu*, maneno yanayoundwa kwa njia hizo aghalabu si sahihi na hayakubaliki katika umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Matokeo mengine yanayotokana na saili ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza ni: *Mmekamu kutucheki*, *doo*, *beste*, *buda*, *fathee na mbuyu*.

Saili inaonesha uundaji wa maneno yasiyo ya Kiswahili. Wakati mwingine maneno ya Kiswahili yanaambishwa katika maneno ya Kiingereza na kupewa matamshi ya Kiswahili. Katika maneno haya, "mmekamu kutucheki", *Kamu* ni neno (come) la Kiingereza lenye maana ya Kuja. Katika neno *cheki*, ni kuangalia au hundi katika lugha ya Kiingereza. Vilevile kuna

baadhi ya maneno kama, *doo*, *beste*, *buda* na *fathee* ambayo yanatumiwa na wanafunzi. Matumizi ya neno *doo* kumaanisha pesa, *beshte* kumaanisha rafiki, *buda* kumaanisha baba au tajiri na *fathee* kumaanisha baba linatokana na neno la Kiingereza *father*. Hata hivyo neno hili linafupishwa kwa kudondosha silabi ya mwisho {r} na kuongeza {e}. Neno hili linapewa matamshi ya Kiswahili {fathe}.

4.4.2.3. Athari za Kisintaksia.

Athari za kisintaksia ni athari zote ambazo zinaharibu muundo wa lugha (mpangilio wa maneno). Watafitiwa wanaeleza kuwa sheng' inaathiri Kiswahili kwa sababu inaharibu sintaksia ya lugha. Yaani, kuharibu muundo wa lugha kutokana na kuchanganya misimbo, kutofuata upatanisho wa kisarufi na kutumia mpangilio wa maneno usio sahihi. Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2009), sintaksia ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi na mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake. Watafitiwa wanaeleza kuwa mtindo huu haufuati kanuni za matumizi ya lugha. Hali hii inaathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, baadhi ya sentensi zinachanganya misimbo (Kiingereza na Kiswahili). Kwa mfano,

S “*Wasee wakichota tutado zile maswali*”

T. Watu wakitoe pesa watafanya yale maswali ya jarabati.

Sentensi hii imechanganya misimbo kwa sababu mwanzo inatumia Kiswahili lakini kuna neno la Kiingereza *do*. Neno *wasee* linamaanisha watu, *chota* katika Kiswahili sanifu linamaanisha kuchukua kitu kwa kikombe kama vile chai au maji. Lakini katika sentensi hii neno hili linatumiwa kumaanisha kutoa pesa au kuwapa pesa ili wafanye ule mtihani wa jarabati. Vilevile neno *zile* linatumiwa vibaya kulingana na ngeli ya swali ambayo ni li/ya lakini wanaipa ngeli ya i/zi. Hivyo, athari inayopatikana kutokana na kuchanganya misimbo ni kuharibu sarufi ya lugha na kupunguza dhana ya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

li. Pia kutumia ngeli vibaya kunaathiri umilisi katika lugha husika. Mifano ifuatayo: Mtatupa *doo* tukijibu maswali haya, *doo* yangu imesanywa, *doo zitatusot vipoa* na *tutaandika mdogomdogo*, sentensi hizi zinachanganya lugha mbili.

Baadhi ya sentensi zinachanganya misimbo (Kiingereza na Kiswahili). Mfano mzuri ni sentensi, *Doo zitatusort vipoa*. Sentensi hii ina maneno ya Kiingereza na Kiswahili. Neno *sort* ni la Kiingereza linalomaanisha kupanga, kuainisha au gawanya. Neno (*zitu*), sio neno lenye maana, kwa sababu ni viambishi tu. (*Zi*) ni kiambishi awali, (*ta*) ni kiambishi wakati ujao na (*tu*) ni kitendewa. Katika sentensi ya pili, mtatupa *doo* tukijibu maswali haya. Sentensi hii inapachikwa neno lisilo la Kiswahili. Neno *doo* linatokana na *dough* la Kiingereza lenye maana ya unga uliotiwa maji tayari kuokwa mikate. Katika sentensi hii neno hili limetumiwa kumaanisha pesa, ingawa halina uhusiano wowote na pesa katika Kiswahili. Watafitiwa walihitaji pesa baada ya kumaliza kujibu maswali katika saili au hojaji, lakini maana inayojitokeza ni unga wa kuoka mikate ambayo sio kile walichokihitaji. Katika sentensi *tutaandika mdogomdogo*. Haifuati kanuni za undaji wa sentensi za Kiswahili. Kwa sababu *tutaandika* ni kitenzi na katika mpangilio wa sarufi ya Kiswahili, kitenzi hufuatwa na kielezi na wala sio kivumishi kama ilivyo katika sentensi ya sheng'. Neno dogo ni kivumishi yaani kinaelezea zaidi kuhusu nomino na sio kitenzi kama ilivyo katika sentensi. Katika sentensi ifuatayo, "Tunaishia *dar*o hatuwezi *manze*".

Sheng' _____ *dar*o

Neno *dar*o hapa linamaanisha darasa katika Kiswahili sanifu.

Sheng' _____ *manze*

Neno *manze* linamaanisha bwana katika Kiswahili sanifu.

Sheng' _____ *Tunaishia*

Neno *tunaishia* linamaanisha tunaenda katika sheng' lakini katika Kiswahili neno hili likichanganuliwa linakuwa; *tu* ni kiwakilishi nafsi ya kwanza wingi, *na* ni kiwakilishi wakati uliopo na neno *ishia* ni kitenzi kinachotokana na neno kuishi, kwa maana ya kukaa mahali. Hivyo katika mnyambuliko wa vitenzi katika hali ya kutendea neno *ishia* linapatikana kumaanisha mtendee mtu kitendo cha kuishi. Lakini katika sheng' neno hili lina maana tofauti kabisa. Neno hili linamaanisha kwenda. Hivyo sentensi, *Tunaishia daro hatuwezi manze*, ina maana kuwa "Tunaenda darasani hatuwezi bwana". Sentensi hii ni mfano wa kishazi tengemezi kwa sababu tunaenda darasani hatuwezi nini? Maana ya sentensi hii haijakamilika. Huu ndio mtindo wa sheng' ambao sentensi nyingi huwa hazikamiliki na maana haieleweki. Uchanganuzi wa sentensi hii kuwa; Tunaenda ni Kitenzi, *daro* ni kielezi cha mahali, hatuwezi ni kitenzi na bwana ni nomino. Ikiwa tutachanganua sentensi jinsi ilivyo katika sheng', sentensi itakuwa, *tunaishia* ni kitenzi, *daro* ni nomino, *hatuwezi* ni kitenzi na *manze* ni kielezi. Sentensi sanifu ya Kiswahili haifuati mtindo huu na ikiwa wanafunzi wanaiga mtindo huu katika maandishi ya Kiswahili basi waathiriwe na hivyo kufanya umilisi wao kuwa wa kiwango cha chini. Moja kati ya athari zinazotolewa na watafitiwa ni kupoteza sifa kuu za lugha. Sifa kuu za lugha ni kukua. Lugha inakua kwa kuongezeka kwa idadi ya msamiati. Kadiri lugha inavyoongezeka kimsamiati, ndivyo inavyozidi kukua.

4.4.2.4. Athari za kisemantiki

Athari za kisemantiki ni athari zote ambazo zinasababisha maana inayokusudiwa isifike kwa anayekusudiwa. Watafitiwa wanabainisha kuwa mtindo huu unaleta athari hasi kwa sababu unasababisha utata katika lugha. Pia hufanya ujumbe usieleweke kwa urahisi na hivyo hufanya baadhi ya wasomaji kushindwa kufahamu ujumbe huo. Msomaji huchukua muda mrefu kusimbua ujumbe unaokusudiwa kwa vile lugha yenyewe inakaa kimafulmo. Kwa mujibu wa TUKI (2010), utata katika lugha ni hali ya neno kuwa na maana zaidi ya moja.

Utata huu unasababishwa na maneno ya sheng'ambayo inatumiwa katika mazungumzo ya wanafunzi. Kwa mfano:

S: Huyo tiche hapendi udo tukihata lesa yake.

T: Huyo mwalimu hapendi mchezo tukikosa kushiriki somo lake.

T: Huyo mwalimu hapendi mchezo tukikosa kitambaa chake.

Neno *tiche* ni kutokana na neno la Kiingereza *teacher*, *udo* ni mchezo, *lesa* ni neno lilikopwa kutoka neno la Kiingereza *lesson*, *hata* ni neno la Kiswahili linalomaanisha kukosa. Katika mifano hii miwili, sentensi ya kwanza ina maana tofauti na ile ya pili. Sentensi ya kwanza ina maana kuwa wakikosa kwenda darasani mwalimu huwa hapendi mchezo kama huo. Nayo sentensi ya pili ina maana kuwa wakikosa kitambaa au lesa mwalimu hapendi mchezo huo. Maana inayojitokeza katika sentensi ya pili inakuwa tofauti na ile ya kwanza ya kwenda darasani, kwa sababu msamiati wake haukubaliki katika Kiswahili na hatuwezi kukuza lugha kwa kutumia msamiati usiokubalika katika lugha. Hii ni tofauti na mitindo mingine ya lugha kama misimu ambayo baada ya msamiati wake kukubalika katika jamii, husanifiwa na kuwa msamiati rasmi wa lugha. Msamiati wa mtindo huu katu hauwezi kufikia hatua hiyo ya kusanifiwa na kuingizwa katika lugha kwa vile muundo wa msamiati wake ni tofauti na wa Kiswahili kutokana na kuchanganya herufi na misimbo. Mfano mwingine ni kuwa, sentensi nyingi katika Kiswahili huundwa kwa kutumia konsonanti na irabu pamoja na kufuata mpangilio sahihi wa maneno lakini hizi zinazoundwa katika lugha hii ni mara chache sana kufuata utaratibu huu. Mara nyingi hudondosha irabu, hutumia herufi za Kiingereza lakini hutamkwa kwa Kiswahili, huandikwa kwa kuchanganya misimbo na bila ya kufuata tahajia sanifu ya Kiswahili. Hivyo, ujumbe unaoandikwa unakuwa ni mgumu kueleweka. Hivyo, huu ni upotoshaji wa maana. Tafsiri inayopatikana hapa ni kwamba ujumbe unaoandikwa katika maandishi haya unaashiria maana nyingine kabisa tofauti na unavyosomeka katika maandishi ya Kiswahili, licha ya kuwa unatumia maneno mengi ya Kiswahili. Kwa maana hiyo, maana

inayokusudiwa kwa walengwa inachelewa kufika kutokana na utata unaojitokeza kwa baadhi ya maneno yanavyoandikwa.

4.4.2.5. Athari za kimsamiati

Matokeo yameonesha kuwa kuna maneno mengi ambayo yanawekwa katika sheng' na yanaundwa bila kufuata sheria za kisarufi. Maneno kama *Kuchop* kwa maana ya kusoma, *anakam* kwa maana ya kuja, *doo* kwa maana ya pesa, *buda*, *fathee* kwa maana ya baba, *bashte* kwa maana ya rafiki, *mayouth* kwa maana ya vijana, *tiche* kwa maana ya mwalimu, *kuchop* kwa maana ya kusoma, *mnoma*, kwa maana ya mtu mbaya, *daro*, kwa maana ya darasa, *tukimada*, kwa maana ya kumaliza, *kumanga*, kwa maana ya kula, *wakichota*, kwa maana ya kutoa pesa, *tutado*, kwa maana ya tutafanya, *kubanjuka* kwa maana ya kucheza ni baadhi ya misamiati katika sheng'. Moja kati ya athari zinazotolewa na watafitiwa ni kupoteza sifa kuu ya lugha. Sifa kuu ya lugha ni kukua. Lugha inakua kwa kuongezeka idadi ya msamiati. Kadiri lugha inavyoongezeka msamiati, ndivyo inavyozidi kukua. Hivyo, watafitiwa wanaeleza kuwa mtindo huu unaathiri Kiswahili kwa sababu hauongezi msamiati wa lugha, haukubaliki kwa vile sio halisi na haufuati sarufi ya Kiswahili kwani huandikwa kinyume na ilivyo katika Kiswahili. Baadhi ya mifano ni kufupisha kwa vifupisho visivyo sanifu na baadhi ya wakati unachanganya misimbo. Hali hii inadumaza maendeleo ya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa sababu msamiati wake haukubaliki katika Kiswahili na hauwezi kukuza lugha kwa kutumia msamiati usiokubalika katika lugha. Hii ni tofauti na mitindo mingine ya lugha kama, misimu ambayo baada ya msamiati wake kukubalika katika jamii, husanifiwa na kuwa msamiati rasmi wa lugha. Msamiati wa mtindo huu katu hauwezi kufikia hatua hiyo ya kusanifiwa na kuingizwa katika lugha kwa vile muundo wa msamiati wake ni tofauti na wa Kiswahili kutokana na kuchanganya herufi, na misimbo. Hauwezi kufaa katika Kiswahili na kwa maana hiyo Kiswahili hakipati kukua kwa mtindo huu.

Kulingana na utafiti wa Mutungu (2001), Rapando (2005), Mbula (2010) na Moraa (2012), ambao walichunguza makosa ya kimofolojia na ya kisintaksia katika shule mbalimbali walipata kuwa, lugha ya Kikamba iliathiriwa na Kiswahili, moraa alichunguza makosa ya kimofolojia na kifonolojia ya Kiswahili, alipata kuwa Kiswahili kiliathiri umilisi wa Ekegusi. Naye Rapando akichunguza makosa ya kimofosintaksia katika shule za Nairobi alipata kuwa wanafunzi waliathiriwa pakubwa katika umilisi wa lugha ya Kiswahili. Tafiti hizi zinachangia kuelewa mbinu zinazotumiwa katika uchunguzi huu na namna athari zinaathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Mtaalam Chomba (2013) alichunguza athari za sheng' kwa umilisi wa lugha ya Kiingereza katika shule za mji wa Nairobi. Matokeo yameonesha kuwa sheng' iliathiri umilisi wa lugha ya Kiingereza na umilisi katika lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa kwa wanafunzi wa shule za upili.

Kwa kuhitimisha hoja hii ya maoni ya watafitiwa kuhusu athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika Kiswahili, imegundulika kuwa sheng' ina athari hasi katika Kiswahili kama ilivyo katika kubadili misimbo. Pia imebainika kuwa athari hizi zinapatikana katika misingi ya kiisimu yaani kimofolojia, kisemantiki, kisintaksia na kimsamiati. Mtindo huu haufuati sarufi ya Kiswahili kwa vile hutumia tahajia isiyo sahihi ya Kiswahili. Huu ni mtindo unaochanganya misimbo, kukata maneno na kudondosha irabu. Wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza na wa mwaka wa nne wanatumia mtindo huu katika Chuo Kikuu cha Maseno. Athari hizi ni mbaya sana kwa vile zinaathiri sarufi ya lugha ya Kiswahili na maandishi kwa ujumla. Kwa kawaida, maandishi ni kumbukumbu ya muda mrefu kuliko mazungumzo. Hivyo, kuendelea kutumia mtindo huu ni kusambaza utaratibu usiokubalika wa maandishi ya Kiswahili. Hali hii inaweza kuwa ni ishara ya kuanza kubadilika kwa lugha ya Kiswahili hasa katika maandi-

shi yake kwani kasi ya matumizi ya sheng' kwa vijana wa vyuo vikuu inaongezeka kwa nguvu kila uchao.

4.5. Changamoto ambazo wahadhiri na wanafunzi hukumbana wakati wa ujifunzaji na ufundishaji wa isimu katika lugha ya Kiswahili.

Lengo la nne ni kuchanganua changamoto ambazo wahadhiri na wanafunzi hukumbana nazo wakati wa ujifunzaji na ufundishaji wa isimu katika Kiswahili. Kwa kutumia mbinu ya hojaji na usaili mtafiti amekusanya maoni mbalimbali ya wasailiwa kuhusu changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa isimu kwa Kiswahili kupitia maswali matatu yanaulizwa. (Taz swali nambari 8, 9 na 10 kiambatisho 1,2 na 3 uk 107-111).

4.5.1. Majibu ya watafitiwa

Kutokana na majibu ambayo yametolewa na watafitiwa baada ya uchambuzi wa kina, imebainika kuwa watafitiwa wanakumbwa na changamoto nyingi katika ujifunzaji wa isimu katika lugha ya Kiswahili. Changamoto zinazotolewa zimegawanywa katika sehemu mbili: Changamoto za kiisimu na zile zisizo za kiisimu. Wahadhiri na wanafunzi wametoa changamoto ambazo zinashabihiana.

4.5.2. Changamoto za kiisimu

Changamoto za kiisimu ni zile ambazo hutokana na stadi za kiisimu. Nazo ni: Kifonolojia, kimofolojia, kisémantiki, kisintaksia na kimsamiati. Ingawa stadi hizi zilishughulikiwa katika lengo nambari tatu kwa undani, mtafiti ameamua kuchunguza mbili ambazo ni kifonolojia na kimofolojia. Makosa ya kifonolojia na kimofolojia katika fonimu, miundo ya maneno, virai na vishazi.

Mifano ya maneno;

Papa badala ya baba

Samani badala ya samahani

Rara badala ya lala

Chioni badala ya jioni

Tawa badala ya dawa

Mkomba badala ya mgomba

Hama badala ya ama

Ana badala ya hana

Huna badala ya una

Naendanga badala ya naenda

Anasomanga badala ya husoma

Wanakulanga badala ya hula.

Kutokana na matokeo haya, imebainika kuwa watafitiwa hukumbana na changamoto za kii-simu katika ujifunzaji wao. Baadhi ya watafitiwa wanaeleza kuwa wao wanatumia sauti /P/ kumaanisha /b/ katika neno *papa* badala ya *baba*. Vilevile sauti /r/ hutumika kama /l/ katika neno *rara* badala ya *lala*. Katika neno *tawa*, sauti /t/ hutumika badala ya sauti /d/ katika neno *dawa*. Mifano mingine ni, sauti /ch/ hutumika kama sauti /j/ katika neno *chioni* badala ya *jioni*. Sauti /k/ hubadilika na kuwa /g/ katika neno *mkomba* badala ya *mgomba*. Mifano mingine ni ya maneno ambayo huandikwa tofauti na Kiswahili sanifu. Kwa mfano, neno *hama* badala ya *ama*, *ana* badala ya *hana*, na *huna* badala ya *una*.

Mifano zaidi ni: *Naendanga* badala ya *naenda*, *anasomanga* badala ya *anasoma*, *anakulanga* badala ya *hula*. Changamoto hizi hutokana na lafudhi katika lugha ya kwanza.

4.5.3 Changamoto zisizo za kiisimu.

Hizi ni changamoto ambazo hazihusiani na stadi za kiisimu. Matokeo yanatokana na saili ya wahadhiri swali nambari 8, saili ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza swali nambari 9 na hoja ya wanafunzi wa mwaka wa nne swali nambari 8. Taz viambatisho uk 107-111. Matokeo ni kama yafuatayo:

- i. Ukosefu wa wahadhiri wa kutosha
- ii. Ukosefu wa vitabu vya kiisimu vilivyoandikwa kwa Kiswahili
- iii. Mielekeo ya wanafunzi
- iv. Idadi kubwa ya wanafunzi wanaosoma Kiswahili
- v. Istilahi tofauti baina ya nchi tofauti
- vi. Tafsiri za Kiingereza

Matokeo haya yameonesha kuwa wahadhiri wanakumbwa na changamoto nyingi. Ukosefu wa wahadhiri ni tatizo ambalo limetajwa. Tatizo hili linawafanya wahadhiri kuwa na kazi nyingi na hivyo kushindwa kuwashughulikia wanafunzi walio na shida mbalimbali za kiusomi, vilevile hufanya usahihishaji wa karatasi ya mitihani hasa ya jarabati ya mwisho wa muhula kuwa ngumu na wakati mwingine huchukua muda mwingi kabisa kusahihisha. Matokeo yameonesha kuwa wahadhiri huchukua muda mwingi kusahihisha kazi zao na wakati mwingine huchukua muhula mzima ndio wanafunzi wapewe matokeo ya kazi hizo. Ingawa huwa hawajui ni kwa nini lakini wao huchukulia kuwa wahadhiri huzembea katika kazi yao na ndio maana huchelewa kurudisha kazi hizo. Wanafunzi wanapochelewa kurudishiwa karatasi zao za jarabati huwa hawajui makosa wanayofanya na hivyo kutojua namna ya kurekebisha makosa haya. Hali hii inaathiri viwango vya umilisi wa kiisimu katika Kiswahili.

Hoja ya ukosefu wa vitabu vya isimu vilivyoandikwa katika lugha ya Kiswahili ni tatizo lingine ambalo watafitiwa wote wanataja. Wahadhiri wote watatu wanasema kuwa Idara ina vitabu vichache mno vya kiisimu vilivyoandikwa katika lugha ya Kiswahili. Vitabu vingi wanavyovitumiwa ni vile vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Wao hutafsiri makala haya katika lugha ya Kiswahili ili kufundishia wanafunzi wa isimu katika Kiswahili. Watafitiwa wa mwaka wa kwanza na nne wana maoni sawa na wahadhiri. Hali hii inatuelekeza kwa hoja ya sita ambapo tasfiri nyingi za Kiingereza hutumiwa na wahadhiri katika ufunzaji wa isimu katika Kiswahili. Makala mengi yaliyoandikwa katika lugha ya Kiingereza hutafsiriwa kwa Kiswahili na kufunzia isimu katika Kiswahili. Hali hii inaathiri umilisi wa kiisimu wa watafitiwa wa mwaka kwanza na mwaka wa nne. Hii ni kwa sababu tafsiri za istilahi za Kiingereza katika Kiswahili huenda ziwe tofauti na inavyokusudiwa. Utafiti wa Musau na Ngugi (1997), Buliba (1998) na Mathooko (2000) ukilinganishwa na utafiti huu unatoa maoni sawa kuhusu changamoto za ufunzaji na ujifunzaji wa isimu katika Kiswahili. Tofauti ni watafitiwa ambao wanashiriki katika utafiti huu na ule wao. Vilevile utafiti huu una nafasi ya kutathmini utoshelevu wa nadharia ya umilisi ya Lehmann katika kutafiti masuala ya ufunzaji na ujifunzaji ya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unachangia kuelewa suala la uhusiano wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili na matumizi yake kwa kurejelea nadharia ya umilisi wa kiisimu.

Kuhusu hoja ya mielekeo ya watafitiwa, matokeo yameonesha kuwa watafitiwa wenye mielekeo chanya hupenda kujifunza lugha ya Kiswahili na hivyo umilisi wao huwa wa juu. Wale wenye mielekeo hasi hawapendi kujifunza lugha ya Kiswahili na hivyo umilisi wao huwa wa kiwango cha chini. Matokeo ya saili ya wahadhiri yanaonesha kuwa watafitiwa wanaofanya vizuri katika somo la isimu katika lugha ya Kiswahili huwa na mielekeo chanya ilhali wale watafitiwa wa mwaka wa kwanza hawakuelewa suala la mielekeo na hivyo ha-

wakuweza kutoa majibu kwa swali hili. Watafitiwa wa mwaka wa nne wanalielewa suala la mielekeo na wanakubaliana na wahadhiri kwa kusema kuwa mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiswahili huweza kuathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na nadharia ya Gardner (1985) kuhusu mielekeo ya kujifunza L2, inaeleweka wazi kuwa watafitiwa walio na mielekeo chanya watapenda lugha kuliko wale walio na mielekeo hasi na watafanya bidii kujifunza lugha hiyo.

Idadi kubwa ya wanafunzi wanaosajiliwa katika idara ya Kiswahili huleta utata. Hali hii hufanya masahihisho ya karatasi za jarabati kuwa ngumu kama ilivyobainika hapo awali. Vilevile kuangazia matatizo ya kibinafsi ya mwanafunzi ya kiusomi huwa vigumu kwa sababu ya idadi kubwa ya wanafunzi ambao mhadhiri mmoja hushughulikia. Matokeo ya hojaji na saili ya wanafunzi yanakubaliana na matokeo ya wahadhiri. Watafitiwa wa mwaka wa kwanza na wa nne wanasema kuwa idadi yao kubwa huwafanya wasishughulikiwe kibinafsi na ikiwa wana shida huwa vigumu kwa mhadhiri kushughulikia kila mwanafunzi. Hali hii inaathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa.

Hoja ya istilahi tofauti katika mataifa mawili ya Kenya na Tanzania huleta utata kwa wanafunzi. Istilahi za kiisimu kutoka Kenya huenda ziwe tofauti na zile za nchi ya Tanzania. Hali hii huenda ikawakanganya wanafunzi wanapozitumia. Nchini Kenya istilahi huweza kuwa na maana tofauti na ilivyo nchini Tanzania. Wanafunzi wanapovisoma vitabu vya isimu vilivyoandikwa katika nchi hizi mbili huwa tofauti. Saili ya watafitiwa wa mwaka wa kwanza na nne wanatoa matokeo yanayofanana na wahadhiri kuhusu istilahi hizi.

Hoja ya mwisho kuhusu ukosefu wa vifaa vya kufunzia ilitokana na watafitiwa, ambapo inaonekana kuwa vifaa vya kufunzia isimu ya lugha katika Kiswahili havipo. Wanatoa mfano

kama maabara ya lugha ambayo haijajengwa katika Chuo Kikuu cha Maseno. Hali hii inatinga umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Watafitiwa wa mwaka wa kwanza na nne hawaelewi ikiwa maabara ni muhimu, kwa sababu hawakusema chochote kuhusu vifaa vya kufunzia ila ukosefu wa vitabu pekee yake. Ukosefu huu unatinga umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili kwa sababu wahadhiri wanapokosa vifaa muhimu vya kufunzia basi kazi yao huwa ngumu. Pia wanashindwa kutekeleza malengo muhimu ya somo hilo.

Kwa ujumla matokeo ya changamoto za wahadhiri na wanafunzi wanapofunzwa na kusoma umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili yanaonekana kukithiri. Makundi yote matatu yameeleza wazi changamoto hizi. Saili ya wahadhiri inatoa bayana ukosefu wa wahadhiri na vitabu, matokeo kutoka saili na hojaji yanaonesha ukosefu huu pia. Mielekeo chanya na hasi ya wanafunzi watafitiwa huweza kuathiri umilisi wa kiisimu katika Kiswahili. Watafitiwa walio na mielekeo chanya ya umilisi wa kiisimu katika lugha, matokeo yameonesha kuwa wao huwa wepesi wa kuelewa lugha haraka na hupenda kusoma lugha hiyo. Kwa mfano mtafitiwa aliye na mwelekeo chanya kuhusu umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili atakipenda na kukihusudu sana kinyume na yule aliye na mwelekeo hasi, hatakipenda na hatakihusudu.

Matokeo haya yanalingana na yale ya Babusa (2010) kuhusu mielekeo ya umilisi wa kiisimu kwa wanafunzi wa shule za upili za mji wa Nairobi na Mombasa. Watafitiwa walio na mielekeo chanya kuhusu lugha watafanya vizuri na wale walio na mielekeo hasi hawatafanya vizuri katika mtihani wa Kiswahili wa KCSE. Mawazo haya ya Babusa (kishatajwa) yanaungwa mkono na Kamau (2015) aliyechunguza mielekeo ya wanafunzi kuhusu athari za lugha ya Kiingereza, Kiswahili na sheng' kwa lugha ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Murang'a. Hata hivyo utafiti huu unachunguza umilisi wa kiisimu katika lugha ya

Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno ambao matokeo yake yanaonesha kuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wana umilisi wa kiwango cha chini kuliko wenzao wa mwaka wa nne. Matokeo ya makundi yote yanaonesha wazi kuwa idadi kubwa ya watafitiwa katika mihadhara ya kiisimu katika lugha ya Kiswahili huwa kizingiti kwa ujifunzaji wa somo la isimu katika Kiswahili. Matokeo yanaonesha kuwa wahadhiri huwa na kazi ngumu katika kusahihisha karatasi za jarabati za mwisho wa muhula kwa sababu ya idadi kubwa ya wanafunzi wanaosajiliwa katika idara kusoma isimu katika lugha ya Kiswahili. Aidha wahadhiri wanashindwa kushughulikia matatizo ya kibinafsi ya mwanafunzi kuhusu umilisi wa kiisimu kwa sababu ya idadi kubwa. Hali hii inatinga umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Istilahi tofauti za isimu katika lugha ya Kiswahili na ukosefu wa vifaa vya kufunzia ni suala ambalo huwakera wanafunzi na wahadhiri. Suala hili linazua changamoto na huathiri namna mafunzo yanatolewa. Maabara ya Kiswahili haipatikani katika Chuo na masomo ambayo wangesoma wakitumia maabara hiyo huwa hawasomi. Hali hii inaathiri umilisi wa kiisimu wa wanafunzi katika lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno.

4.6. Jinsi wahadhiri na wanafunzi wanavyokabiliana na changamoto

Mbali na malengo manne ambayo yameshughulikiwa kupitia maswali tofauti katika utafiti huu, mtafiti pia amepata fursa ya kuuliza swali la ziada kwa watafitiwa. Swali linataka watafitiwa waeleze jinsi wanavyokabiliana na changamoto za ufunzaji na ujifunzaji. Swali limeulizwa kwa kutumia mbinu ya hojaji na usaili na majibu yanayopatikana katika mbinu hizi hayakutofautiana.

4.6.1. Majibu ya watafitiwa

Majibu mbalimbali yametolewa kutokana na uchunguzi huu kama vile:

- i. Kurekebisha makosa ya wanafunzi katika karatasi za mjarabu.

- ii. Kuwashawishi wanafunzi kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zao nyingi
- iii. Kuwahimiza kuipenda isimu na kuwa mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili.
- iv. Kuhimiza kushiriki makongamano kupitia chama cha Kiswahili cha Maseno.
- iv. Kuhimiza kupitia uandishi bunifu wa insha na makala mbalimbali ya Kiswahili.

Matokeo haya yameonesha kuwa wahadhiri hufanya bidii na wanarekebisha makosa ya wanafunzi katika makaratasi yao ya mitihani. Huwashawishi wanafunzi kutumia Kiswahili katika shughuli zao nyingi wakiwa chuoni na huwahimiza kuipenda isimu na kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili, wahadhiri wanawahimiza kushiriki makongamano kupitia chama cha Kiswahili cha Maseno, wanawahimiza kupitia uandishi wa insha bunifu na makala mbalimbali ya Kiswahili. Vilevile wahadhiri wanasema kuwa wao hutafsiri makala ya Kiingereza na kuwapa wanafunzi yakiwa katika Kiswahili.

Kwa kuhitimisha hoja hii ya changamoto za ufunzaji na ujifunzaji wa isimu katika lugha ya Kiswahili, imebainika kuwa kuna matatizo aina mbili: yale ya kiisimu na yale yasiyo ya kiisimu. Matatizo haya yanaonekana kutinga umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa watafitiwa wa Chuo Kikuu cha Maseno. Tatizo la lafudhi linajitokeza na linakuwa gumu kuelewa ikiwa lafudhi ya Kiswahili sanifu ipo au haipo. Vilevile athari za lafudhi zinaonekana katika uzungumzaji wa baadhi ya watafitiwa. Wale wanaoathirika sana wanahusishwa na lugha za Bukusu, Dholuo, Kalenjin na Ekegusi.

4.7. Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu ambazo zilipatikana kwa kutumia mbinu ya hojaji, mahojiano na jarabati. Uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu. Aidha, Nadharia ya

Lehmann (2006) ya Umilisi wa Kiisimu na ya Gardner (1985) ya Motisha na Mielekeo ya kujifunza L2 inayotumika katika utafiti huu inasaidia kuchanganua data za utafiti kwa kueleza viwango vya umilisi wa kiisimu na kuonesha athari zake katika Kiswahili. Utafiti umefanikiwa kubainisha vipengee muhimu vinavyoeleza badiliko la umilisi wa kiisimu kama vile: Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha, kutositasita, kurudiarudia maneno au sentensi na wakati mwingine kunyamaza. Utafiti umeweza kufafanua sababu za kutumia sheng' na athari zake kwa umilisi wa kiisimu. Aidha umebainisha maoni ya watafitiwa kuhusu changamoto ambazo wahadhiri na wanafunzi hukumbana nazo wakati wa ujifunzaji na ufunzaji wa isimu katika lugha ya Kiswahili. Mwisho, majibu ambayo yametolewa na watafitiwa yamefanikisha kufikiwa kwa malengo yote ya utafiti huu kama yalivyopangwa. Sura inayofuata ni ya muhtasari, mahitimisho na mapendekezo.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1. Utangulizi.

Sura hii inahitimisha utafiti unaohusu “Uchanganuzi wa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili; Changamoto na udhihirifu katika Chuo Kikuu cha Maseno nchini Kenya”. Sura imegawika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza inaeleza muhtasari wa utafiti mzima. Sehemu ya pili inatoa matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Sehemu ya tatu inaeleza mchango wa utafiti. Sehemu ya nne inaeleza mapendekezo yaliyotolewa na watafitiwa kuhusu umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili na sehemu ya mwisho inapendekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

5.2. Muhtasari wa tasnifu.

Utafiti huu unachunguza “umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili; changamoto na udhihirifu katika Chuo Kikuu cha Maseno nchini Kenya. Jumla ya watafitiwa 124 wanashiriki katika utafiti huu wakiwemo wanafunzi na wahadhiri kutoka Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Maseno.

Utafiti umelenga kuchunguza mambo manne. Kwanza, kubainisha viwango vya umilisi wa kiisimu kwa wanafunzi wa mwaka kwanza na mwaka wa nne katika Chuo Kikuu cha Maseno, Kueleza vipengee vinavyoonyesha mabadiliko la umilisi wa kiisimu katika Lugha ya Kiswahili, kueleza athari za sheng’ kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno na kufafanua changamoto ambazo wahadhiri na wanafunzi hukumbana nazo wakati wa kufunza na ujifunzaji katika Chuo Kikuu cha Maseno. Mpangilio mzima wa kazi hii ulikuwa kama ifuatavyo: Sura ya kwanza inatoa taarifa zinazohusiana na mada ya utafiti. Sura iligawika katika sehemu saba. Sehemu ya kwanza imeeleza utangulizi

wa jumla wa mada ya utafiti. Sehemu ya pili imeeleza suala la utafiti. Sehemu ya tatu imetoa maswali ya utafiti. Sehemu ya nne imeeleza madhumuni ya utafiti. Sehemu ya tano imeeleza umuhimu wa utafiti. Sehemu ya sita imeeleza upeo wa utafiti na sehemu ya mwisho imeeleza misingi ya kinadharia ya utafiti.

Sura ya pili inaeleza baadhi ya kazi zilizofanywa na wataalamu mbalimbali juu ya umilisi wa kiisimu wa lugha na nadharia ambazo ziliongoza utafiti huu. Sura ya tatu nayo imefafanua namna utafiti ulivyofanyika. Sura iligawanywa katika sehemu saba. Sehemu ya kwanza imeonesha muundo wa utafiti. Sehemu ya pili imefafanua kundi lengwa. Sehemu ya tatu imeeleza eneo la utafiti. Sehemu ya nne imeeleza mchakato wa usampulishaji. Sehemu ya tano imeeleza mbinu za kukusanya na kuchanganua data. Sehemu ya sita imeeleza maadili katika utafiti na sehemu ya saba imeeleza udhabiti wa vifaa vilivyotumika katika utafiti.

Sura ya nne imewasilisha na kuchambua data ambazo zimekusanywa katika utafiti huu na sura ya tano imetoa muhtasari wa matokeo, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti. Sura imegawika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza imetoa muhtasari wa utafiti mzima. Sehemu ya pili imetoa matokeo ya utafiti huu. Sehemu ya tatu imeeleza mchango wa utafiti. Sehemu ya nne imetoa mapendekezo yaliyotolewa na watafitiwa kuhusu umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili na sehemu ya mwisho inapendekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

5.3. Muhtasari wa matokeo ya utafiti.

Muhtasari huu umepangwa kulingana na madhumuni ya utafiti ambyo ni manne.

5.3.1. Viwango vya umilisi vya kiisimu

Katika kuchunguza madhumuni ya kwanza ya utafiti huu, matokeo yanaonesha viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza huwa vya chini lakini wanafunzi wa mwaka wa nne huwa na viwango vya juu vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Sababu ambazo zimetolewa kwa hivi viwango tofauti ni kuwa, wanafunzi wa mwaka wa kwanza wanapotoka katika shule za upili wanakuwa hawajatangamana na kazi za chuo. Lakini wanafunzi wa mwaka wa nne huwa tayari wanamalizia mtaala wa isimu katika Chuo Kikuu na hali hiyo inachangia umilisi wao kuwa wa kiwango cha juu.

Matokeo ya jarabati ya wanafunzi wa mwaka wa nne yameonesha kuwa umilisi wa wanafunzi ulikuwa wa juu ingawa kuna wale ambao wanaonesha makosa ya kurudiarudia katika sentensi na wengine wanashindwa kumaliza kujibu maswali. Wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi wanapata alama 33 kwa 40 ambayo ni asilimia 82.5, na wale wa chini wanapata alama 14 ambayo ni asilimia 35. Vilevile viwango vya umilisi wa wanafunzi wa kike vimeonekana kuwa vya juu kuliko wenzao wa kiume. Utafiti umebaini kuwa kuna vigezo tofauti vya kupima umilisi wa kiisimu katika lugha. Vigezo hivi ni jarabati ya maandishi na jarabati ya mazungumzo. Vigezo vingine ni uchunguzi, usikilizaji na usomaji. Hata hivyo utafiti huu ulitumia vigezo vya kuzungumza na kuandika.

5.3.2. Vipengee vinavyoonyesha badiliko la umilisi wa kiisimu.

Matokeo ya swali hili yameonesha kuwa badiliko la umilisi wa kiisimu huonekana katika, mijarabu na jarabati ya mwisho wa muhula. Vilevile inaonekana katika uzungumzaji wa mwanafunzi anapowasilisha mbele ya wenzake. Wahadhiri wameeleza kuwa mabadiliko haya yanaonekana katika maandishi ya mitihani. Kutokana na jinsi wanavyopanga na kueleza

hoja katika mitihani hii inaonesha kuimarika au kudorora kwa umilisi wa kiisimu. Matokeo yameonesha kuwa wahadhiri wanaweza kukadiria umilisi wa wanafunzi katika mazungumzo kupitia vigezo vya kusitasita, kushindwa kujibu maswali, kurudiarudia maneno, kucheka, kunyamaza, matamshi mabaya ya maneno, kiimbo kibaya, kuchanganya na kuhamisha misimbo, kutofuata ruwaza maalumu na ung'amuaji wa maana ya maneno. Wanafunzi wanao yaonesha haya inasemekana kuwa wana umilisi wa kiwango cha chini. Kwa ujumla vigezo vitatu muhimu vinatumia kuonyesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu. Vigezo hivi ni katika mazungumzo, maandishi na usomaji.

5.3.3. Athari za sheng' kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili

Matokeo ya madhumuni haya ya tatu yamebaini kuwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili huathiriwa na matumizi ya sheng' inayotumiwa na wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Maseno. Athari hizi za sheng' kwa umilisi wa isimu katika lugha ya Kiswahili zinaonekana katika mofolojia, sintaksia, semantiki na msamiati kama inavyoelezwa katika sura ya nne.

Sababu ambazo zimetolewa na watafitiwa kuhusu matumizi ya sheng' katika Chuo Kikuu cha Maseno ni kuwa, huweza kufupisha maneno ili kuweka siri na kile wanachokisema kisijulikane na wengi. Hoja nyingine ni kwenda na wakati ambapo watafitiwa wanasema kuwa matumizi ya sheng' ni ya wakati wa sasa na hawawezi kuachwa nyuma. Vilevile utafiti umeonesha kuwa wanatumia sheng' kwa sababu ni lugha ya vijana na wanapokosa kutumia wao huonekana watu wasiostaarabika. Hoja nyingine inayotolewa ni kuwa, matumizi ya sheng' inajenga urafiki baina ya wazungumzaji na vilevile inaonesha ubunifu wa aina yake. Hata hivyo matokeo yameonesha kuwa matumizi sheng' inaathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno kwa kiwango kikubwa.

5.3.4. Changamoto za wanafunzi na wahadhiri katika ujifunzaji na ufunzaji

Matokeo ya madhumuni ya nne ya utafiti huu, yamebaini kuwa katika ujifunzaji na ufunzaji kuna changamoto nyingi. Changamoto hizi zinazowakumba wahadhiri na wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Maseno zimegawanywa katika makundi mawili, za kiisimu na zile zisizo za kiisimu. Changamoto zisizo za kiisimu ni: ukosefu wa wahadhiri wa kutosha katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, ukosefu wa vitabu vya isimu vilivyandikwa katika lugha ya Kiswahili, mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili, idadi kubwa ya wanafunzi katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, istilahi za kiisimu, makala yaliyotafsiriwa katika Kiswahili na ukosefu wa vifaa vya kufunzia kama vile maabara ya isimu.

Matokeo haya yamebaini kuwa matatizo haya hufanya ufundishaji na ujifunzaji wa isimu katika Kiswahili kuwa changamano na hufanya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kuwa wa kiwango cha chini. Matokeo yameonesha kuwa uwezo wa mtafitiwa kujieleza kwa ufasaha katika lugha ya Kiswahili na kutumia sheria za lugha hii vyema katika mazungumzo na maandishi huweza kupima umilisi wake katika lugha husika.

5.4. Mahitimisho kulingana na madhumuni

Utafiti huu umechunguza umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno na changamoto ambazo wanafunzi na wahadhiri hupitia wakati wa kusoma na kufundisha isimu katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na matokeo haya wanafunzi wa mwaka wa kwanza wanaonesha umilisi wa kiwango cha chini ikilinganishwa na wale wa mwaka wa nne. Umilisi wao umeonekana kuimarika wakati wanafunzi wanapoendelea kusoma. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa wanafunzi wanapofika mwaka wa nne kuna wale ambao huwa wameimarika katika lugha ya Kiswahili na kulikuwa na wale ambao wanakuwa na umilisi wa chini kama

inavyoonekana katika jarabati ya mwaka wa nne. Wale wanaoimarika wametoa sababu kuwa wanapenda lugha hii na wana motisha ya kusoma kwa bidii, kwa sababu wanajua kile wana-weza kupata baada ya kumaliza masomo yao.

Utafiti umeeleza kuwa vipengee vinavyotumika katika kupima umilisi wa kiisimu vilikuwa na upungufu wake kama ilivyojadiliwa hapo mbeleni ingawa ndivyo vinavyotumiwa na wa-hadhiri. Vipengee hivi vimeonesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswa-hili. Kwa mfano jarabati maandishi ni rahisi kupima umilisi wa kiisimu kuliko jarabati ma-zungumzo. Kutokana na nadharia ya Lehmann kuhusu umilisi wa kiisimu na ile ya Gardner ya mielekeo kuhusu lugha ya pili, imebainika kuwa wanafunzi wa kike wana umilisi wa ki-wango cha juu kuliko wenzao wa kiume. Hali hii inatokana na mielekeo yao chanya. Wana-funzi wa kiume wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Ili kuboresha uandikaji wa isimu na kuboresha matokeo ya mtihani wa Kiswahili, yatakikana makosa haya yarekebish-we. Kurekebisha makosa ya kisarufi kunahitaji mbinu mwafaka ambazo ni wazi kwa wana-fuzi na wahadhiri. Kulingana na madhumuni ya kwanza ya utafiti huu kuhusu viwango vya umilisi wa kiisimu, utafiti unatoa mapendekezo yafuatayo;

(i) Stadi za lugha ya Kiswahili zikiwa ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika zis-hughulikiwe ipasavyo ili kuweza kupima viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya.

(ii) Marekebisho ya makosa ya kisarufi yatakayobainishwa katika kazi za wanafunzi yaelezewe wanafunzi darasani.

(iii) Vipengee vinavyoonyesha mabadiliko ya umilisi wa kiisimu katika lugha vya paswa kuelezwa kwa wanafunzi ili waelewe na kuvitumia katika maandishi na mazungumzo yao.

(iv) Wanafunzi wanaofanya vizuri wapewe motisha ya aina yoyote ili kuzidi kuwapa

msukumo wa kufanya vizuri zaidi. Aidha, wanafunzi ambao utendaji wao si mzuri, waweze kusaidiwa ili waimarike katika umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

Vipengee vinavyoonesha badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili ni vingi. Hata mwanafunzi ambaye ataonesha kusitasita katika mazungumzo, kuchanganya na kuhamisha msimbo, matamshi mabaya ya maneno, kiimbo kibaya na kutokuwa na uwezo wa kujieleza kwa ufasaha katika lugha ya Kiswahili huonesha kuwa umilisi wake ni wa kiwango cha chini katika lugha husika. Wahadhiri wamebaini kuwa, wao hujua kuwa mwanafunzi ameimarika kupitia mijarabu na jarabati ya mwisho wa muhula. Vilevile wanaweza kuchunguza jinsi wanavyowasilisha kazi zao katika mihadhara mbele ya wenzao. Wahadhiri wanaweza kukadiria kuimarika kwao. Utafiti unapendekeza kuwa vigezo vingine vitafutwe vya kuelezea badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha Kiswahili.

Utafiti ulipata kuwa sheng' inaathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa. Utafiti ulichunguza sheng' na haukuchunguza lugha za kwanza kwa sababu haikuwa kwenye mipaka yake ya utafiti. Matokeo yamebaini kuwa matumizi ya sheng' yanaathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Athari hizi ni za kiisimu na zinahusisha stadi za kiisimu ambazo ni: i) Mofolojia ii) Sintaksia iii) fonolojia iv) semantiki na v) Msa-miati.

Sababu zinazotolewa na matokeo haya kuhusu matumizi ya sheng' ni kuwa:

- i) Kuweka mambo yao siri, ii) Kujenga urafiki, iii) Kwenda na wakati,
- iv) Lugha ya vijana na kuonesha ubunifu.

Utafiti unapendekeza kuwa lugha ya Kiswahili ihusishwe katika shughuli nyingi katika Chuo Kikuu cha Maseno na Kiswahili sanifu kitumiwe kila mara pasipo kuhamisha au kubadili

misimbo katika mihadhara ya Kiswahili ili kuimarisha umilisi wa wanafunzi katika Kiswahili. Vilevile utafiti unapendekeza kuwa wanafunzi wahimizwe kutumia lugha ya Kiswahili kwa sababu ya uzuri wake ili umilisi wao wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili uimarike.

Changamoto wanazokumbana nazo wanafunzi na wahadhiri zimeoneshwa kuwa, ukosefu wa vitabu vya kutosha vilivyoandikwa katika lugha ya Kiswahili uliathiri umilisi wa kiisimu wa wanafunzi katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wengi wanakumbana na vitabu vingi vya isimu vilivyoandikwa katika lugha ya Kiingereza na wanalazimika kusoma na kutafsiri makala haya katika lugha ya Kiswahili. Wahadhiri pia wanapatwa na mashaka yale yanayowapata wanafunzi. Wao wanalazimika kusoma makala katika Kiingereza na kuyatafsiri katika Kiswahili kabla ya kwenda kuwafunza wanafunzi. Utafiti unapendekeza kuwa waandishi wengi wa vitabu vya isimu katika Kiswahili wapewe motisha ya kuweza kuandika na kuchapisha vitabu na makala ya isimu katika Kiswahili ili yaweze kutumiwa na wanafunzi pamoja na wahadhiri wa somo la isimu katika Kiswahili. Idadi ya wanafunzi wanaosajiliwa katika idara ya Kiswahili ni ya juu na wahadhiri wanakuwa na wanafunzi wengi ambapo inakuwa vigumu kwa wahadhiri kushughulikia matatizo ya uandishi ya kila mwanafunzi. Utafiti unapendekeza kuwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaosajiliwa katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika ipunguzwe ili wahadhiri wawe na idadi ya kutosha kurahisisha ufundishaji na usahihishaji wa kazi za wanafunzi. Iwapo mapendekezo ya mtafiti yatatekelezwa, yatawanufaisha wanafunzi katika kutambua viwango vya umilisi katika lugha. Aidha, wanafunzi watanufaika kupitia kwa wahadhiri wao ambao kulingana na ushauri wao na mapendekezo ya mtafiti, watatambua kanuni za upimaji wa umilisi katika lugha ya Kiswahili. Wahadhiri wa lugha ya Kiswahili nao kupitia mapendekezo ya mtafiti, wataimarisha mbinu za ufundishaji kisha wataweza kusaidia wanafunzi kupita mitihani ya lugha ya Kiswahili. Hati-

maye, wahadhiri wanaweza kutambua njia za kupunguza na kukabiliana na aina mbalimbali za changamoto zinazowakabili.

5.5. Mapendekezo ya utafiti zaidi.

Utafiti unapendekeza kuwa tafiti zaidi zifanywe kuhusu umilisi wa vipengee vingine vya Kiswahili kama vile fasihi na ushairi. Mtafiti anapendekeza kuwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu athari za lugha za kwanza kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili na mwisho mtafiti anapendekeza kuwa utafiti zaidi ufanywe juu ya mielekeo kijinsia kuhusu umilisi wa uzungumzaji wa lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu nchini Kenya.

MAREJELEO

- Adams, D. (1993) *Defining education quality*, University of Pittsburg: USA
- Alreck, L. & Settle, R. (1995). *Survey Research handbook*. Chicago: Irwin publishers.
- Al – Juboury, N (1999). *A Language Teacher's Guide to Assessment*, Iraq: University of Baghdad.
- Baker, C. (1992). *Altitudes and Language*. Clevedon: Multilingual Matters.
- Babusa, H. (2010). *Uchanganuzi linganuzi wa mielekeo na umilisi wa wanafunzi wa Kiswahili katika mkoa wa Nairobi na Pwani*: PhD Thesis ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Buliba, L. (1998). *Utata katika istilahi za isimu ya Kiswahili*. Makala ambayo hayajachapishwa, yaliyowasilishwa katika kongamano la Kiswahili, Kenyatta University, 23-25 Septemba 1998.
- Brenzinger, M. (1998), *Endangered Languages in Africa*“ Köln: Rüdiger Kö
- [http://portal UNESCO org/culture/es/files/8283/11195176347 Language _ Vitality_and_Endangerment.pdf](http://portal.unesco.org/culture/es/files/8283/11195176347/Language_Vitality_and_Endangerment.pdf) [accessed 19. 05. 2012]
- Buschenhofen, P. (1998) “English Language attitudes of final and first university year students in Papua New Guinea”, *Asian journal of English Language no. 8*.
- Carell, D (1993) *Metacognitive strategy training for ESL reading*, USA: Wiley Browse pub, Ltd.
- Canale, M. & Merrill S. (1980) “Theoretical base of communicative approaches to second Language teaching and testing”, *International journal for applied linguistics*.
- Chassen, J. (1979). *Research Design in clinical Psychology and Psychiatry*. New York. Ardent Mechew incl.
- Clark, C. (1977). *Psychology and language*. San Diego: Harcourt Brace Publ.
- Crystal, G. (1971). *Linguistics*, England: Penguins.

- Crystal, D. (1987). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge. Oxford University press
- Cohen and Manion (1994) *Research methods in education*. London: Croom Helm
- Chomsky, N. (1965). *Aspects of the theory of syntax*. Cambridge: Mass MIT press.
- Chomsky, N. (1986). *Knowledge of language, its nature and use*. Cambridge: Mass MIT press.
- Coseriu, E. (1985). *Linguistic competence: what is really? The modern language Review*. Cambridge: Cambridge university press.
- Edwards, J. (1982). *Language attitudes and their implications among English speakers*. London: Edward Arnold.
- Ellis, R. (2004). *The definition of L2 explicit knowledge*. Language learning.
- Essa, R. (2001) *Evaluation of oral efficiency of intermediate school teachers of English*. Unpubl. MA Thesis, University of Al Mustansiriyah, college of Teachers.
- Enon, C. (1998), *Education Research and Measurement*, Department of Distance Education; Makerere University; Uganda
- Fasold, R. (1984). *Sociolinguistics of Society*. Blackwell Publishers, USA:
- Fahmy, J. & Bilton, L. (1990). *University Language Policy: Identifying Student Attitudes*. Makala Iliyowasilishwa Katika Kongamano la Ulimwengu la Isimu Tekelezi (9, Thessaloniki, Ugiriki, Aprili 15-21, 1990) Lililodhaminiwa na Chama cha Kimataifa cha Isimu Tekelezi.
- Flutcher, G. & F. Davidson. (2007). *Language Testing and Assessment: An Advance Resource Book*. New York, Routledge Taylor.
- Flick, U. (1998). *An Introduction to Qualitative Research*. London: Sage.
- Fillmore & Charles, J. (1979). *Individual differences in language ability and language Behavior*. New York: Academic press

- Fraser, B. & Nolan, W. (1981) "The association of deference with linguistic forms".
International Journal of Sociology of Language 27: 93-100.
- Friedrich, P. (2000). *English in Brazil: function and attitudes*. World Englishes.
- Furaha, J. (1991). *Matumizi ya Lugha mjini Malindi: Jinsi Mielekeo inavyoathiri Uteuzi wa Lugha*. Tasnifu ya M.A. ya Chuo Kikuu cha Kenyatta
- Gardner, R.C. (1985). *Social Psychology and Second Language Learning: The Role of Attitude and Motivation*. London: Edward Arnold.
- Gardner, R. & Smythe, P. C. (1981). *On the development of the Attitude/Motivation Test Battery*. Canadian Modern Language Review.
- Gachiri, O. (2009) *Kenyan Language Ideologies, Language Endangerment an Gikuyu (Kikuyu): How Discourses of Nationalism, Education and Development have Placed a Large Indigenous Language at Risk*. Phd Thesis: The University of Arizona (Unpublished).
- Gorman, T. (1974). *The Teaching of Languages at Secondary Level*, katika: Whitely, W.H. *Language in Kenya*. Nairobi: OUP.
- Habwe & Karanja (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi. Phoenix publ.
- Halloran, J. (1967). *Attitude Formation and Change*. Great Britain: Leicester University Press.
- Hoffman, (1977). *Empathy prosocial: Its development and application in Keasey, Nebraska symposium on motivation; vol 25 (169-218)*.
- Hashim, H. (2005). *Writing as asocial practice in higher education in Tanzania*. Unpublished PhD Thesis. Cape Town: Western Cape University.
- Hymes, H. (1971). *Competence and performance in Linguistic theory language acquisition. Models and Methods*. London & New York: Academic Press.

- Ilomak, A. (2005). *Across linguistic influence: Across sectional study with particular reference to Finnish and English speaking learners*, MA thesis unpublished UOF.
- Jokey, M. (2007). *An assessment of intermediate school Teachers English classroom*, Unpubl MA. Thesis. University of Baghdad.
- Lee, J (1994). *Ralative risk of cross sectional data*, California: Amazon pub.
- Lehmann, C. (2006). *Linguistic competence*. Erfurt. University of Erfurt publ.
- Landweer. (2000), Indicators of Ethno Linguistic Vitality'. Notes on Sociolinguistics pg 5 – 22 [Online: <http://www.s.l.org/socialx/ndg-lg-indicators.html>]
- Kamau, M, (2015) *Taathira za Kiswahili na lugha nyingine kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama: Mfano wa lugha ya Kikuyu*. Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Kamusi ya Kiingereza- Kiswahili*, (1939) Oxford University Press Nairobi.
- King'ei, K. (2000). *Research in African language*. Makala ambayo hayajachapishwa, yaliyowasilishwa katika kongamano la kwanza la lugha za kiafrika: Sunset Hotel Kisumu tarehe 10-12 Mei 2000.
- Kombo, D. & Tromp, A. (2006). *Propasal and thesis writing: An introduction*; Nairobi: Pauline publications Africa.
- Kothari, R, (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi; New Age publishers.
- Kitsao, R (2015) *Uchanganuzi wa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi katika kata ya Ganze*, Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa: Pwani University.
- Kim, Y. (2007). *Korean adults' attitudes toward varieties of English*. Unpublished MSc in Applied Linguistics. The University of Edinburgh.

- Kimemia, J. N. (2001) *KISWAHILI The Dilemma Of Developing The National Language*, Njoro, Kenya: Egerton University Press
- Kress, T. M (2008), *Critical Praxis Research; Breathing New Life into Research Methods for Teachers*, United States of America; Springer
- Massamba, D (2004), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*, Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
- McNamara, T. (2000). *Language Testing*. Hong Kong: Oxford University press.
- Massamba, D, Y Kihore & L Hokororo. 1999. *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dares Salaam: TUKI
- McNamara, T(2000). *Language Testing*. Hong Kong: Oxford University Press.
- Mathooko, M, (2002) *Kutoka lugha kienzo hadi lugha ya isimu: matatizo yanayotinga kiswahili kama lugha ya kufunzia isimu vyuoni vikuu nchini Kenya*. Makala ya Swahili forum- IX-125-133.
- Macaro, L, (2003) *Teaching and learning a second language*. A review of recent research. London: Bookcraft Ltd.
- Malhotra, K. & Birks, S. (2007). *Marketing Research: An applied approach*. London: Prentice Hall.
- Munialo (2009) *Mielekeo ya wanafunzi kuhusu matumizi ya Kiswahili katika shule za msingi wilaya Nyando*. MA thesis haijchapishwa: Moi University.
- Mutungu, (2001) *Makosa ya Kileksia katika Insha za Wanafunzi wa Kidato cha kwanza*. Tasnifu ya M.A. (UON)
- Mcdonough. S. (2002). *Applied Linguistics in language education*. G.Britain.MPG Books.
- Marshall, M. (1996). *Sampling for Qualitative Research*; Family Practice, 13(6) 522-525.
- Miguda, A. (2002). *The study of Sheng language and its influence in Eastland Nairobi*. Unpublished PhD Thesis. Maseno: Maseno University Press.
- Milroy, L. (1987). *Observing and Analyzing Natural Language: A Critical Account of Sociolinguistic Method*. Basil Blackwell: Oxford.

- Mlama, Penina & Matteru, (1977). *Haja ya kutumia Kiswahili kufundishia katika Elimu ya juu*. Dar es Salaam: Bakita.
- Mohochi, E.S (2007). *Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Lugha ya Kiswahili: Mfano wa Mikoa ya Pwani na Nyanza, Nchini Kenya*; *Lugha na Fasihi ya Kiswahili, CHAKAMA* (2007), UK 23 - 38
- Mohochi, E. (2006). *Mielekeo Ya Wanafunzi Kuhusu Lugha Ya Kiswahili Na Athari Zake Katika Matokeo Ya Mtihani Wa Kiswahili Wa Kidato Cha Nne Katika Mikoa Ya Pwani Na Nyanza, Kenya* Tasnifu Ya Uzamifu Ya Chuo Kikuu Cha Eger ton, Kenya.
- Moraa O, (2014) *Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusi*. Tasnifu ya M.A UON
- Muaka, L. (2011), *Language Perceptions and Identity among Kenyan Speakers*". In:
- Eyamba, G.B et al *Selected Proceedings of the 40th Annual Conference on African Linguistics*, (ed) Somerville, MA Cascadilla Proceedings Project pp 217-230.
- Muchemi, J.A. (2011) *Lexical and Morphosyntactic Attrition in Secondary School Students who Speak Gikuyu as L1*. Kenyatta Universty: M.A Thesis (Unpublished).
- Mbula, J. (2011) *Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia yanayofanywa na Wazungumzaji wa Kikamba wanapojifunza Kiswahili Sanifu*. Tasnifu ya M.A. (UON).
- Mparutsa, C. (1986). *An Investigation into Diglossia in Harare* (Harare, Dept. of Linguistics, University of Zimbabwe, mimeo.)
- Musau & Ngugi. (1997). *Kiswahili Research in Kenyan Universities: Where are we now*. Makala ya (Swahili forum iv)
- Mugenda, A. & Mugenda, O. (1999). *Research methods. Quantitative and qualitative approaches*. Nairobi: Acts press
- Mwangi, B (2014). *Umilisi wa stadi za maamkizi katika ujifunzaji wa Kiswahili*. Tasnifu ya uzamifu ambayo haijchapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Nicuolo, G. (1991) *Problems of Testing Communicative Performance*. Baltimore: University Park Press.

- Ngara, E. (1982). *Bilingualism, Language Contact and Planning*, Gweru: Mambo Press.
- Nunan, D. (2003). *Practical English Language Teaching*. Singapore: McGraw-Hill Education (Asia).
- Ng'ong'a, O (2002). *An assessment of University English language teacher Education in the light of classroom needs*.Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa: Maseno University.
- Newmark, P. (1966), *How to interfere with language learning*, internal journal of American Linguistics 40.
- Okwany, L. (1993). *Attitudes of high school students in Kenya toward the learning of Kiswahili*. University of New Brunswick, Fredericton, NB, Canada. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa.
- Onyango, P. (1998). *Jinsi ya kuimarisha kozi za Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya*. Makala ambayo hayajachapishwa ambayo yaliwasilishwa katika kongamano la Kiswahili lililokuwepo tarehe 23-25 Septemba, 1998, Kenyatta University.
- Onyango, J.O. (1990). *Mielekeo ya Wasomi Kuhusu Matumizi ya Kiswahili nchini Kenya*. Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Oso na Onen (2005). *Sms linguistics creativity in small screen technology*, Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa: Masai Mara University.
- Oxford English Dictionary (1974), Oxford University Press. UK.
- Patridge, N. (1996) *Motivation training to help individuals*: UK, Cambridge.
- Radford, A (1981), *Transformational syntax*, LONDON: CUP
- Ramadhan. K. (1998). *Assessing the proficiency competence of primary school teachers of English in Baghdad*. Unpul. MA. Thesis. University of Baghdad.
- Raheem. H. (2003) *Oral profficiency of primary school teachers in English in Iraq*. Unpul. MA. Thesis. An Arabic Higher institute of Education and Psychology Studies.

- Rapando, M. M. (2005) *Makosa ya Kimofosintaksia Yanayojitokeza katika Kazi za Kiswahili Zilizoandikwa na Wanafunzi wa Shule za Upili Jijini Nairobi*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijchapishwa (UON).
- Republic of Kenya, (1981). *Second University Report: Report of the Presidential Working Party (Mackay Report)*. Nairobi: Government Printers
- Richard, C & Rodgers, S (1986). *Approaches and methods in language teaching: USA*, CUP.
- Rubin, R (1992). *Assessing Speaking and Listening Competence at the College Level: The Communication Competency Assessment Instrument*. Communication Education Vol 31, pp 9-18.
- Saunders, M. & Lewis, A. (2003). *Research methods for business students*. England: Pearson Education limited.
- Ruane, J. M (2005), *Essentials of Research Methods; A Guide to Social Science Research*, Australia; Blackwell Publishing
- Seidel, J. (1998). *Qualitative data analysis*. The ethnograph V5 manual, appendix E, <http://www.qualiresearch.com/> Accessed on February 15th, 2013.
- Savignon, N. (1983). *Communicative competence, theory and practice*. New York: Mcgraw Hill.
- Siregar, F. (2009) "The language attitudes of students of English literature and English language at maranatha Christian university". *A language education policy journal of Indonesia*.
- Sigh, K. (2007), *Quantitative Social Reseach Methods*, India; SAGE Publication,
- Sherif, P. et al. (1965). *Attitude and Attitude Change: The Social Judgment Involvement Approach*. Philadelphia: W.B. Saunders Company.
- Shim, R. (2002) "Changing attitudes toward TEWOL in Korea" *Journal ofAsian Pacific Communication*, 12 (1), 143-158.
- Stern, H. (1983) *Fundamental Concepts of Language Teaching*: Oxford; Oxford University Press.

- Sultani, M. (1976). *Matatizo katika ufunzaji wa Kiswahili, A journal for language teachers in Kenya.*
- Tan, R. (1994). *The use of English in selected domains amongst first year students of the Faculty of Arts and Social sciences in the University of Malaya.* unpublished M.A. thesis. University Malaya, Malaysia.
- Tewes, U(1991), *Intergration of visual and linguistic information in spoken language.* Toronto: Wechesler pub.
- Triandis, H. (1971). *Attitude and A ttitude Change.* New York: John Wiley & Sons, Inc.
- TUKI, (1990). *Kamusi ya isimu na lugha,* Dar es Salaam:
- Vartanian, T. (2011), *Secondary Data Analysis,* New York; Oxford University Press
- Verhoeven, L. (1992) "Assessment of Bilingual Proficiency."In: L. Verhoeven & J.
- Verma, S. (1997). *Modern Linguistics, An introduction.* New Delhi: Oxford University Press.
- Walliman, N (2011), *Reseach Methods; The Basic,* London & New York; Routledge Taylor & Francis Group
- Wanyoike, P. (1978), *Vikwazo katika mafunzo ya Kiswahili Kenya.* Lugha 5-3
- Weiner, S (2000), *Perception of word likeness: Effects of segment probability,* London: CUP.
- Wendo, N. (2009), Language Policy in Kenya: Negotiation with Hegemony " *The Journal of Pan African Studies,* vol.3, no.1. pp 121 - 138
- White, L. (1959). *Motivation considered the concept of competence.* NewYork: Rockvillepike
- Widdowson, Henry G. (1973). *An applied linguistic approach to discourse analysis (Unpublished PhD dissertation).* Edinburgh: University of Edinburgh.
- Woods, D. (1995). *Attitudes towards French, national Languages, and mother tongues across age and sex in Congo.* New Jersey: African World Press,

VIAMBATISHO

Kiambisho.1. Usaili ya wahadhiri.

Usaili huu ni kwa ajili ya utafiti unaohusu “Uchanganuzi wa umilisi wa kiisimu kwa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno”. Tafadhali jibu maswali haya kwa mujibu wa uelewaji wako na kwa usahihi ili usaidie kutoa matokeo yakinifu yatakayochangia maendeleo ya Kiswahili. Majibu ya watafitiwa yatawekwa siri.

1. Unaweza kukadiria kiwango cha umilisi wa kiisimu cha mwanafunzi wa mwaka wa kwanza na mwaka wa nne?
2. Unatumia nini kukadiria viwango hivi?
3. Viwango hivi huathiri vipi umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili?
4. Ni vipengee vipi vinavyoonyesha badiliko la isimu wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili?
5. Badiliko hili huwa la kiwango kipi na vipi unaweza kukadiria badiliko hili?
6. Isimu katika lugha ya Kiswahili huathiriwa vipi na sheng’?
7. Unaweza kutoa baadhi ya mifano ya athari za sheng’ kwa umilisi wa kiisimu katika Kiswahili?
8. Unakumbana na changamoto zipi wakati wa ufunzaji na ujifunzaji wa isimu?
9. Changamoto hizi huathiri vipi umilisi wa Kiisimu wa lugha ya Kiswahili?
10. Unakabilianaje na changamoto hizi?

Asanteeni kwa ushirikiano wenu

Kiambatisho 2. Usaili ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza.

Usaili huu ni kwa ajili ya utafiti unaohusu “Uchanganuzi wa umilisi wa kiisimu kwa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno”. Tafadhali jibu maswali haya kwa mujibu wa uelewaji wako na kwa usahihi ili usaidie kutoa matokeo yakinifu yatakayochangia maendeleo ya Kiswahili. Majibu ya watafitiwa yatawekwa siri.

1. Ulipata gredi gani katika mtihani wa KCSE katika somo la Kiswahili?
2. Unaweza kukadiria kiwango chako cha umilisi wa kiisimu?
3. Kiwango chako cha umilisi wa kiisimu kinakuathiri vipi katika masomo ya kiisimu?
4. Ni vipengee vipi ambavyo huonyesha badiliko la umilisi wa kiisimu?
5. Unajuaje umeimarika katika maandishi yako?
6. Unaweza kujuaje umeimarika katika mazungumzo yako?
7. Isimu katika lugha ya Kiswahili huathiriwa na sheng’?
8. Unaweza kutoa mifano ya maneno au sentensi za sheng’ ambayo huathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili?
9. Ni changamoto zipi ambazo huathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili?
10. Mnakabilianaje na changamoto hizi wakati wa kusoma isimu katika lugha ya Kiswahili?

Asanteni kwa ushirikiano wenu

Kiambatisho 3. Hojaji ya wanafunzi wa mwaka wa nne.

Hojaji hii ni kwa ajili ya utafiti unaohusu “Uchanganuzi wa umilisi wa kiisimu kwa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno”. Tafadhali jibu maswali haya kwa mujibu wa uelewaji wako na kwa usahihi ili usaidie kutoa matokeo yakinifu yatakayochangia maendeleo ya Kiswahili. Majibu ya watafitiwa yatawekwa siri.

Weka alama kwenye kijisanduku au uandike kwa kwenye nafasi ilioachwa wazi.

1. Ulipata gredi gani ulipofanya mtihani wa KCSE katika somo la Kiswahili?

A [] A- [] B+ [] B [] B- [] C+ [] C []

2. Unaweza kukadiria kiwango chako cha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili

3. Kiwango chako cha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili kinaathiri vipi somo la kiisimu_____

4. Ni vipengee vipi ambavyo huonyesha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili?

5. Umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili huimarishwa na nini?

6. Umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili huathiriwaje na sheng’ katika

Mazungumzo _____

Uandishi _____

Jarabati _____

7. Unaweza kutoa baadhi ya mifano ya athari za sheng’ katika

i. Maandishi _____

ii. mazungumzo _____

8. Ni changamoto zipi ambazo huathiri umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili?

9. Mnakabilianaje na changamoto hizi?

Asanteeni kwa ushirikiano wenu.

Kiambatisho. 4. Jarabati ya mwaka wa nne

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Maseno. Jarabati hii ni ya kufanyia utafiti na kuboresha ufunzaji wa Kiswahili pekee. Mchango wako utatumiwa kama data ya kuandikia tasnifu. Taarifa zote zitazingatiwa kwa usiri wa hali ya juu. Muda; Saa moja.

Maagizo. Jibu maswali yote kwa karatasi uliopewa

1. Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya mstari

- i) Nyumba ilijengwa na mwashi aliyehitimu.
- ii) Mtoto aliupiga mpira uliokuwa mweusi.

2. Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya matawi.

- i) Baba huyu analima vizuri ilhali mjomba anafyeka nyasi.
- ii) Wale wote wameondoka leo lakini hawa wengine watasafiri jumamosi.
- iii) Sisi sote tuliohitimu juzi tumetuzwa zawadi.

3. Changanua sentensi hizi kwa njia ya majedwali.

- i) Yeye ni mwerevu ingawa mimi simpendi moto huyu.
- ii) Mwizi aliyetorokea msituni jana usiku amepatikana leo alfajiri.
- iii) Mwanafunzi ambaye alimpiga mama amepelekwa mahakamani.

Asanteni.

Kiambatisho 5a. Muhtasari wa jarabati (wasichana)

Alama	Gredi	Marafukizi	Asilimia %
0- 29	E	2	09
30-34	D-	2	09
35-39	D+	3	13.5
40-44	C-	2	09
45-49	C	1	4.5
50-54	C+	5	22.7
55-59	B-	0	00
60-64	B	3	13.6
65-69	B+	3	13.6
70-74	A-	1	4.5
75-100	A	0	00
Idadi	12	22	100

Chanzo ; Matokeo ya jarabati ya mwaka wa nne.

Kiambatisho 5b. Muhtasari wa matokeo ya wavulana

Alama	Gredi	Marafukizi	Asilimia %
0- 29	E	3	16.6
30-34	D-	2	11.1
35-39	D+	1	5.5
40-44	C-	1	5.5
45-49	C	1	5.5
50-54	C+	0	00
55-59	B-	2	11.1
60-64	B	4	22.2
65-69	B+	3	16.5
70-74	A-	1	5.5
75-100	A	0	00
Idadi	12	18	100

Chanzo; Matokeo ya jarabati ya mwaka wa nne.

Kiambatisho 5c. Kibali cha kushiriki katika utafiti

Mimi----- nakubali kushiriki katika utafiti huu bila kushurutishwa
na mtu yeyote na nitatoa maoni yangu kwa uaminifu. Ewe mwenyezi Mungu unisaidie.

Jina la Mtafitiwa-----

Umri wake-----

Darasa-----

Tarehe-----

Sahihi-----

Maoni yako yatawekwa siri na mtafiti na hayatatolewa kwa vyovyote vile.

Mtafiti-----

Sahihi-----